# UCHUMI WA VIWANDA NA UCHUMI WA KITAIFA: DHANA, MAANA NA UZOEFU WETU

# UCHUMI WA VIWANDA NA UCHUMI WA KITAIFA: DHANA, MAANA NA UZOEFU WETU

## Zimekusanywa na Kuhaririwa na Ng'wanza Kamata

**Kutoka Kavazini Na. 2**

**2018**



Mwalimu Nyerere akiweka jiwe la msingi la Kiwanda cha Urafiki kilichojengwa kwa msaada wa China mwaka 1966

Kimechapishwa na Kavazi la Mwalimu Nyerere
Toleo la kwanza 2018
© Kavazi la Mwalimu Nyerere

ISBN: 978-9976-9903-8-6

Kitabu hiki kimechapishwa kwa hisani ya
Rosa Luxembourg Stiftung (RLS) inayofadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Kijerumani.

Kimechapwa na Inter Press of Tanzania Ltd. Dar es Salaam.

# DIBAJI

Kavazi la Mwalimu Nyerere, lililo chini ya Tume ya Sayansi na Teknologia, limepanga kuandaa mijadala, midahalo na kozi fupi kuhusu uchumi wa viwanda katika muktadha wa ujenzi wa uchumi wa kitaifa kama programu yake ya 2018. Ni matumaini yetu kwamba tutakuwa na mijadala mipana na ya kina kuhusu dhamira ya nchi yetu kuelekea kwenye maendeleo yaliyo huru na endelevu kwa manufaa na maslahi ya walio wengi. Dhana ya uchumi wa kitaifa ni muhimu kwa nchi kama yetu ambayo ilikuwa chini ya himaya ya ubeberu katika sura zake mbali mbali, pamoja na ukoloni mkongwe, ukoloni mambo leo na sasa uliberali mamboleo. Sura hizi mbali mbali hatimaye zimejikita katika mfumo wa kibepari wa kimataifa ambao kila mara, kutokana na uhalisia wa mapambano ya wanyonge, hubadili rangi zake ilhali ukiendelea kunyonya jasho la wavuja jasho na rasilimali za nchi za dunia ya tatu. Bila kuelewa ukweli huu inakuwa vigumu kutambua mbinu na viini vya mfumo wa kibepari. Hatimaye, safari ya kujenga uchumi wa kitaifa ulio huru, endelevu na kwa faida ya wanyonge ni safari ya kujikomboa kutoka uchumi tegemezi kuelekea kwenye uchumi na jamii inayojitegemea. Ni safari ya ukombozi.

Mjadala kuhusu uchumi wa viwanda hauwezi kukamilika bila kuelewa historia yetu na hasa uzoefu wetu wa jitihada zilizofanyika enzi ya Mwalimu kujenga uchumi na siasa huru inayojitegemea. Katika kijitabu hiki tumekusanya nyaraka mbali mbali kama kianzio cha kujadili tulikotoka. Tuzisome kwa makini, tuzitafakari hoja mbali mbali katika muktadha huu mpya wa nchi yetu na hali ya dunia ilivyo sasa.

Matajario yetu ni kwamba mtaendelea kushiriki katika matukio mbali mbali ya Kavazi ili katika ujumla wetu tuweze kuendeleza dhamira na malengo yetu ya kujenga nchi tunayotaka na tutakayorithisha kwa vizazi vijavyo.

**Issa Shivji**
Mkurugenzi
Kavazi la Mwalimu Nyerere
Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| Dibaji | | v |
| Utangulizi | *Issa G. Shivji* na *Ng'wanza Kamata* | viii |
| Mafanikio yetu chini ya Azimio la Arusha | *Julius K. Nyerere* | 1 |
| Kujenga Msingi wa Uchumi wa Ujamaa wa Taifa Linalojitegemea | *Mwongozo 1981* | 14 |
| Hotuba ya Mwenyekiti Mkutano Mkuu wa CCM 1982 | *Julius Nyerere* | 25 |
| Hotuba ya Mjumbe wa Mkoa wa Arusha Katika Mkutano Mkuu wa CCM 1982[1] | *Edward M. Sokoine* | 58 |
| Jitihada Zetu zilenge Kujitoa katika Hali ya Uchumi Tegemezi | *Julius Nyerere* | 80 |


[1] CCM 1987 Majadiliano ya Mkutano Mkuu wa Kawaida Oktoba, 1982: Taarifa Rasmi; Dodoma, Idara ya Uenezi na Ushirikishaji Umma. Uk.353-371.

# Utangulizi

## Tathmini ya Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda Katika Muktadha wa Ujenzi wa Uchumi wa Kitaifa

*Issa G. Shivji na Ng'wanza Kamata*

Viwanda, ndio suala linalotamba hivi sasa katika majukwaa ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii ndani na nje ya Tanzania. Toka iingie madarakani mwaka 2015, Serikali ya Tanzania, chini ya Uongozi wa Rais John Pombe Magufuli, imekuwa ikihimiza ujenzi wa viwanda vipya na ufufuaji wa viwanda vya zamani. Barani Afrika kwa ujumla Umoja wa Afrika, mwaka 2015, ulipitisha Dira ya Maendeleo (Vision 2063), ambapo suala la maendeleo ya Viwanda limepewa umuhimu wa kipekee katika azma ya kujenga Afrika Tuitakayo (*The Africa we Want*), Afrika yenye maendeleo na ustawi mkubwa kwa watu wake. Mwelekeo huu wa kufikiria maendeleo na kuwa viwanda ni njia mojawapo ya kuharakisha maendeleo ya nchi na watu wetu linatia moyo na hamasa ya kufanya tathmini na kujadili zaidi fikra na ajenda ya maendeleo ya Tanzania na nchi za Afrika. Hii ni kwa sababu katika miongo zaidi ya mitatu iliyopita suala la maendeleo na viwanda lilikuwa limewekwa pembezoni sana, na soko huria ndio lilionekana jibu la matatizo yetu yote. Muda ni mwalimu mzuri, na ni wazi kuwa soko si jibu la matatizo ya maendeleo yetu, na kwamba lazima kujifunza kutokana na makosa tuliyoyafanya huko nyuma.

Kihistoria, hoja na ajenda ya viwanda si mpya. Na hii si katika Tanzania tu bali katika bara la Afrika na nchi nyingi za dunia ya tatu. Katika Afrika, mara tu baada ya uhuru, mwanzoni mwa miaka ya 1960, suala la ujenzi wa viwanda lilipewa msukumo mkubwa sana kama njia ya kusukuma haraka maendeleo ya nchi changa na zilizokuwa nyuma kimaendeleo. Nadharia za kuleta usasa (*modernization theory*) zikaongoza mwelekeo wa aina ya maendeleo ya kipindi hicho cha awali cha maendeleo ya Afrika.

Wanazuoni wa nadharia za kuleta usasa, kwa nyakati hizo, hasa Rostow na Parson, walisukuma nadharia iliyodai kuwa umasikini na kukosekana kwa maendeleo kwa nchi za Afrika lilikuwa ni jambo la kawaida ambalo nchi zingine zilizoendelea pia ziliwahi kupitia. Nadharia hii ikadai kuwa umasikini wa nchi hizi haukutokana na miongo mingi ya nchi za kiafrika kutawaliwa na kunyonywa na mataifa yaliyokuwa yakiwatawala. Rostow na Parson wakadai kuwa ili nchi za Afrika ziweze kuendelea sharti zianze kujenga sekta za kisasa za maendeleao, na sekta mojawapo kuu ilikuwa ni viwanda. Wakadai kuwa kwa vile nchi hizi zilikuwa zinaingia katika harakati za maendeleo wakati kulikuwa na nchi zilizowatangulia kimaendeleo, hasa Ulaya na Marekani, basi nchi hizi zingeweza kupiga hatua za haraka sana katika kuondokana na umasikini na hali duni za maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kwa vile nchi zilizoendelea zitasaidia mataifa haya madogo na masikini kuendelea. Baadhi yao, kama kina Hyden, wakahimiza kuwa Afrika lazima ikimbie wakati wengine wakitembea, na moja ya njia za kufikia azma hiyo ilikuwa ni kuwadhibiti wakulima, kwa kuwaweka chini ya utawala wa tabaka la kibepari, kwa vile wakiachwa huru watakuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo. Kina Rostow, Parson, na Hyden kwa namna moja walikuwa wakisema kuwa njia ya kibepari ndio itakayoziletea maendeleo nchi masikini, na mitaji kutoka nje ndio itakuwa chachu ya maendeleo hayo. Aidha, walilenga kusaidia kundi dogo la watu wa nchi hizi, waliokuwa wamestaarabika, ‘wasasa’ (*modern*), kuwa washirika wa njia hiyo ya maendeleo.

Mwitikio mkubwa wa ujenzi wa viwanda katika nchi za kiafrika ulifuatia. Viwanda vingi vilijengwa kati ya miaka ya 1960 na 1970, kwa pesa ya ndani au ya kukopa nje. Mkakati wa awali wa viwanda ukawa ni ule wa viwanda ambavyo vingepunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa bidhaa zilizoagizwa nje kwa kuzitengeneza ndani. Shabaha ya kufanya hivyo ilikuwa ni kujiwekea akiba ya fedha za kigeni kwa ajili ya shughuli zingine za maendeleo. Haikuchukua muda mrefu mkakati huu ulishindwa kwa sababu

viwanda hivi badala ya kuleta nafuu iliyotarajiwa viligeuka kuwa mzigo mkubwa kwa wazalishaji, hasa wakulima.

Kabla hata haujaanza kutekelezwa mkakati huu ulipingwa sana na wanazuoni wa maendeleo wa kizalendo na wa kimapinduzi, ambao waliona kuwa mkakati ulikuwa haotoi mwanya wa nchi hizi kujikomboa. Mkakati ulipingwa kwa sababau haukuwa umelenga kubadili muundo na mfumo wa uzalishaji katika nchi zilizotawaliwa, na usingeweza kukomesha mahusiano ya kitegemezi na kinyonyaji kati ya nchi zilizokuwa makoloni na nchi za kibeberu zilizokuwa zikiwatawala. Uchambuzi uliofanywa na wanazuoni hawa ulionyesha kuwa uchumi wa nchi zote za Afrika ulitokana na mfumo wa kikoloni, ambao ulijengeka katika misingi ya utegemezi. Kwa hivyo mara baada ya uhuru uchumi wa nchi za kiafrika, kama anavyobainisha Edward Sokoine katika moja ya hotuba zake, ulikuwa ni uchumi wa kikoloni mamboleo. Tatizo la msingi la uchumi wa aina hii, ambao Nyerere anauita 'uchumi kilema,' ni **utegemezi nje ya nchi.** Na utegemezi huu unachukua sura ifuatayo: utegemezi wa soko la nje kwa bidhaa zinazozalishwa ndani, utegemezi wa mitaji ya kuwekeza kwenye maendeleo, na ushauri wa kitaalamu. Na sura ya uchumi huu tegemezi ni:

*Kwanza*: Sekta kuu ya uzalishaji ni ile ya Uzalishaji wa Mali ghafi (extractive industry), hasa kilimo, madini, na mali asili zingine;

*Pili*: sehemu kubwa ya mazao yatokanayo na sekta hiyo ya uzalishaji wa mali ghafi hutegemea sana soko la nje;

*Tatu*: sehemu kubwa ya mahitaji ya bidhaa za viwanda kwa walaji wa ndani huagizwa kutoka nje – badhaa kama vile mafuta ya kula, nguo, viatu, na madawa;

*Nne*: kwa sehemu kubwa sekta ndogo ya viwanda iliyopo hufanya kazi ya uchakataji wa mazao ya sekta kuu kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa hizo nje; na

*Tano*: hakuna uhusiano na uwiano wa sekta ya uzalishaji mali ghafi na ile ya viwanda, kwa mfano kilimo na viwanda.

Aina hii ni tofauti sana na sura ya uchumi wa kitaifa na unaojitegemea. Samir Amin, aliwahi kubainisha sekta kuu nne za uzalishaji katika uchumi. Sekta ya kwanza ni ile ya uzalishaji wa bidhaa za kuzalishia mali – mashine na mitambo; pili, uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya mahitaji ya walaji wengi (*goods for mass consumption*); tatu, uzalishaji wa bidhaa za anasa – kama vile utalii, vinywaji baridi n.k; na nne, uzalishaji kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje. Katika nchi zenye uchumi ulioendelea na unaojitegemea, upo uwezekana wa kuwa na sekta kuu zote zikitegemeana, aidha sekta ya uzalishaji wa bidhaa za kuzalisha mali na ile ya uzalishaji wa mahitaji ya msingi ya watu wengi – kama vile nguo, chakula, na malazi – huwa zimeendelezwa vya kutosha. Tofauti na nchi zenye uchumi tegemezi ambapo sekta zilizoendelezwa ni zile za uzalishaji wa bidhaa za anasa (zisizo za msingi) mathalani huduma zote zinazohudumia utalii, bidhaa kama pombe n.k.; na sekta nyingine ni ile ya uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kusafirisha kwenda nje – ambayo kwa kiasi kikubwa imetawaliwa na bidhaa za kilimo na madini. Bidhaa hizi ama husafirishwa nje zikiwa hazija chakatwa kabisa au kuwa zimechakatwa kwa kiasi kidogo (*semiprocessed*) – lakini huko zinakosafirishwa hutumika kama mali ghafi katika viwanda. Kwa kiasi kikubwa sura hii inashabihiana kabisa na sifa na sura ya uchumi tegemezi iliyoainishwa hapo awali.

Kundi la wasomi wa kimapinduzi lilisisitiza kuwa ili nchi za Afrika ziweze kujenga uchumi wa kitaifa na unaojitegemea sharti kuu la kwanza lilikuwa ni kuendeleza sekta ya uzalishaji wa viwanda vya kuzalisha mashine na mitambo, na sekta ya uzalishaji wa bidhaa za matumizi ya watu walio wengi katika nchi. Aidha, kuwepo uwiano mkubwa baina ya uzalishaji wa viwandani na kilimo. Kwa muhtasari sifa kuu za uchumi wa kitaifa ni kama zifuatazo: Sifa kuu ya kwanza ni uzalishaji unaolenga kukidhi mahitaji ya ndani – chakula, mavazi, malazi, madawa, na mitambo na mashine itakayosaidia uzalishaji wa mahitaji hayo ya ndani; pili, uzalishaji katika viwanda unaotegemea zaidi malighafi kutoka ndani na sio nje; tatu, matumizi makubwa ya rasilimali WATU wa ndani na sio

wataalamu kutoka nje; na nne, mahusiano ya kutegemeana baina ya shughuli za kilimo na viwanda. Ni muhimu kuzingatia kuwa uchumi wa kitaifa umejikita zaidi katika uzalishaji na sio uchuuzi. Shughuli za biashara na huduma zingine japo ni muhimu lakini msingi wake ni uzalishaji.

Hoja na mgongano huu wa mawazo ulitawala sana mijadala ya miaka ya 1960 na 1970, kabla ya mijadala hiyo kudhoofishwa na sera za ubepari wa kiliberali uliokumbatiwa na serikali nyingi za nchi zetu. Mkazo ukawekwa katika soko huria lisilo na udhibiti kwa hoja kuwa soko ndio lenye uwezo wa kugawa na kuelekeza rasilimali ziende wapi na kutumika kwa tija; sekta binafsi ikapewa nafasi ya mstari wa mbele kama kiongozi mkuu katika ukuaji wa uchumi, na tukaaminishwa kwamba ni sekta binafsi pekee itakayotengeneza ajira, kuongeza tija katika uzalishaji, na kuongeza ubora wa maisha ya watu; tukaaminishwa pia kwamba sekta ya umma/dola haikutakiwa kabisa katika uchumi kwa sababu ilikuwa inawabebesha tu mzigo walipa kodi, dola ikatakiwa ikae pembeni isipokuwa pale tu ilipohitajika katika kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya sekta binafsi kufanya mambo yake; aidha ili kuiwezesha sekta binafsi kuwepo, ubinafsishaji wa sekta ya umma ukapewa msukumo mkubwa. Matokeo ya yote haya ni kinyume kabisa na matumaini na matarajio yaliyojengwa – viwanda vingi vilifungwa au kuuliwa; sekta binafsi ikajielekeza zaidi katika shughuli zenye kupata faida kubwa na ya haraka na sio ujenzi wa viwanda, ajira hazikuzalishwa kama ilivyotarajiwa, na hali za maisha hazikubadilika, na vijana wengi wakakosa kazi. Hii ndio hali iliyojitokeza na ndio iliyopo kwa hivi sasa katika nchi zetu nyingi.

Ni katika muktadha huu suala la ujenzi na uendelezaji viwanda limekuja. Hii ni fursa nzuri ya kutafakari kwa kina na makini wapi tunakotoka, wapi tulipo, wapi tulijikwaa, nini tunaweza kujifunza kutokana na uzoefu wetu wenyewe wa kujiletea maendeleao, kujenga na kuendeleza viwanda siku zilizopita. Katika kujaribu kujibu baadhi ya masuala hayo kitabu hiki kinafanya rejea kidogo ya namna suala la ujenzi wa uchumi wa kitaifa lilivyofikiriwa na

kushughulikiwa katika nyakati mbalimbali hapa nchini. Hotuba na nyaraka nyingine zinazochapishwa katika kitabu hiki zitasaidia kuonyesha fikra na mitazamo, mipango, uzoefu, na matatizo mbalimbali yaliyozikumba jitihada za awali za ujenzi na uendelezaji wa viwanda nchini. Baadhi ya masuala yanayozungumziwa katika nyaraka zilizomo katika kitabu hiki yanakumbusha hoja kinzani juu ya masuala mbalimbali yaliyohusu ujenzi na uendelezaji uchumi wa nchi zetu, na hususan ujenzi na uendeleaji wa viwanda na mahusiano ya sekta hiyo na sekta zingine kuu hasa kilimo. Baadhi ya masuala yanayoibuka katika nyaraka hizi ambayo ni wazi bado yana umuhimu wake hata leo tunapozungumzia suala la ujenzi wa viwanda ni haya yafuatayo:

- Ni aina gani ya viwanda vinahitajika kujengwa katika nchi yetu – baina ya vile vya kuzalisha bidhaa za kuzalisha mali na vile vya kuzalisha bidhaa kwa ajili ya walaji wengi, au viwanda vya kuzalisha bidhaa za kifahari na anasa?
- Shabaha ya ujezi na uendelezaji wa viwanda ni ipi – kupunguza uagizaji wa bidhaa toka nje na matumizi ya fedha za kigeni (*import substitution*) au kujenga uwezo wa kujinasua katika hali ya utegemezi (yaani ujenzi wa uchumi wa kitaifa)?
- Je viwanda tunavyojenga ni kwa ajili ya mahitaji ya ndani au kusafirisha bidhaa kwenda nje (uchuuzi)?
- Ni teknolojia ipi inayofaa, ile ya kisasa na yenye kuhitaji nguvu kazi kidogo au teknolojia rahisi na yenye kuhitaji nguvu kazi kubwa?
- Na je upo uhusiano kati ya ujenzi na maendeleo ya viwanda na uendelezaji wa sekta ya kilimo?
- Na ni nani hasa kiongozi katika ujenzi wa maendeleo ya viwanda (*captain of industrialisation*) sekta binafsi (mtaji toka nje), sekta binafsi (mtaji wa ndani), dola, au wote?

Baadhi ya masuala haya yanajitokeza kwa namna na mitazamo mbalimbali katika nyaraka zilizochapishwa humu ambazo ni Hotuba na Taarifa ya Mwalimu Julius Nyerere kwenye Mkutano Mkuu wa TANU, juu ya utekelezaji wa Azimio la Arusha baada ya

Miaka Kumi; hotuba hii ilitolewa mwaka 1977; Mwongozo wa 1981 na Tathmini yake juu ya utekelezaji wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea; Hotuba na Taarifa ya Mwenyekiti wa CCM, Mwalimu Julius Nyerere, kwenye Mkutano Mkuu wa CCM, Miaka mitano baada ya CCM kuzaliwa, aliyoitoa mwaka 1982; Hotuba na Mchango wa Edward Moringe Sokoine, akiwakilisha Mkoa wa Arusha, kwenye hotuba ya Mwalimu Nyerere kwenye mkutano Mkuu wa CCM wa mwaka 1982; na Hotuba ya Mwalimu Nyerere, kwenye Semina ya Wazalishaji aliyoitoa Mwaka 1989. Moja ya sifa ya nyaraka zilizomo katika kitabu hiki ni tafakari ya wazi, kina, na ya kujikosoa juu ya nia na shabaha, matatizo, na makosa yaliyofanyika katika ama kubuni au kutekeleza mipango iliyokusudiwa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mathalani, katika hotuba yake ya Mwaka 1977, miaka kumi baada ya Azimio la Arusha, Mwalimu Nyerere anaonyesha jitihada kubwa zilizofanyika katika ujenzi wa viwanda baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Kilichofanyika si utaifishaji tu wa baadhi ya viwanda vilivyokuwepo bali juhudi kubwa ilifanyika ya kujenga viwanda vipya. Shabaha kuu mbili za ujenzi na uendelezaji viwanda wakati huo zilikuwa kwanza, uzalishaji wa mahitaji ya wananchi walio wengi, na pili, uuzaji nje bidhaa zilizochakatwa na kuongezewa thamani. Katika miaka kumi baada ya Azimio la Arusha tayari kulikuwa na viwanda vikubwa vya kutengeneza vitu mbali mbali kama zana za kilimo, magurudumu ya motokari, mbolea, radio, beteri na baiskeli, na saruji, na mitambo ya uchapishaji.

Lakini ilikuja kubainika kwamba viwanda hivi vilikuwa tegemezi kwa kiasi kikubwa. Vilihitaji sehemu kubwa ya malighafi toka nje, na hivyo kusababisha mahitaji na matumizi makubwa ya fedha za kigeni. Katika hotuba yake ya mwaka 1982, kwenye mkutano mkuu wa CCM, miaka mitano tu baada ya hotuba yake ya 1977, Mwalimu Nyerere anabainisha kuwa sehemu kubwa ya viwanda hivi vilikuwa havitumii uwezo wake wote kwa asilimia 100. Vingi vilikuwa

vikifanya kazi chini ya uwezo wake. Mwalimu aliendelea kueleza: [hotuba 1982].

> Karibu viwanda vyetu vyote vinafanya kazi chini ya uwezo wake, wakati mwingine vinatengeneza chini ya asilimia 50 ya bidhaa ambazo zingeweza kutengenezwa kwa kutumia mitambo hiyo hiyo. Hata mitambo ya bia imetumia asilimia 68 tu ya uwezo wake mwaka 1975; Tegry Plastics ilitumia asilimia 46, na Maziwa ya Mara chini ya asilimia 30 ya uwezo wake. Vile vile kiwanda cha saruji cha Wazo hakitengenezi saruji ukomo wake, kama kiwanda hicho kingekuwa kinafanya kazi sawa sawa; na pengine viwanda vya nguo vigeweza kuongeza kiasi cha nguo kinachotengenezwa. Mwaka 1975 kiwanda cha Bora kilikuwa kinatengeneza viatu vichache zaidi kulingana na uwezo wa mitambo yake, na tena havikuwa vizuri.[1]

Katika hotuba hiyo hiyo Mwalimu Nyerere anabainisha na kukiri chanzo na asili ya tatizo lilokumba viwanda vyetu:

> […] makosa yetu ya awali sasa yameanza kutototoa. Tumefanikiwa kujenga viwanda, lakini vile vile tumepata funzo. Karibu viwanda vyetu vyote tulivyovijenga tokea 1967 (maana hatukuwa tumeanza kabla ya hapo) vilijengwa kwa namna ambayo vinategemea sana vifaa vya kuagizwa kutoka nchi za nje. Wakati mwingine bidhaa zinazotengenezwa zinatumika badala ya zile zilizokuwa zinaagizwa kutoka nje […]. Lakini hakuna kiwanda hata kimoja ambacho kinaweza kufanya kazi kutwa bila kuhesabu mafuta ambayo tunayaagiza pia. Viwanda vingi vikubwa vinategemea utaalamu wa uendeshaji kutoka katika nchi za nje vile vile.[2]

Kimsingi, Mwalimu Nyerere anasema, asili ya tatizo la viwanda vikubwa vilivyoanzishwa toka mwaka 1967 lilikuwa utegemezi mkubwa toka nje – mali ghafi, na utaalam. Kwa maana hii ya utalaamu, Mwalimu Nyerere anabainisha kuwa teknolojia iliyotumika katika viwanda vilivyoanzishwa ilikuwa ni ghali na ya utaalamu wa juu kiasi kuwa watu wetu wenyewe hawakuwa na utaalamu wa kuendesha na kusimamia uendeshaji wake, aidha kila tulipohitaji vipuri ilibidi pia tuviagize kutoka nje.

Mwalimu Nyerere pia alilinganisha ufanisi na gharama za uendeshaji wa viwanda vikubwa na vile vidogo vidogo, vilivyoanzishwa chini ya Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo yaani SIDO. Viwanda vya SIDO vilikuwa vimeanzishwa mijini na vijijini. Mpaka kufikia mwaka 1982 kulikuwa na Viwanda vidogo vidogo 3,978 na kati ya hivyo viwanda 1,483 vilikuwa vijijini. Katika kipindi hicho, ambacho kilikuwa ni cha matatizo makubwa ya kiuchumi, ilibainika akuwa:

> [ ] hata kabla ya matatizo ya fedha za kigeni, ufanisi wa kila mtu ni mkubwa zaidi katika kiwanda kidogo kuliko kiwanda kikubwa au cha kati. Kwa mfano, katika mwaka 1976/77 mfanyakazi katika kiwanda kidogo alikuwa akitoa bidhaa zenye wastani wa thamani ya shilingi 16,110 kwa mwaka. Katika viwanda vyetu vikubwa vilikuwa kila mfanyakazi aliweza kutoa bidhaa za thamani ya shilingi 14,172 kwa mwaka, ingawa katika viwanda hivyo kuna zana za gharama kubwa sana, kwa hoja ya kwamba kiwanda cha namna hiyo kitafanya bidhaa kwa gharama ndogo zaidi! Vile vile utoaji mali katika viwanda vidogo umeathirika kwa kiwango kidogo zaidi kuliko ilivyo katika vile viwanda vikubwa. Viwanda vya SIDO vinatumia asilimia 3 tu ya malighafi zote zinazoagizwa kutoka nje zinazotumiwa katika viwanda vyote kwa ujumla.[3]

Kutokana na uzoefu huu Mwalimu Nyerere alisisitiza kuwa ingefaa, toka wakati huo, kusisitiza uendelezaji wa viwanda vidogovidogo kwa vile si tegemezi kama vile vikubwa.

Suala jingine linalojitokea wazi katika nyaraka hizi ni uongozi katika ujenzi na uendelezaji viwanda, na chanzo cha rasilimali ya kusaidia kujenga na kuendeleza viwanda. Tokea mwishoni mwa miaka ya themanini na kuendelea mpaka leo, suala la ujenzi wa uchumi limeongozwa na hoja kuwa sekta binafsi ndio kiongozi katika uchumi. Na hivi leo tunapozungumza kujenga viwanda, sekta binafsi inapewa nafasi kubwa kuliko dola. Katika suala hili Mwalimu Nyerere alidhani kwamba suala la ujenzi na uendelezaji wa viwanda lazima liwe na shabaha zinazoeleweka na zenye malengo ya kitaifa. Hili lisingeachiwa sekta binafsi, ni la dola. Dola lazima iwe mstari wa mbele kutoa uongozi. Mwalimu alikuwa na mashaka na sekta binafsi kwa sababu kazi yake ni kunyonya na kujiongezea faida. Mwalimu Nyerere anabainisha kwamba wakati ule ingewezekana kabisa kuvutia uwekezaji toka nje lakini matokeo yake yangekuwa ni kujengwa kwa viwanda ambavyo visingezalisha bidhaa zinazohitajika nchini au kwa watu walio wengi, na kwamba visingeweza kutumia kwa ukamilifu mazao ya Tanzania. Kwa mantiki hii Mwalimu Nyerere anasema sekta binafsi inaweza kujenga viwanda, lakini si vyenye manufaa katika shabaha za nchi. Japo Mwalimu anazungumzia miaka ya 1960 hadi 1980, hali hii ni bayana katika nyakati hizi, kwa sababu viwanda vichache vilivyojengwa katika zama za soko huria ni ama vile vilivyotumia fursa ya soko la nje, kama la AGOA, kuja kuwekeza nchini ili waweze kuzalisha na kusafirisha bidhaa nje (bidhaa ambazo hazina uhusiano kabisa na soko la ndani); ama vinavyoagiza bidhaa zilizokwisha chakatwa na hivyo kuvipitisha tu viwandani ili kuonekana vimezalishwa humo na kukwepa kodi, kama ilivyo katika baadhi ya viwanda vya mafuta ya kula. Viwanda vya namna hii havikidhi shabaha ya ujenzi wa uchumi wa kitaifa kwa sifa tulizobainisha awali.

Miaka saba baadae, baada ya hotuba yake ya mwaka 1982, na hasa baada ya sera za ulegezaji masharti ya kiuchumi kuanza, Mwalimu Nyerere aliona uwezekano wa ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi. Lakini kwa maoni yake, sekta hiyo binafsi inahusu wananchi wa Tanzania na sio kutoka nje, na kuwa sekta hiyo binafsi ya kitaifa itashirikiana na sekta ya ‘umma’ kupambana na mitaji kutoka nje. Kwa kirefu Mwalimu Nyerere alifafanua:

> Tutazidi kuongeza sekta ya umma na kuifanya imara … Lakini sekta ya binafsi ipo tangu 1967 na kabla, sasa fanyeni kazi nzuri lakini tukabiliane na watu wa nje kwa pamoja. Mtu ambaye tutamkataa sisi ni yule ambaye kazi yake yeye ni kutufanya sisi tu ni wafanyakazi wa nchi za Kaskazini. Huyo si mwenzetu hata kidogo. Si mwenzetu, […] Jifanye bepari mzalendo, tutakuunga mkono asilimia mia moja kama bepari mzalendo. Hatutakusaidia, tutapambana nawe kama utajaribu kuifanya nchi hii koloni mamboleo kwa ajili ya mtu mwingine nje ya Tanzania. Tuelewane hivyo. Kuwa bepari, tengeneza fedha, lakini fedha hizo kwa ajili ya Tanzania – kwa ajili ya kujitegemea kwa nchi yetu – lakini tukupe uwanja wa nchi yetu uutumie kutufanya wafanyakazi wa watu wengine, hatukubali hata kidogo. Tutapambana na nyinyi mkiwa namna hiyo. Ndio maana sasa hivi tunasema waziwazi. Tujenge nchi yetu. Hatutaji, katika hali ya kujaribu kuutoa uchumi wetu katika hali hii ya ovyo, tutatumia uwezo wetu wa ndani kwa ajili ya maendeleo, ubepari na ujamaa. Tutazichanganya zote hizi kwa nguvu kabisa kabisa kujenga uchumi wa nchi yetu.[4]

Katika hoja hii ya Mwalimu kuna masuala mawili yanaibuka. Moja, ambalo sio wazi sana ni kwamba sekta binafsi ya kizalendo

inaruhusiwa kufanya kazi kwa masharti na shabaha maalumu, na Mwalimu anabainisha wazi wazi kabisa kwamba ikienda kinyume watapambana nayo. Ni kwa namna gani, suala hili linaweza likajadiliwa, lakini ni wazi anachosema Mwalimu, na kwa kweli ni sahihi kabisa, kuwa dola ndio itaongoza ujenzi wa uchumi wa kitaifa, na sekta binafsi ya ndani itaongozwa na kusimamiwa na dola, kwa masharti. Bila hivyo kutakuwa na uholela aliousema Mwalimu mwaka 1982. La pili, ni kuwepo kwa mapebari wazalendo, je walikuwepo mwaka 1989 wakati Mwalimu akiwapa jukumu alilowapa, na je hii leo wapo, na kama wapo ni wengi na wana uwezo kiasi gani? Suala hili ni muhimu kwa sababu kwa muda mrefu imefahamika kuwa nchi zetu zinao mabepari uchwara, ambao kazi yao kubwa ni kutumika kama wasimamizi wa mirija toka nje. Je hali hii ni tofauti sasa?

Suala la mwisho ambalo limejitokeza sana katika nyaraka hizi ni chanzo cha mtaji na msingi wa mapinduzi ya kweli ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Mwalimu Nyerere na Edward Sokoine katika hotuba zao zilizomo kwenye kitabu hiki wanazungumzia kilimo kama msingi wa maendeleo ya taifa. Mwalimu anakiri kuwa ni kilimo ndicho kilichotupatia maendeleo. Kuhusu ukweli huu Mwalimu anasema: ‘Kitu chochote kinachoweza kuitwa maendeleo hapa ni matokeo ya kazi za wakulima wa Tanzania. Wao ndio waliolima mazao yaliyotusaidia kupiga hatua katika elimu, afya ujenzi wa viwnada, ulinzi na kujenga njia za usafirishaji unaoaminika.’[5] Umuhimu wa kilimo unapata msisitizo zaidi kwenye Mwongozo wa 1981, hasa pale Mwongozo unaposema kuwa msingi wa maendeleo ya taifa linalojitegemea ni kilimo. Katika hili Mwongozo ulionyesha umuhimu wa taifa kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula ya wananchi na ‘kulipa Taifa uwezo wa kujitegemea katika mahitaji ya maendeleo ya baadaye.’ [Uk. 80]. Juu ya hili Mwngozo ulisisitiza kuwa :

> Msingi wa uchumi wa nchi yetu ni kilimo. Asilimia themanini na tano ya watanzania wanaishi kwa kilimo; biashara yetu na nchi za

> kigeni inategemea zaidi mazao tunayoyatoa katika kilimo; Viwanda vichache tulivyonavyo nchini vinategemea mazao ya kilimo; uwezekano wa kutoa ziada itakayowezesha nchi kugharimia mapinduzi ya viwanda [kugharimia Viwanda vya madawa] upo katika sekta ya kilimo. [Mwongozo 81]

Na Edwatd Sokoine katika mchango wake sio tu alisisitiza umuhimu wa kilimo bali pia umuhimu wa taifa kujitosheleza kwa chakula. Yote haya mawili, kwa mtazamo wa Sokoine siyo tu yanajenga msingi mathubuti wa maendeleo ya nchi bali pia yanalinda heshima na uhuru wa watu. Katika kusisitiza hili Sokoine alisema:

> Suala la kilimo hatujawahi kulisahau lakini nafikiri sasa tutatilia mkazo kuliko tunavyofanya wakati mwingine wowote huko nyuma. Jana ulitumia maneno ya kusema "mwalimu mmoja wa zamani aliwaambia wanafunzi wake kwamba ukweli utawakomboa" ***Nafikiri kwa hivyo ungeweza ukatuambia kwamba kujitosheleza kwa chakula kwa Watanzania, vile vile kutatukomboa na kulinda uhuru wetu.*** [6]

Kwa vile vijiji ndio eneo la muhimu la uzalishaji katika nchi Sokoine pia alisisitiza umuhimu wa kubadili mtazamo wa kuviona vijiji kama viko katika mpito wa kuwa miji bali kuwa vitovu vya uzalishaji. Juu ya hili alishauri:

> …. namna ya kufikiria … kuwapata wataalamu wanaohitajika kwa siku za usoni. Kama tulivyokwisha kusema katika vikao vingi vya Chama, vijiji ndivyo vitovu vya maendeleo ya Tanzania na kule ndiko wanakohitajika wataalamu walio bora sana. Hili ni pambano kubwa, maana vijijini hakupendeki sana …..[7]

Nyaraka zilizomo katika kitabu hiki ni za muda kidogo, na baadhi ya mambo ya kimuktadha yawezekana kabisa yakawa yamebadilika. Lakini hoja zinazoibuliwa hazijapitwa na wakati kabisa, hivyo haziwezi kupuuzwa. Safari ya ukombozi kutoka katika ukoloni mambo leo itawezekana tu pindi tutakapotambua kuwa ujenzi wa uchumi wa kitaifa ndio njia kuu ya kufikia shabaha hiyo. Na ujenzi na uendelezaji wa uchumi wa viwanda hauna budi kuongozwa na sura na dhamira ya dhati ya ujenzi wa uchumi wa kitaifa. Katika dunia ambamo ubepari mamboleo unatamba, ni rahisi sana kupoteza mwelekeo na dira. Ubepari mamboleo umejaa hila na viini macho. Katika hadithi moja ambayo Mwalimu aliwahi kuitoa, ambayo inatoa taswira ya namna mbinu na hila za ubepari zilivyo, ni pale ambapo watu fulani [wapumbavu] walikuwa wana almasi mikononi mwao, akatokea mjanja mmoja akawaomba atazame almasi zao, baada ya kuzitazama na kuzichunguza akawaambia zile hazikuwa almasi, ndipo alipotoa vipande vya chupa vinavyo meremeta na kuwaonyesha, kisha akawaambia kuwa zile chupa ndizo almasi, wale watu [wapumbavu] akawapa zile chupa na wao wakampa zile almasi. Wao wakawa wamepoteza na yeye akawa amepata. Hali kama hii ingevumilika tu wakati nchi haina wataalamu wake yenyewe. Tanzania leo inao wataalamu wengi iliosomesha. Lakini haitoshi tu kuwa na wataalamu wetu wenyewe, lazima kupambana na mawazo ya kitegemezi na hali ya kutojiamini. Vinginevyo tutaendelea kuhadaiwa kwa mipango inayo meremeta tukadhani ni almasi kumbe ni chupa zisizo na thamani yoyote.

Ni katika muktadha huu lazima tujihadhari sana na aina za viwanda ambavyo vinaweza kuhamishwa toka nchi zingine na kuletwa huku kwetu – aina ya viwanda ambavyo vitachafua mazingira yetu. Aidha, tunaweza kukumbatia mifumo ya ujenzi na uendelezaji viwanda ambayo haijali sana maslahi ya wafanyakazi na mazingira yao wanapofanyia kazi. Hadhari kubwa haina budi kuchukuliwa ili tusifanye makosa ya zamani, na makosa ambayo nchi zingine zilizokumbatia aina ya mifumo ya viwanda kama hivyo zimeyafanya.

Mwisho, katika msukumo huu wa kujenga na kuendeleza viwanda, Rais Magufuli ametangaza vita vya kiuchumi. Tangazo hili la vita ni muhimu. Tangazo kama hilo liliwahi kutolewa na Mwalimu Nyerere mwaka 1982 kwenye Mkutano Mkuu wa CCM. Katika tangazo hilo Mwalimu alitoa masharti matatu ya kushinda vita vya kiuchumi. Masharti hayo ni:

> Kwanza lazima unuie kuendelea kupigana. Na sisi hatuna la kufanya isipokuwa tunuie kuendelea kupigana. … Pili, lililo lazima kama tunataka kupata ushindi ni kutambua kiasi cha hasara tuliyopata mpaka sasa, na kuchambua matatizo yanayoikabili nchi, ili tuweze kujua ubovu na makosa yetu wenyewe yaliyotuongezea uzito wa madhara. …. Tatu, ni kuchukua hatua zozote zilizo lazima kusahihisha makosa na kuondoa ubovu wetu; kukusanya uwezo wetu wote, na kupigana kwa dhati katika mazingira halisi ya dunia ya leo.[8]

Wakati Mwalimu akitangaza vita hii shabaha ya kitaifa ilikuwa dhahiri, kujenga nchi ya Ujamaa na Kujitegemea. Inawezekana kabisa mkakati haukuwa sahihi sana. Sasa hivi shabaha si dhahiri sana, japo dhamira na nuio la kupigana vita hivi lipo. Lakini tunaweza tukaanzia mahala, ili kuifafanua na kuipa ufasaha dhamira ya vita vya sasa vya kiuchumi, ambayo sehemu yake moja kubwa ni ujenzi na uendelezaji wa viwanda. Tunadhani, shabaha kuu ya vita hivi vya sasa ni kujenga uchumi wa kitaifa, uchumi unaojitegemea. Kwamba, sekta muhimu tutakayotakiwa kuiendeleza na kuikuza ni ya viwanda; na kwamba rasilimali zetu zote kwa maana ya nguvu kazi ya watu wetu, mali asili yetu anuai, na kila uwezo wa ndani tulio nao sasa na tutakaoupata baadae utusaidie kujenga uchumi wa aina hiyo. Tunaweza kunuia kupigana vita hivi, lakini lazima tumjue adui yetu, vinginevyo tutashindwa. Kazi ya kumbaini adui inahitaji uchambuzi wa kina, na mijadala ya kina, huru na wazi. Hali kadhalika, katika uchambuzi na tafakari hii

lazima kubaini askari wa mstari wa mbele katika vita hivi, na nani msindikizaji au atakayehujumu vita hii. Na ili kuweza kuuhamasiha umma mkubwa wa watanzania kuunga mkono vita hii – yaani kundi la wavuja jasho: wazalishaji viwandani na mashambani, na wale wengine wenye shughuli zao mitaani, ni lazima kufafanua kwa ufasaha sana shabaha za muda mrefu na mfupi za vita hivi vya uchumi, na umuhimu wa viwanda na aina ya viwanda katika kufikia shabaha za vita hii.

Ni safari ya mapambano makubwa, lakini ya lazima, na inahitaji ushirikiano wa kila mwananchi anayeamini katika vita vya ukombozi, kutoka katika mfumo wa uchumi tegemezi wa kikoloni mamboleo kwenda kwenye uchumi wa kitaifa, unaojitegemea.

# SURA YA KWANZA

## Mafanikio yetu chini ya Azimio la Arusha[2]

***Julius K. Nyerere***

*Tarehe 5 Februari 1977 Mwalimu Julius Nyerere alitoa taarifa kwa Chama na kwa Taifa juu ya hali ya uchumi na maendeleo ya kijamii katika nchi miaka kumi baada ya kutangazwa Azimio la Arusha. Katika sehemu hii ya hotuba yake Mwalimu anatoa tathmini ya hatua za ujenzi wa viwanda, maendeleo ya kilimo na uzalishaji mali …….*

**[…]**

**Kumiliki kwa Nguzo Kuu za Uchumi na Biashara**.

Kutaifishwa kwa viwanda na huduma zilizokuwapo kulikofanywa mara baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha halikuwa jambo muhimu kwa sababu ya kutaifishwa kwenyewe tuu, bali kwa sababu ya yale yaliyofuata ya baada hapo. Maana kutaifisha ni kutaifisha kitu kilichopo, na wakati ule maendeleo ya viwanda katika Tanzania yalikuwa madogo sana. Lakini hata hivyo, hatua zenyewe za kutaifisha zilikuwa hatua muhimu kwa sababu ya matokeo ya baadae. Na maana yake ilikuwa kupunguza kuhamishwa kwa mali ya Tanzania iliyokuwa ikitolewa nchini kwa njia ya faida au riba.

Haiwezekani kukadiria jumla ya fedha ambazo zingetolewa nje ya Tanzania katika kupindi hiki cha miaka kumi kama tusingetaifisha njia kuu za uchumi na biashara mwaka 1967. Tukitazama Benki ya Taifa ya Biashara peke yake, jumla ya faida iliyobakia Tanzania katika kipindi hiki 1967/1977 ni shilingi milioni 557.3. Na hizo ni baada ya kulipa fidia kamili kwa mabenki ya binafsi yaliyotaifishwa ili kuanzisha Benki yetu. Hesabu hiyo inasaidia kidogo kuonyesha

[2] Nyerere, Julius, 1977. Azimio la Arusha Baada ya Miaka Kumi; Dar es Salaam; Uk. 8-40.

kiasi cha fedha ambazo labda zingetolewa nje ya Tanzania kutoka katika Benki tu katika kipindi hiki.

Kwa hiyo mtu anaweza kusema bila ya kusita kwamba moja ya matokeo ya Azimio la Arusha ambayo sasa yanatunufaisha ni kwamba mali ile tunayoizalisha katika Tanzania inapatikana na kutumiwa Tanzania. Mrija uliokuwa unatumika kunyonyea mali yetu kidogo sasa umekatwa.

Lakini lililo muhimu zaidi ni kwamba kwa kuzitia mikononi mwa umma shughuli za uzalishaji mali na biashara tumeweza kujiamulia wenyewe vitu tunavyohitaji kuvijenga, na kupanga umuhimu wake. Kwa hiyo tumeweza kutumia kidogo tulichonacho (ama chetu wenyewe, au tunachokopa) kujenga viwanda ambavyo vitatosheleza mahitaji ya watu wetu. Ni wazi kwamba tumefanya makosa fulani fulani; mara moja au mbili tumetumbukia katika mtego wa kutamani mno kufanya mambo ya “kisasa’’, tukajenga viwanda vikubwa vya gharama kubwa, ambapo viwanda vingi vidogo vidogo vinavyotumia zaidi jasho la wananchi vingeweza kutoa huduma ile ile kwa gharama ndogo zaidi na wataalam wachache zaidi kutoka nchi za nje.

Lakini ukiacha makosa hayo madogo madogo, utaona kwamba tumepiga hatua katika maendeleo ya viwanda. Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita tumeanzisha idadi kubwa ya viwanda vidogo vidogo, ama katika sehemu za mijini ama katika sehemu za vijiji vya Tanzania. Vilevile tumeanzisha viwanda vikubwa vya kutengeneza vitu mbali mbali kama zana za kilimo, magurudumu ya motokari, mbolea, radio, beteri na baiskeli, na saruji, mitambo ya uchapishaji, n.k. Vyote hivyo, na shughuli nyingine za viwanda hutengeneza bidhaa zinazohitajiwa na wananchi wa Tanzania. Pia baadhi ya viwanda vyetu tulivyovitaifisha mwaka 1967 tumevipanua, kwa mfano kiwanda cha viatu na cha sigara. Viwanda vingine zaidi vimo katika kujengwa.

Pamoja na hayo yaliyokwisha kutajwa, tunatia mkazo maalum katika kuongeza shughuli zinazotumia rasilimali zetu wenyewe.

Kwa mfano, mnamo mwaka 1967 sehemu ndogo sana ya pamba yetu ilikuwa ikitengenezwa nguo katika Tanzania; kufika mwaka 1975 tulikuwa na viwanda vinane vya nguo vyenye uwezo wa kutengeneza mita za mraba milioni 84 za nguo. Shughuli za kusokota kamba za mkonge zimeongezwa sana. Na bado mipango ya kupanua zaidi viwanda hivi inaendelea. Kiwanda kipya cha nguo kitajengwa Musoma, na kiwanda cha Mwanza hivi sasa kimo katika kupanuliwa. Upanuzi wa Kiwanda cha Urafiki umekwisha. Kiwanda cha kutengenezea mazulia ya mkonge kinajengwa huko Kilosa; viwanda vipya vya saruji vinatayarishwa kujengwa Tanga na Mbeya; viwanda vya aina mbalimbali vinatayarishwa kujengwa Morogoro; na kadhalika. Katika viwanda vyote hivyo tuna shabaha mbili: ya kwanza ni kuwa na uwezo wa kutosheleza mahitaji ya wananchi wetu wenyewe kwa kuwatengenezea bidhaa hizo mumu humu Tanzania, na pili kuyageuza mazao yetu kuwa bidhaa iliyotengenezwa kabla ya kuyauza nchi za nje. Kwa njia hii tutaongeza kiasi cha fedha za kigeni tutakazozipata, kwa sababu thamani iliyoongezeka kutokana na kuitengeneza mali ile sasa itarudi Tanzania, na italipwa kwa Watanzania kwa njia ya mshahara au rasilimali itakayotumiwa na Watanzania.

Kwa kweli upanuzi wenyewe wa viwanda katika kipindi cha miaka kumi iliyopita ni mdogo mno, ukilinganishwa na mahitaji yetu. Lakini hakuna sababu ya kuona haya. Hapa tena inafaa kukumbuka tulikotoka. Katika kipindi hicho thamani ya mali iliyotengenezwa viwandani imeongezeka mara tatu. Sasa hivi viwanda vinatoa karibu asilimia 10 ya pato la Taifa, badala ya asilimia 8 kama ilivyokuwa mwaka1968. Na hiyo ni katika uchumi ulioongezeka sana. Idadi ya watu wanaoishi kwa kufanya kazi viwandani imeongezeka mara $2^{1/2}$ zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 1967.

Kama tungetegemea watu au makampuni binafsi kutia rasilimali zao katika kupanua viwanda, pengine viwanda vichache katika hivi vipya vingeanzishwa nchini mwetu. Hata kama rasilimali za watu binafsi kutoka nchi za nje zingeongezeka, na kuongeza uwezo wa fedha za kutumika katika uzalishaji wa viwandani, ni jambo la

hakika kabisa kwamba viwanda vipya visingekuwa vya aina ya kutengeneza bidhaa zinazohitajiwa na watanzania, au ya kutumia kwa ukamilifu zaidi mazao ya Tanzania. Maana shughuli kama hizo katika nchi maskini hazileti faida kubwa sana ya fedha.

Ni kweli kwamba tungejaribu kuvutia, holela tu, rasilimali kutoka nchi za nje, viwanda vingeweza kujengwa, lakini kwa kutengenezea vitu vingine. Kwa mfano katika nchi nyingi changa makampuni makubwa ya nje yamejenga viwanda vinavyotengeneza baadhi ya vifaa vya kuundia vyombo vikubwa zaidi. Baadaye vifaa hivi na vinginevyo kutoka nchi nyingine maskini hupelekwa ili viunganishwe na kuunda hivyo vyombo vikubwa. Matokeo ya maendeleo ya bandia ya viwanda vya aina hiyo ni kuhakikisha kwamba sehemu fulani muhimu ya uchumi daima itategemea kampuni hilo la nje. Na kwa kuwa shabaha peke yake ya makampuni kama hayo ni kujizidishia faida kutoka katika mataifa mengine, bila ya kujali manufaa ya nchi ile ambamo viwanda vimejengwa, basi ‘’maendeleo’’ kama hayo kwa kweli si maendeleo ya nchi ile hata kidogo. Inawezekana kiwanda kama hicho kitafanya takwimu za viwanda zionekane nzuri, lakini hatimaye nchi ile inaweza ikawa imerudi nyuma katika suala la uhuru wake na maendeleo ya watu wake. Nchi nyingine zina matatizo makubwa ya watu wake kukosa kazi, na wala hazina ardhi ya kutosha. Nchi kama hizi haziwezi kukataa kabisa kujenga viwanda vya aina hyo. Lakini Tanzania haina sababu kama hizo za kuifanya itegemee mabepari wa kigeni. Na tumekwepa hatari yoyote ya kufika hapo kwa kushikilia kwamba katika shughuli zote muhimu fedha za wageni zitatumika katika nchi hii kwa kushilikiana na fedha za Serikali, hisa ya Serikali ikiwa kubwa zaidi; na kwa njia hiyo umma umeweza kumiliki na kutawala viwanda hivyo.

[….]

**Kilimo, msingi wa maendeleo:**

Toka Azimio la Arusha kupitishwa tumezungumza sana habari ya maendeleo ya vijijini na kupanua shughuli za kilimo ikiwa ndio

msingi wa maendeleo ya Tanzania ya kesho. Na tumetumia kiasi kikubwa sana cha fedha katika maendeleo ya vijijini, na sehemu ya fedha hizo inatoka kwa marafiki zetu katika nchi za ng'ambo. Kwa hyo, kwa mfano, katika miaka miwili iliyopita kila mwaka tumetumia kiasi cha shilingi milioni 400 katika shughuli za kilimo, ambapo mwaka 1967 fedha zilizotumiwa kwa maendeleo ya kilimo zilikuwa kiasi cha shilingi milioni 45 tu.

Vile vile, ili kuunga mkono juhudi za kupanua kilimo serikali imefidia gharama za mbolea, ambayo matumizi yake yameongezeka kwa zaidi ya mara mbili katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Serikali imetoa mikopo kwa vijiji vya Ujamaa na Vyama vya Ushirika kwa kutumia Benki ya maendeleo ya vijijini. Serikali imesaidia katika mipango ya umwagiliaji maji; imetoa mafunzo katika matumizi ya plau la kukokotwa na ng'ombe, na kadhalika. Bado misaada inahitajiwa, na wakati mwingine huduma hizo zimetumiwa vibaya, au zimechelewa mno kupelekwa. Lakini jitihada zimefanywa.

Lakini ukweli ni kwamba mapato yatokanayo na kilimo hayakuwa ya kuridhisha. Utaalam wa kisasa haukuenea kwa haraka, na wala haukuenea kote. Mazao mengi tuliyozoea kuyalima bado yanalimwa kwa namna ilieile kama walivyolima babu zetu. Umwagiliaji maji mashambani, na hata ujenzi wa mabwawa madogo madogo, bado ni maneno ya mitaani tu, utekelezaji ni mdogo, au hakuna kabisa. Bado watu wanafikiria kupata trekta kulimia mashamba yao, hata kama mashamba hayo ni madogo, kuliko kujifunza kutumia plau la kukokotwa na ng'ombe; au wanafanya bidii kuchanga fedha za kununua lori ambapo mahitaji yao yanaweza kutekelezwa kwa kutumia magari madogo madogo ya kukokotwa na ng'ombe kubebea mbegu au mazao kutoka shambani kupeleka ghalani kijijini. Kuhusu kilimo, na maarifa ya kilimo, hata fikira zetu hazikubadilika kiasi kinachohitajiwa.

Ni wazi kwamba kiasi cha mazao ya kilimo kimeongezeka katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Kwa mazao mengine maendeleo yake yamekuwa makubwa sana, hasa ukikumbuka kuwa tumepata

msimu wa mvua haba katika miaka michache iliyopita. Lakini kwa mazao ya chakula, kwa mfano, kuongezeka kwake hakukulingana na kuongezeka kwa watu nchini. Ni kweli kwamba mwaka tulipopata mvua nzuri tumeweza kujitosheleza kwa chakula. Kuagiza kutoka nchi za nje kiasi kikubwa cha nafaka mwaka 1974/75 halikuwa jambo la kawaida. Lakini sababu ya kujitosheleza kwetu kwa chakula katika miaka ya kawaida si uhodari wetu wa kilimo. Nchi yetu ni nchi ya wakulima; na wakulima wakiwa na ardhi wataweza kulima chakula angalau cha kujishibisha wenyewe. Na hili ndilo walilokuwa wanafanya. Idadi ya wananchi wanaoishi katika miji yetu ni ndogo sana; kwa hiyo kiasi cha chakula cha ziada kinachohitajiwa kuwalisha hawa ni kidogo pia. Mvua zikiwa nzuri wakulima wanaweza kuipata ziada hii. Lakini ufanisi wetu wa kilimo ni mdogo mno kutuwezesha kupata ziada inayoweza kuwalisha watu wengi zaidi wa mjini au kujiwekea akiba ya lazima kwa maafa.

Tukitazama nyuma tunaweza kuona sababu zilizofanya kilimo chetu kisitupe maendeleo ya kutosha. Serikali imechelewa mno kuongeza bei wanayopewa wakulima, hata wakati mwingine ikatokea wakulima hawakupata malipo ya haki kwa jasho lao kwa kuuza mazao ya chakula, au hawakuweza kufidia gharama zao za kilimo kwa sababu ya kupanda kwa bei za vifaa. Hali hii sasa imebadilika. Bei mpya za sasa zinamwezesha mkulima mwenye juhudi, kujipatia kipato cha kutosha kwa juhudi yake, mradi mvua zinyeshe. Vile vile matatizo ya usafirishaji na huduma mbovu za vyama vya ushirika ni mambo mawili yaliyorudisha nyuma juhudi hii. Lakini sababu kubwa zaidi ambayo imefanya maendeleo yetu katika kilimo yasiwe ya kuridhisha inatokana na kukosekana kwa uongozi bora wa siasa na utaalam wa kilimo vijijini na wilayani. Pamoja na wito wa ``Siasa ni Kilimo'' uliowataka viongozi wote wa siasa kujifunza mambo ya msingi ya kilimo bora katika maeneo yao, na kushirikiana na wakulima katika shughuli za kilimo; bado tumekuwa tukiwapigia kelele wakulima na kuwadai walime zaidi, bila ya kufanya juhudi ya kuwasaidia au ya kufanya kazi pamoja

nao kwa uhusiano wa kuheshimiana. Viongozi wetu wengi hawajui chochote juu ya kilimo, na wala hawataki kujifunza.

[…]

Wakulima wa Tanzania wanaweza wakalaumiwa kwa mambo mengine, lakini hawawezi kulaumiwa kwa kutofanya kazi katika kipindi cha miaka kumi iliyopita na ile ya kusema kuwa wakulima wameshindwa kufanya kazi. Wamefanya kazi sana. Lakini wamefanya kazi kwa juhudi bila maarifa ya kutosha ya kilimo cha kisasa; vile vile wamepigwa vibaya sana na ukame baada ya miaka mingi mfululizo kupita bila ya mvua nzuri. Ikifanywa juhudi zaidi ya kutengeneza mipango midogo midogo ya kujenga mabwawa na kumwagilia maji mashambani inawezekana angalau kupunguza hasara inayoweza kupatikana kutokana na uhaba wa mvua. Na vile vile lazima tutilie mkazo umuhimu wa kupanda, kupalilia, na kuvuna kwa wakati wake, pamoja na kupanda kwa nafasi zinazotakiwa. Maana mambo haya hayatugharimu chochote cha zaidi, lakini matokeo yake yanaweza yakawa kuongezeka sana kwa mazao yanayopatikana.

Zaidi ya hayo, lazima tuongeze matumizi ya ujuzi na mbegu zilizojaribiwa na wataalam katika vituo vyetu vya uchunguzi; maana kazi nzuri sana ya uchunguzi inafanywa nchini. Katika miaka hii ya karibuni mbegu za aina mpya zimepatikana na mazao ya chakula na ya fedha. Zamani uchunguzi ulikuwa ukifanywa kwa ajili ya mazao ya fedha tu. Sasa kuna mbegu za aina mbali mbali za mahindi na mtama zinazotumika nchini; lazima tuzipande mbegu hizo katika maeneo yaliyochaguliwa. Siku hizi kuna tabia iliyoenea mno ya wananchi kutaka kupanda mahindi hata katika maeneo ambako uwele au mtama (ambao ni chakula bora zaidi) ni mazao yenye hakika zaidi kwa mvua za sehemu hiyo. Katika kilimo juhudi kubwa imeonekana; sasa mkazo wetu inafaa tuutie katika maarifa.

Jambo jingine la jadi yetu ambalo lazima tulirudie ni kuweka akiba ya chakula vijijini. Mara nyingi utaratibu wa kiasili ungeweza kutumika kwa manufaa kwa kufanya mabadiliko kidogo tu ya

kukinga wadudu waharibifu. Na akiba ya chakula kijijini ingeweza kuwa kinga ya wananchi kuepukana na mikasa ya siku za mbele, pamoja na shida za usafiri, na ingeweza kupunguza matumizi ya fedha za mkulima kwa chakula, akazitumia fedha hizo kwa shughuli nyingine. Lakini bado itakuwa lazima kwa Taifa kujenga maghala ya chakula kwa Taifa zima katika sehemu mbali mbali za nchi hii, jambo ambalo tulilipuuza katika siku za nyuma.

[…]

**Kuzalisha mali:**

Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita tumepiga hatua nzuri katika kueneza huduma kwa wananchi wengi zaidi vijijini. Bado iko kazi kubwa mbele yetu, lakini tunaweza kuifanya kazi hiyo kama tu tutazalisha mali nyingi zaidi. Na katika hilo mafanikio yetu si mazuri sana.

Kwa hesabu za bei za kudumu, Pato la Taifa limeongezeka kidogo zaidi tokea 1967 kuliko lilivyokuwa likiongezeka kabla ya hapo. Maana kutoka mwaka 1964 hadi 1967 Pato la Taifa katika Tanzania liliongezeka kwa wastani wa asilimia 6.4 kwa mwaka. Lakini kati ya mwaka 1967 na 1975, Pato liliongezeka kwa wastani wa asilimia 4.2 tu kwa mwaka. Hata ukiondoa mwaka ule wa ukame, ambapo tusingeweza kuzuia kupungua kwa Pato, bado wastani wa miaka hiyo mingine ulikuwa asilimia 4.6 kwa mwaka. Kwa kuwa idadi ya watu inaongezeka nchini kwa kiasi cha asilimia 2.8 kwa mwaka, maana yake ongezeko hili la pato ni kwamba kuongezeka kwa hali ya maisha ya kila mwananchi ni kidogo sana. Hali ya maisha ya Watanzania wengi imekuwa nzuri zaidi kutokana na mgawanyo mzuri kwa pato lililopo, siyo kwa kuongezeka sana kwa pato hilo.

Ni kweli kwamba miaka kumi iliyopita ilikuwa ni miaka mibaya sana kwa uchumi. Kwa mfano bei za biashara kati ya bidhaa tulizokuwa tunaziuza nchi za nje na zile tulizokuwa tunaziagiza zimekuwa zikitukandamiza sisi katika kipindi chote hicho. Hili maana yake ni kwamba bidhaa tunazozalisha na kuuza katika nchi za nje zinapata bei ndogo kulinganisha na bidhaa tunazolazimika

kuagiza. Lakini si vizuri kutumia hali ya uchumi wa dunia na miaka ya ukame, kuwa kisingizio cha kufichua ubovu wetu wenyewe. Ubovu huo lazima tuuchunguze na kuugundua ili tuweze kufanya vizuri zaidi katika kipindi cha miaka kumi ijayo.

Tatizo halikuwa kushindwa kupata rasilimali ya kujengea viwanda vipya au kuanzisha mashamba mapya. Katika miaka minne 1967—1970 rasilimali ya shilingi milioni 1,155 ilitumiwa katika miradi mipya ya uchumi katika mashirika ya umma peke yake, na kiasi cha fedha kilichotumiwa kwa kazi kama hizo kiliongezeka kidogo kidogo mwaka hata mwaka kwa kipindi cha miaka mitano iliyofuata. Ulipofika mwaka wa fedha 1975/76 ikawezekana kutilia mkazo zaidi miradi inayozalisha mali kuliko miradi mingine. Mwaka ule makadirio ya mipango ya maendeleo yaliweka shilingi milioni 890, ukiacha rasilimali zilizotumika mikoani, kwa ajili ya mipango inayozalisha mali moja kwa moja. Na mwaka huu fungu hilo litaongezwa zaidi. Ingawa hatujapata bado matokeo ya rasilimali hii tuliyotumia miaka miaka michache tuu iliyopita, lakini ni wazi kwamba matunda ya rasilimali iliyotumika mnamo nusu ya kwanza ya kipindi hiki cha Azimio la Arusha yangeanza kuonekana.

Lakini hatutumii rasilimali zetu kwa manufaa kama ambavyo tungepaswa kuzitumia. Karibu viwanda vyetu vyote vinafanya kazi chini ya uwezo wake, wakati mwingine vinatengeneza chini ya asilimia 50 ya bidhaa ambazo zingeweza kutengenezwa kwa kutumia mitambo hiyo hiyo. Hata mitambo ya bia imetumia asilimia 68 tu ya uwezo wake mwaka 1975; Tegry Plastics ilitumia asilimia 46, na Maziwa ya Mara chini ya asilimia 30 ya uwezo wake. Vile vile kiwanda cha saruji cha Wazo hakitengenezi saruji ukomo wake, kama kiwanda hicho kingekuwa kinafanya kazi sawa sawa; na pengine viwanda vya nguo vigeweza kuongeza kiasi cha nguo kinachotengenezwa. Mwaka 1975 kiwanda cha Bora kilikuwa kinatengeneza viatu vichache zaidi kulingana na uwezo wa mitambo yake, na tena havikuwa vizuri. Lakini kiwanda hiki kimeonyesha marekebisho katika mwaka uliopita.

Wala mashirika yetu hayatoi ziada ya kutosha kutuwezesha kuanzisha mipango mingine. Katika kipindi cha miaka minane toka 1967 hadi 1974, asilimia 20 tu ya rasilimali mpya ilitokana na fedha kutoka mashirika ya umma yaliyopo. Kwa kifupi, mashirika hayo hayakuwa yanapata faida ya kutosha. Maana faida ni kitu cha lazima, ikiwa kampuni ni mali ya bepari au mali ya umma. Tofauti tu ni kwamba ikiwa ni mali ya umma, basi umma unajua faida hiyo inatumikaje; umma hausemi hakuna haja ya faida. Kwa kipimo cha jumla, faida kutokana na mashirika yetu katika kipindi hicho cha miaka minane ilikuwa ni wastani wa asilimia 6.5 tu ya mauzo yote kwa mwaka.

Mwaka 1975, hata faida ya shirika la bia, kabla ya kukata kodi, ilikuwa shilingi milioni 4 hivi, kwa mauzo ya bia ya shilingi milioni 535.5. Na wala hatuwezi kusema kuwa tulikuwa na matatizo ya kuiuza!

Ukweli ni kwamba hatukuwa, na mpaka sasa hatujawa, katika hali ya kufanya kazi kwa ufanisi katika viwanda vyetu. Kwa mfano, thamani ya kazi mtu katika viwanda vyetu ilipungua kutoka wastani wa shilingi 18,870 mwaka 1967 kufikia wastani wa shilingi 16,540 mwaka 1974: na wakati huo thamani ya fedha ilikuwa imeshuka. Vile vile kumekuwako na upungufu wa uzalishaji mali kwa kila saa ya mfanyakazi katika kampuni za ujenzi, na uzalishaji wa mazao ya kilimo hauongezeki kulingana na kuongezeka kwa idadi ya watu nchini.

Kushindwa huku kunapotokea pengine makosa huwa siyo ya kampuni. Kwa mfano tatizo kubwa la kiwanda cha Maziwa ya Mara ni kwamba wafugaji wa sehemu ile hawatoi maziwa ya kutosha, na moja ya matatizo ya makampuni mengine wakati mwingine ni shida za mara kwa mara za kupatikana kwa mali ya kutumika katika viwanda hivyo, ingawa mara nyingi hata hiyo ni dalili ya viongozi kushindwa kuagiza mali hizo na mapema. Vile vile kukatika mara kwa mara kwa maji na nguvu za umeme Dar es Salaam na Mwanza katika kipindi cha 1974—1976 lazima kulipunguza uzalishaji mali. Na vizingiti hivyo vilitokea kwa sababu Serikali ilikuwa

imechelewa mno kutengeneza huduma hizo, ambazo ujengaji wake ulikuwa nyuma kuliko ilivyotarajiwa.

Lakini matatizo yanayotokana na nje ya kiwanda siyo peke yake yaliyosababisha upungufu uliotokea. Ziko na sababu nyingi nyingine, na kila moja lazima ichunguzwe kwa kukiangalia kila kiwanda peke yake.

Mara nyingi gharama za mishahara na za kuendeshea ni kubwa mno kulingana na mali inayopatikana. Katika kila shirika tuna msululu mrefu wa mameneja wa kazi mbali mbali, na Meneja Mkuu juu yao. Kila meneja ana mwandishi wake, ana ofisi yake, na mara nyingi ana gari lake. Mambo haya yanaweza yakakubalika ikiwa mameneja wenyewe ni hodari sana katika kazi zao, na marupurupu hayo yanawapa uwezo wa kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa zaidi. Lakini mara nyingi mambo sivyo yalivyo. Tunaajiri meneja wa uuzaji ambaye hukaa ofisini mwake na kungojea wanunuzi waje kumtafuta, bila ya kufanya juhudi yoyote ya kuchunguza mahitaji ambayo kiwanda ama kinayatosheleza au hakiyatoshelezi, au mabadiliko katika utengenezaji wa bidhaa yangekuwa ya manufaa zaidi kwa wanunuzi n.k. Tunaajiri mameneja wazalishaji ambao hawaagizi spea au vifaa vinavyohitajiwa kwa wakati wake, au mara baada ya kuviagiza vitu hivyo wanakaa tuu na kulalamika badala ya kuendelea kuvisaka endapo vimefika bandarini na havijatolewa. Tunao Mameneja wa Matengenezo katika mashirika yetu ya usafiri ambao inaonekana wanakubali wakati wowote kuwa na kiasi cha asilimia 40 ya magari yao mabovu yanayongojea kutengenezwa au kutiwa girisi! Sijui wanachotengeneza.

Baadhi ya kasoro hizi ni matokeo ya kutokujua au kukosa kujiamini kwa vijana wanaozishika nafasi hizo. Kama hivyo ndivyo, basi mafunzo zaidi yanaweza kusaidia, na vile vile kutafuta ushauri kutoka kwa mameneja wenye ujuzi zaidi katika viwanda vingine ambao wanaweza kuulizwa yanapotokea matatizo makubwa. Maana ni kweli kwamba mameneja wetu kwa ujumla ni vijana wadogo sana, wasiokuwa na ujuzi mwingi, na ambao wana nafasi kidogo sana ya kujifunza kwa kuwaangalia wengine wakifanya

kazi, kama wenzao wanaoshika nafasi kama hizo katika nchi zilizokomaa zaidi. Wananchi kama hao wanaweza kupewa nafasi na muda wa kujifunza na kujiendeleza. Lakini kama hawajifunzi upesi, na kama hawajiendelezi, basi lazima wapewe kazi nyingine au waachishwe kazi; ni bora kuwa na nafasi isiyokuwa na mtu kuliko kuwa na mtu anayelipwa mshahara bila kufanya kitu.

Lakini sababu ya kupungua kwa mazao yetu ya viwandani si makosa ya viongozi wa viwanda peke yao. Kwa kweli tunao mameneja wanaofanya kazi kwa bidii kwa saa nyingi kila siku. Lakini baadhi ya wafanyakazi wetu viwandani, katika maofisi na madukani nao hawajatambua bado kwamba kwa kadiri haki za mfanyakazi zinavyozidi kuheshimiwa ndivyo wajibu wake pia unavyoongezeka. Maana tumefuta kabisa utaratibu wa nidhamu ya vitisho; sasa ni vigumu sana kwa meneja ama mwajiri yeyote kumfukuza mfanyakazi, au hata kumsimamisha kazi au kumpiga faini kwa ajili ya uzembe kazini. Lakini katika Tanzania si jambo la ajabu meneja kufungiwa nje ya ofisi yake na wafanya kazi. Lakini hatujaweza kujenga kila mahali nidhamu inayotokana na watu kuelewa wajibu wao, na kufanya juhudi ya pamoja ya kuongeza mazao. Ingawa sasa hivi mawazo yanabadilika, lakini bado mahali pengi matawi ya TANU na NUTA ni hodari zaidi kwa kumtetea mfanyakazi mzembe pale kiwandani; kuliko kuwatetea wakulima na wafanyakazi wa Tanzania kwa ujumla, ambao wanaoumizwa na ubovu na uzembe wa mfanya kazi huyo.

Ni jambo muhimu kwetu kutilia mkazo suala la nidhamu viwandani. Uzembe kazini, au kushindwa kufanya kazi ya kutwa kwa ujira wa kutwa, ni aina ya unyonyaji; ni unyonyaji wa mtu kuwanyonya wenzake nchini. Na bila ya shaka uzembe umeongezeka toka kupitisha Azimio la Arusha. Mameneja na wafanya kazi wote wanahusika na tabia hii, na kila kundi liko tayari kulaumu kundi lingine. Ukweli ni kwamba kila mmoja wetu lazima aondoe uzembe wake, na awe tayari kuufichua uzembe wa wengine mahali panapostahili. Mameneja lazima wawashirikishe wafanya kazi wao katika kazi hii; lazima na wao wawe radhi kukosolewa, na

kuwasahihisha wenzao. Na hivyo ndivyo inavyopasa kuwa kwa wafanyakazi katika ngazi za chini zaidi. Tarishi asiyepeleka barua kwa haraka anaweza kusababisha hati ya kuagizia vitu ikapotea, au vitu vilivyoagizwa kuchelewa, na kazi yote ya kiwandani ikasimama. Uzembe wa kusimamia mashine ya kiwandani au basi la kubebea abiria, unaweza kugharimu maelfu ya shilingi ya fedha za Umma. Lazima matawi ya Chama yawe macho zaidi kupambana na fikira na vitendo vya namna hiyo. Kutetea uzembe si ujamaa, ni upumbavu, tena upumbavu wa hali ya juu.

Lazima kila shirika lichunguzwe hali yake ya ufanisi na kujaribu kutafuta njia za kupunguza gharama au za kuongeza mazao kutokana na rasilimali iliyopo, Katika sehemu nyingine kazi hii imekwishaanza. Shirika la Maendeleo ya Taifa limeanza kufanya kazi ngumu ya kutafuta namna ya kupunguza gharama na kuongeza ubora wa bidhaa katika makampuni yake yote. Lakini kazi hii ni muhimu na lazima ifanywe na mashirika yetu yote. Na lazima tujue katika kila kampuni shabaha zinazotarajiwa ili iwezekane kupima ufanisi. Kipimo hiki kitahitilafiana kama zinavyohitilafiana kazi za mashirika. Kwa mfano kinaweza kikawa ni uwiano wa mabasi mazima yanayotembea mabarabarani kulinganishwa na yale yanayotengenezwa karakarani; au wingi wa nguo zilizotengenezwa, au idadi ya majembe, n.k. yaliyotengenezwa na kuuzwa kulinganisha na rasili mali iliyoko, idadi ya wafanya kazi, na kadhalika. Jambo hili ni muhimu sana. Kutoshelezwa kwa shabaha zetu, na kuongezeka kwa mapato ya wananchi wetu, kunategemea ufanisi wetu katika kuzalisha mali.

# SURA YA PILI

## Kujenga Msingi wa Uchumi wa Ujamaa wa Taifa Linalojitegemea[3]

### *Mwongozo 1981*

*Hii ni sehemu ya Tatu ya Mwongozo wa 1981 uliopitishwa na Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi uliofanyika kuanzia tarehe 23 Novemba hadi tarehe 7 Desemba 1981. Sehemu hii ya Mwongozo inatoa tathmini ya utekelezaji wa siasa ya ujamaa na kujitegemea hususan katika sekta ya viwanda na kilimo ……*

[…]

67. Lengo kuu la mapinduzi ya Tanzania ni kujenga nchi ya ujamaa ambamo unyonyaji wa mtu na mtu utakuwa umetokomezwa, ambamo uchumi wa taifa utakuwa unamilikiwa na kudhibitiwa na umma wa wakulima na wafanya kazi washirika na ambamo uhusiano wa watu katika jamii utakuwa ni wa udugu na kushirikiana kwa maendeleo ya wote na ambamo kazi imepewa hadhi ya kuwa wajibu wa kila mtu.

68. Uamuzi wa kujenga Ujamaa Tanzania ni uamuzi wa kimsingi na kihistoria na haubadiliki. Chama kilijua tangu mwanzo kuwa kujenga ujamaa hakungekuwa mteremko bali ni mapambano magumu dhidi ya ubepari na unyonge wa humu humu ndani na dhidi ya njama za ubeberu wa dunia. Na isitoshe, Chama kilijua tangu mwanzo kuwa kujenga Ujamaa pia ni mapambano dhidi yetu wenyewe katika ubinafsi na upungufu wetu wa aina mbalimbali. Harakati za miaka kumi na minne tangu Azimio la Arusha zimetudhibitishia ukweli huu.

---

[3] CCM 1986. Mwongozo wa CCM; Dodoma; Idara ya Uenezi na Ushirikishaji Umma. Uk. 54-76.

69. Mapambano ya kutekeleza siasa ya Ujamaa ya Chama katika miaka kumi na minne tangu Azimio la Arusha yametuwezesha kufanya mabadiliko ya kimsingi katika uchumi wa nchi yetu. Kabla ya Azimio la Arusha uchumi wetu ulikuwa na mfumo wa kikoloni mamboleo kwani benki, bima, biashara ya nje yote yalikuwa matawi tu ya makampuni ya kibepari ya ulaya na Marekani wakati mazao ya kilimo cha biashara yaliwekewa lengo la kutumikia viwanda vya kibepari vya nchi za ng'ambo.

70. Kutaifishwa kwa benki, bima na kampuni za biashara za nje za kibepari na kuanzishwa kwa mashirika ya biashara ya ndani na ya nje katika kutekeleza Azimio la Arusha kumeleta marekebisho ya kimapinduzi ya mfumo wa uchumi. Hatua thabiti zimechukuliwa pia za kuanzisha na kupanua viwanda vinavyotumia bidhaa asili za kilimo chetu kama ngozi, pamba, katani, korosho, tumbaku, pareto, miwa na kadhalika. Kwa upande wa kilimo hatua za mwanzo zimechukuliwa kukielekeza kwenye mfumo wa kijamaa: sehemu kubwa ya mashamba ya kibepari, hasa ya mkonge ilitaifishwa, mashamba makubwa kadhaa ya Taifa ya kilimo na ya ufugaji yameanzishwa wakati sekta ya ujamaa katika baadhi ya vijiji imeanza kushamiri. Tanzania Visiwani, Serikali ya Mapinduzi ilitaifisha ardhi, benki, nyumba na kuanzisha mashirika ya biashara ya nje na ya ndani na kuanzisha viwanda vinavyotumia miwa na mbata. Hatua zote hizi zilizochukuliwa zimetujengea msingi wa uchumi wenye mwelekeo wa nchi ya ujamaa. Mafanikio haya yamewezekana kutokana na kazi, ujasiri na kujitolea mhanga kwa wakulima na wafanyakazi chini ya uongozi wa Chama.

71. Lakini, pamoja na mafanikio haya, nchi yetu hivi sasa imekumbwa na hali mbaya ya uchumi kama vile hali hiyo ilivyozikumba nchi zote duniani, zilizoendelea na zisizoendelea, nchi kubwa na ndogo, za kibepari na za kijamaa. Hali hii lazima tuikabili kwa kujipa kazi mbili ambazo zitakwenda sambamba. Kazi moja ni kutekeleza malengo ya muda mrefu ya kujenga msingi wa uchumi wa kijamaa wa Taifa linalojitegemea. Na kazi ya pili ni kuchukua hatua thabiti kuanzia sasa za kujihami kiuchumi ili

kuhakikisha kuwa hali ya uchumi wetu haiendelei kudidimia na kuathiri hata msingi tuliokwisha ujenga.

72. Ni muhimu kutamka hapa kuwa siasa ya uchumi ya Chama cha Mapinduzi ina lengo la kutosheleza mahitaji ya wananchi ya chakula na kulipa Taifa uwezo wa kujitegemea katika mahitaji ya maendeleo ya sasa na ya baadaye.

**MWELEKEO WA MAENDELEO YA UCHUMI NA JAMII YA MUDA MREFU**

73. Chama Cha Mapinduzi kimekwishatoa mwelekeo wa maendeleo ya uchumi na jamii kwa miaka ishirini ijayo. MWONGOZO wa Chama unayazingatia na kuyafanya maelekezo hayo ndiyo msingi wa mwelekeo wake wa uchumi na wa jamii kwa kipindi hicho.

74. Kwa hiyo, Mwongozo wa Chama hautayakariri yaliyomo katika mwelekeo wa miaka ishirini isipokuwa kusisitiza juu ya masuala yanayohitaji mkazo maalum pia ni kutoa mwelekeo mpya pale ambapo pana umuhimu wa kutazamwa upya na hapa kushughulikiwa na mwelekeo wa maendeleo ya miaka ishirini.

75. Mambo makubwa mawili yanastahili kutajwa katika kiwango hiki. La kwanza linahusu kilimo. Kwa kuwa kilimo ndio msingi wa maendeleo yetu ya sasa na ya miaka mingi ijayo, ni muhimu kwa Chama kulititilia mkazo suala hili kwa kufanya ufafanuzi wa nafasi ya kilimo katika maendeleo ya uchumi wa taifa na njia inayohitajika kuhudumia maendeleo hayo. Hivyo, suala la kilimo na hasa kilimo cha kijamaa linapewa nafasi kubwa katika mwongozo huu.

76. Jambo la pili linahusu mfumo wa upangaji wetu wa maendeleo. Kwa kuzingatia kwamba maendeleo ya kijamaa ni maendeleo yaliyopangwa, Chama katika kipindi kinachoanza sasa kitalitazama kwa undani zaidi suala la upangaji wetu wa mipango ya maendeleo kwa madhumuni ya kuimarisha na kukaza usimamizi wa utekelezaji. Chama kitaona kama Tume ya Mipango katika sura yake ya sasa kinatimiza makusudio ya Chama. Wakati huo huo

Tume ya Bei itafanyiwa uchambuzi ili ipatiwe nafasi yake ya kuwa chombo cha upangaji wa uchumi badala ya kuwa chombo cha biashara kama ilivyo sasa. Sifa moja kubwa ya uchumi wa kijamaa ni kuwa uchumi wa mpango tofauti na uchumi wa kibepari ambao ni uchumi wa soko. Uchumi wetu kwa sasa ni mchanganyiko: kwa sehemu fulani unapangwa na kwa sehemu kubwa unategemea mvutano wa soko. Chama kitalitazama suala hili kwa undani zaidi ili kuelekeza zaidi uchumi wetu kwenye mfumo wa uchumi wa mpango kuliko ilivyo sasa. Nafasi ya Tume ya Mipango na Bunge katika kupanga; na kusimamia utekelezaji wa mipango itatazamwa upya. Aidha: matumizi ya fedha za kigeni yataingizwa katika mfumo wa upanga, mipango.

77. Kwa kuwa uchumi wa kijamaa ni uchumi wa mipango, basi tutahitaji watu wenye taaluma ya kupanga katika taifa. Mikoa, Wilaya na Vijiji na kwa viwango mbalimbali vya utaalamu. Hivyo Serikali itawajibika kuwaandaa mapema iwezekanavyo wataalamu wa mipango kwa wingi. Wakati huo huo ihakikishwe kuwa upangaji wa kinchi unapewa uzito sawa na upangaji wa kimradi ambao ndio unaoeleweka zaidi na wataalam wetu.

## A. MAPINDUZI KATIKA KlLIMO NDIYO KAZI YA UMUHIMU WA KWANZA

78. Msingi wa uchumi wa nchi yetu ni kilimo. Asilimia themanini na tano ya Watanzania wanaishi kwa kilimo; biashara yetu na nchi za kigeni inategemea zaidi mazao tunayoyatoa katika kilimo; viwanda vichache tulivyonavyo nchini vinategemea m;azao ya kilimo; uwezekano wa kutoa ziada itakayowezesha nchi kugharimia mapinduzi ya viwanda (kugharimia viwanda vya madawa) upo katika sekta ya Kilimo.

79. Katika hali hii, uongozi na usimamizi thabiti na makini wa Chama cha Mapinduzi uelekezwe zaidi katika sekta hii ya uchumi wa Taifa, Kazi iliyo mbele yetu ni kuleta mapinduzi katika kilimo. Kwa kuwa asilimia themanini na tano ya Watanzania ni wakulima wa vijijini basi mkazo wa mapinduzi katika kilimo lazima uwe

kilimo cha: vijijini wakati mashamba ya Taifa pia yanashughulikiwa.

80. Mapinduzi ya kilimo vijijini katika nchi yetu ni kilimo cha kijamaa na cha kisasa ambacho kina sifa zifuatazo: Kwanza ni kilimo cha mashamba makubwa ya kijamaa ya vijiji, pili ni kilimo kinachotumia pembejeo, zana za utaalamlu na tatu ni kilimo kinachotekelezwa kwa utaratibu bora wa kazi unaoleta ufanisi.

81. Sifa moja ya kilimo cha kisasa duniani kote ni kuwa ni kilimo cha mashamba makubwa. Tofauti iliyopo ya mashamba hayo ni katika umilikaji. Katika nchi za kibepari mashamba hayo makubwa ni mali ya mabepari, wakati katika nchi za kijamaa mashamba hayo makubwa ni mali ya Taifa au ni mali ya ushirika wa wanavijiji. Hali hiyo imeanza kujitokeza pia katika kilimo cha kisasa nchini Tanzania.

82. Mantiki iliyokisukuma kilimo cha kibepari cha kisasa kiwe cha mashamba makubwa ni ile ile iliyokisukuma kilimo cha kijamaa cha kisasa kiwe cha mashamba makubwa. Kilimo cha kisasa ni kilimo cha zana, na ukishavuka kilimo cha pIau za maksai na kuingia katika matrekta na mashine nyingine za kupandia na kuvunia, basi ni hasara kubwa kuzitumia zana hizo katika vishamba vidogo vidogo vya ekari kadhaa tu. Ufanisi wa hali ya juu unapatikana wakati zana hizo zinatumika katika maeneo makubwa. Wakati huo huo ni kuwa zana hizi za kisasa ni aghali na haiwezekani kwa kila mkulima mwenye ekari chache kupata uwezo wa kuzinunua hata katika nchi za kibepari. Hivyo, katika nchi za kibepari ni wakulima wakubwa tu ndio wenye uwezo wa kumiliki zana hizi na katika mashindano hayo, wakulima wadogo wamelazimika kutoa nafasi kwa wakulima wakubwa. Katika nchi za kijamaa uwezekano wa kumiliki zana hizi ni kwa kupitia Serikali (Mashamba ya Taifa) na ushirika wa wakulima vijijini.

83. Uwezekano wa kuanzishwa kwa mashamba makubwa ya ujamaa vijijini ni mkubwa katika Tanzania maana mafanikio yaliyopatikana mpaka sasa katika vijiji vilivyotekeleza ujamaa

vijijini yameufungua macho umma wa Wakulima vijijini. Wakati huo huo maeneo ya kuanzisha na kupanua mashamba ya ujamaa hayana matatizo katika sehemu kubwa ya vijiji vyetu nchini mradi tu kuna nia, mipango na uongozi thabiti.

84. Wakulima vijijini wamepiga hatua za mwanzo katika kutekeleza maagizo ya Siasa ni Kilimo kwa upande wa masharti ya kilimo bora cha mazao ya chakula na mazao ya biashara. Pembejeo za viwanda na samadi zimeanza kutumika pia. Katika siku za usoni Chama kitawajibika kufanya mambo mawili kuendelea kuwaelimisha wakulima juu ya umuhimu wa kutimiza masharti ya kilimo bora na kuhakikisha kuwa serikali inakuwa na mipango thabiti ya upatikanaji wa pembejeo na kwa bei nafuu kwa wakulima. Matumizi ya samadi lazima yahimizwe kwa mkazo zaidi.

85. Suala la zana za kisasa ni gumu zaidi. Hivi sasa sehemu kubwa ya kilimo vijijini inalimwa kwa jembe la mkono. Kuna maeneo yenye mifugo mingi ambako kazi ya kilimo inaendeshwa pia na pIau za kuvutwa na maksai. Yapo pia matrekta katika baadhi ya vijiji. Lengo la Chama katika miaka ijayo ni kumtoa mkulima kutoka kwenye hali yake ya sasa ya kutegemea jembe la mkono na kumfikisha kwenye kutumia zana za kisasa. Kazi hiyo, pamoja na ya kuhakikisha kuwa matumizi ya mikokoteni yanaenea vijijini kote lazima itekelezwe kwa nguvu zote.

86. Wakati huo huo Chama kihakikishe kuwa serikali inaagiza matrekta toka ng'ambo kwa kuzingatia uwezo na uzito unaolingana na umuhimu wa kilimo kwa maendeleo ya Taifa letu. Kupanga ni kuchagua. Hivyo, kama kwa mfano, ni kuchagua kati ya magari madogo na matrekta, basi uzito uwe kwenye matrekta. Lakini, kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi wetu (upungufu wa fedha za kigeni na kwamba hatuna viwanda vyetu vya chuma na vya matrekta), itachukua muda wa miaka mingi kabla ya kilimo cha trekta kuwa ndicho kilimo cha vijiji vyetu. Kwa sasa mbinu ya kutufikisha huko siyo kungoja matrekta bali ni kutumia majembe ya mkono na pIau za maksai katika kilimo cha kijamaa na cha binafsi vijijini ili kuongeza ziada ya mazao kitaifa ambayo ndiyo ufunguo wa

kulipatia Taifa uwezo wa matrekta zaidi na kukuza uwezo wetu wa kuanzisha viwanda mama na vinginevyo.

87. […]

88. Lakini mapinduzi katika kilimo nchini lazima pia yaambatane na mapinduzi ya msimamo wa serikali na vyombo vyake kuhusu nafasi ya kilimo katika mapambano ya ujenzi wa taifa. Katika siku za usoni, Chama kitahakikisha kuwa serikali na vyombo vyake, kwa vitendo, vinautekeleza wajibu wake wa kuhudumia na kusukuma maendeleo ya kilimo, kilimo cha kijamaa kikipewa nafasi ya kwanza.

89. Mapinduzi katika msimamo ni pamoja na kuupiga vita umangi meza na mila na tabia zinazopingana na mahitaji ya kilimo cha kisasa na pia kubuni njia bora zaidi za kuandaa wataalamu watakaohitajika sana vijijini kama zile zilizotuwezesha kutekeleza Azimio la Musoma kuhusu Elimu ya msingi kwa wote. Kwa kuwa kilimo cha kijamaa ni kilimo cha mashamba makubwa, basi ihakikishwe kuwa mafunzo ya kilimo yanazingatia pia suala la menejimenti ya mashamba makubwa.

## B. HATUA NYINGINE ZA UMUHIMU WA KWANZA KATIKA UCHUMI

90. Pamoja na maelekezo ya maendeleo ya miaka ishirini yaliyokwishapitishwa na Chama, masuala yafuatayo yanahitaji kusisitizwa:

### (1) Kilimo cha umwagiliaji maji

Kilimo hiki kimepewa umuhimu wake katika mwelekeo wa muda mrefu. Kwa kuelewa kuwa pamoja na miradi mikubwa ya kitaifa ya umwagiliaji, miradi midogo midogo ya vijijini ndiyo ambayo inaweza kutoa matunda ya haraka, hatua za dhati zichukuliwe za kuandaa wataalam wa fani hiyo kwa wingi nchini na ng'ambo na pia kutafuta uwezekano wa kuanzisha kiwanda cha zana za umwagiliaji maji. Wakati huo Chama kijizatiti barabara ili kuimudu kazi ya kuwashirikisha wananchi, maana utekelezji wa miradi ya

umwagiliaji vijijini utategemea zaidi jasho la wananchi wenyewe kuliko matumizi ya zana za kisasa.

**(2) Kilimo cha matunda na mboga**

Kilimo hiki hadi sasa hakijatiliwa mkazo nchini. Licha ya mahitaji ya chakula bora yanavyozidi kuongezeka, matunda na mboga yanaweza kuwa mazao muhimu ya biashara ya nje kwa nchi yetu. Nchi nyingi za Afrika ambazo hazina mazingira bora zaidi ya haya ya nchi yetu hujipatia fedha nyingi za kigeni kutokana na matunda na mboga. Chama kihakikishe kuwa miradi ya Taifa na ya vijiji ya kilimo cha matunda na mboga inaanzishwa kwa madhumuni ya kuwapatia wananchi matunda na mboga za kutosha nchini kote na ziada ya kuuza ng'ambo. Katika lengo maalum la kuwapatia wafanyakazi wa mijini matunda na mboga kwa wingi, vijiji vilivyo karibu na miji mikubwa visaidiwe kuanzisha miradi mikubwa ya vijiji ya mazao haya.

**(3) Uendelezaji wa mifugo na ufugaji**

Tanzania ina utajiri mkubwa wa mifugo hasa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Inakisiwa kuwa idadi ya ng'ornbe peke yake waliomo nchini ni zaidi ya milioni kumi. Lakini hali ya mifugo yenyewe ni duni maana wafugaji walio wengi bado wanathamini zaidi wingi wa mifugo badala ya ubora wa mifugo. Misingi ya ufugaji wa kisasa haijafikishwa ipasavyo kwa wananchi na aina bora za mifugo kwa ajili ya maziwa na nyama hazijaenezwa nchini.

Katika hali hii kazi kubwa ya Chama katika fani ya mifugo itakuwa kuhakikisha kuwa Serikali inaandaa sera ya kuendeleza mifugo nchini na kuhakikisha kuwa wafugaji wanaelimishwa na wanatekeleza misingi ya ufugaji wa kisasa na kuchukua hatua za dhati za kueneza mbegu bora za ng'ombe wa maziwa na wa nyama

Chama kitaongoza jitihada za kuanzisha na kupanua ufugaji wa kijamaa vijijini kwa njia ya ranchi za ng'ombe bora wa maziwa na ranchi za vijijini za kunenepesha mifugo. Katika hali hiyo, suala la mipango bora ya ardhi vijijini linakuwa la umuhimu wa kwanza.

Jingine la kulikabili ni suala la uhaba wa nyama, maziwa na mayai na bei za juu mno za mazao hayo nchini. IIi kulipatia ufumbuzi tatizo hili, Chama kitawajibika kuhakikisha kuwa serikali inaingiza katika mipango yake miradi mikubwa ya ufugaji wa kuku, nguruwe na ng'ombe karibu na miji mikubwa. Aidha, Chama na Serikali visaidie vijiji vinavyozunguka miji kuanzisha miradi ya ufugaji hasa wa kuku, nguruwe, sungura na ng'ombe wa maziwa.

Wakati huo huo, jitihada za kueneza mifugo katika maeneo yasiyo nayo ya kutosha itabidi isimamiwe na Taifa. Pamoja na kwamba wafugaji wengi wa Tanzania wana mifugo mingi, bado wengi wao hawaitumii wala kuiona mifugo kama chombo cha kuwaletea maendeleo na maisha bora zaidi. Hivyo, suala la kutumia mifugo ili kuinua hali halisi ya maisha ya wafugaji na ya vijiji vyao lazima liwe mkabala maalum wa Chama kuanzia sasa.

**(4) Viwanda**

Jambo la kusisitiza linahusu hali ya utengenezaji mali katika viwanda vilivyopo nchini hivi sasa ambapo vilivyo vingi havitengenezi mali kwa kadiri ya uwezo vilivyo nao. Chama itabidi kijihusishe na matatizo ya viwanda hivi na kuhakikisha kuwa vinapata misaada yote ili viweze kutengeneza mali kwa kadiri ya uwezo wake. Licha ya matatizo ya vipuri na utaalam, viwanda hivi vinakabiliwa pia na matatizo ya kisiasa kama vile upungufu wa mwamko wa siasa na utovu wa nidhamu.

Viwanda vingi tulivyonavyo nchini hutoa makapi ambayo yangeweza kutumika kwa utengenezaji wa bidhaa nyingine, lakini jitihada hiyo haijafanywa. Viwanda kama vya sukari, mafuta, mbolea, nyama na vya nguo ni miongoni mwa viwanda vya aina hiyo. Kuanzia sasa Serikali itawajibika kuandaa mipango ya kuyatumia makapi yatokanayo na viwanda vya aina hiyo ili kutengeneza bidhaa zinazoweza kutengenezwa.

Chama pia kitatilia mkazo utekelezaji wa Agizo la Viwanda Vidogo Vidogo mijini na vijijini. Chama kitahakikisha kuwa kila Mkoa

unaandaa mpango wa muda mrefu wa utekelezaji wa Agizo hili la viwanda vidogo.

[…]

## C. MAENDELEO YA JAMII

91. Katika kipindi kinachoanzia sasa Chama kitatilia mkazo suala la ujenzi wa tabia na maadili ya kijamaa nchini. Pamoja na jitihada iliyofanywa ya kutoa elimu na kuunda vyombo vya umma, jamii yetu bado inazo mila, tabia na maadili yaliyo kinyume na maadili ambayo yanafanana na misingi ya siasa ya ujamaa tunayokusudia kuijenga.

92. Watu wameanza kuthamini zaidi vitu kuliko utu na tamaa ya kujipatia mali bila ya kuitokea jasho inaenea, matukio ya wizi wa mali ya umma yameongezeka. Lakini Iililo baya zaidi ni kuwa mwizi wa aina hiyo anapogunduliwa, baadhi ya wananchi badala ya kumfichua au kulaani kitendo chake, humsifu na kumhusudu. Wakati mwingine mvivu na mtegaji kazini hutetewa hata na vyombo vya Chama vyenyewe. Wakati huo huo, bado kuna mabaki ya tabia ya kupuuza elimu ya shule kwa watoto na badala yake kuna wazazi wanaopendelea watoto wao wachunge mifugo au hata kuolewa badala ya kuendelea na shule.

93. Jitihada ya Chama za kujenga tabia na maadili ya kijamaa itaelekezwa kwenye taasisi muhimu za nchi kama shule na vyuo, majeshi na sehemu za kazi. Lakini Chama kitahakikisha pia kuwa maisha ya hadhara ya jamii yetu yanasaidia kujenga misingi ya tabia na maadili ya Taifa linalojenga ujamaa na la kimaendeleo kwa ujumla. Hivyo, Chama kitapiga vita tabia ya baadhi ya wananchi na hasa wakiwa viongozi inayokwaza na kupotosha umma. Jamii lazima iwe shule ya kwanza ya maadili ya kijamaa.
[…]

### (5) Nishati

Suala la nishati ni la msingi kwa maendeleo ya Taifa letu. Pamoja na kuendelea kutafuta mafuta, Chama kitahakikisha kuwa serikali

inazidisha mipango thabiti itakayoliwezesha Taifa kuanza kutumia nguvu za maji, mkaa, upepo na jua. Pamoja na miradi mikubwa ya nguvu za maji kuna haja ya kutia maanani miradi midogo midogo ya nguvu za maji. Suala la kuni itabidi lipewe umuhimu mkubwa kwa kuwa na mipango kamambe ya kupanda miti vijijini na miradi ya Mikoa na Taifa. Chama kiihimize Serikali kuendelea na kutafuta mbinu za kutumia makaa ya mawe tuliyonayo kusukuma uchumi wetu. Umuhimu wa suala la nishati utahitaji sera maalum.

**(6) Msimamo juu va kuendeleza sayansi na teknolojia**

Mpango wa miaka ishirini unatoa mwelekeo wa maendeleo ya sayansi na teknolojia, kwani sayansi na teknolojia ni msingi muhimu kwa maendeleo ya kisasa. Chama kijihusishe zaidi na mipango ya kuwapata wanasayansi na wanateknolojia wenye uwezo wa viwango mbalimbali vya utaalamu na msimamo sahihi wa siasa. Wakati huo huo, Chama kishughulikie ustawi wa wataalamu na mabingwa tulionao hivi sasa nchini ili kuhakikisha kuwa wanaishi katika mazingira yanayowawezesha kutoa mchango wao kwa ukamilifu katika ujenzi wa Taifa letu. Kutokana na kukosa msimamo sahihi wa kuwashughulikia wataalamu wetu kumewafanya baadhi ya wataalam kubabaika na Serikali kupoteza mabingwa katika fani za uganga, uhandisi, urubani wa ndege na kadhalika.

Maendeleo ya uchumi wetu hasa kwa upande wa viwanda na nishati utahitaji mafundi wa viwango mbalimbali kwa wingi sana. Chama kihakikishe kuwa serikali inakuwa na mipango thabiti ya namna ya kuwapata mafundi hawa na kwamba inatumia nafasi zinazoweza kupatikana kuwaandaa hapa nchini na ng'ambo.

94. Chama kitakuwa na utaratibu wa kuandaa mikutano na wataalamu wa fani mbalimbali ili kubadilishana mawazo juu ya mbinu za kusukuma mbele mapinduzi katika sayansi na teknolojia nchini.

# SURA YA TATU

## Hotuba ya Mwenyekiti Kwenye Mkutano Mkuu wa CCM[4]

***Julius K. Nyerere***

*Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu Julius Nyerere alihutubia mkutano mkuu wa CCM uliofanyika Mwezi Oktoba 1982. Katika Hotuba yake Mwalimu alitoa taarifa juu ya hali ya uchumi wa nchi, na kutangaza vita vya uchumi …*

[…]

Ndugu Wananchi. Tarehe Februari 1977, nilitoa taarifa kwa chama na kwa Taifa hili juu ya hali ya uchumi na maendeleo ya jamii katika nchi yetu Miaka kumi baada ya Azimio la Arusha. Ilikuwa taarifa iliyoonyesha maendeleo makubwa. Ilionyesha hatua tulizokuwa tumezipiga kuelekea kwenye malengo yetu ya Ujamaa. Maendeleo tuliyokuwa tumeyapata katika hali yetu ya maisha, hasa kuhusu nafasi za elimu, afya na huduma nyingine za umma. Vile vile taarifa hiyo ilionyesha kuwa tulikuwa tumejenga viwanda vingi kwa shabaha ya kujitosheleza kwa mahitaji yetu na kusindika mazao yetu kabla ya kuyauza katika nchi za nje.

Lakini mwisho, wa taarifa hiyo ya 1977 nilitoa tahadhari, ambayo napenda kuirudia tena. Nilisema hivi:

> ‘’Hakuna shaka hata kidogo kwamba maendeleo ya uchumi wa Tanzania katika kipindi cha miaka mitatu au minne ijayo yatakuwa magumu kabisa. Juhudi zetu lazima zilingane na hali ya kupambana na matatizo hayo.

[4] CCM 1987. Majadiliano ya Mkutano Mkuu wa Kawaida, Oktoba 1982: Taarifa Rasmi; Idara ya Uenezi wa Siasa na Ushirikishaji Umma, Dodoma. Uk. 68-132.

Tunayo sababu ya kufurahia mafanikio yetu ya kipindi hiki cha miaka kumi iliyopita. Lakini hatuna sababu hata kidogo ya kuridhika. Tumefanikiwa kiasi kizuri; lakini kwa juhudi zaidi, na maarifa zaidi tungeweza kufanikiwa vizuri zaidi.

Katika kipindi cha miaka kumi ijayo lazima tujenge katika msingi tuliouweka. Lazima tuongeze sana nidhamu, ufanisi na kujitegemea kwetu. Na hasa lazima tujitahidi zaidi katika kutafuta njia za kujitekelezea mipango yetu sisi wenyewe na kwa kutumia rasilimali zetu sisi wenyewe: na halafu kuitekeleza mipango hio

Hayo niliyasema mwaka 1977.

Kazi yangu ya leo ni kutoa taarifa juu ya kipindi cha miaka mitano iliyopita; yaani kuanzia 1977 hadi 1982. Ni taarifa ndefu sana; lakini si ya kupendeza. Lakini sidhani kama kuna Mtanzania yeyote anayetazamia kuwa taarifa yangu ya leo itasema kwamba tumepiga hatua ya maendeleo bila ya matatizo na vikwazo: maana Watanzania wanafahamu kuwa ukweli wenyewe ni kinyume kabisa. Kipindi hiki kimekuwa ni kipindi cha matatizo makubwa sana. Na wala hakuna mtu mkweli yeyote nje ya nchi hii atakayesema kuwa taarifa yangu haifanani na hali halisi ya dunia; wale wanaoishi nje ya nchi yetu wanapata matatizo kama haya tuliyo nayo. Tanzania ni sehemu ya dunia hii hii, na uchumi wa dunia kwa sasa hivi unakumbwa na matatizo makubwa sana. Na madhali uchumi wa dunia nzima unayumba, uchumi wa Tanzania, ambayo ni sehemu ya dunia, lazima nao utayumba.

Nchi tofauti kabisa kwa siasa na hali ya uchumi kama Mexico, Poland, Ufaransa, Uingereza, Bangladesh, Argentina, Indonesia, Rumania na nyingine nyingi, zina matatizo makubwa ya watu wengi sana kukosa kazi, madeni makubwa ya kimataifa, na kuanguka kwa hali za maisha. Kwa mfano, Canada ina watu milioni $1^{1\backslash 2}$, au asilimia 12.2 ya watu wazima, wasiokuwa na kazi wala shamba la kulima. Marekani kuna watu milioni 11.25, au zaidi ya asilimia 10 wasiokuwa na kazi. Hii ni kiasi kikubwa zaidi kuliko wakati

wowote katika miaka 40 iliyopita. Na idadi ya makampuni ya kimarekani yanayofilisika hivi sasa kwa sababu ya matatizo ya uchumi ni kubwa zaidi kuliko wakati wowote katika miaka 50 iliyopita! Nchi za Jumuiya ya Ulaya Magharibi zina watu milioni 10.9, au asilimia 9.6, wasiokuwa na kazi. Mexico, nchi ambayo ina mafuta mengi, ina madeni ya dola za Marekani milioni 80,000 (au shilingi milioni 720,000); Chile inahitaji kupata mkopo kutoka IMF wa dola za Marekani milioni 890; Uingereza, nchi nyingine yenye mafuta mengi, ina watu milioni 3.4 wasiokuwa na kazi, na hali ya maisha imeanguka kwa asilimia 2 kutoka mwaka jana. Hata nchi zenye uchumi mzuri kama Japan na Ujerumani Magharibi hazikuepuka kukumbwa na matatizo ya uchumi wa dunia yaliyoko sasa. Katika Bara letu, kila nchi ya Afrika ina matatizo yanayotofautiana kwa uzito tu, kutokana na kama nchi ina mafuta ama haina; lakini ni matatizo ya aina ile ile. Hata nchi zenye mafuta, na zinazouza mafuta, kama Nigeria na Libya, nazo zina matatizo makubwa ya uchumi.

Ukweli huu haufanyi hali yetu iwe nzuri zaidi; wagonjwa kuwa wengi hakupunguzi maumivu. (*Kicheko*) Lakini unayaweka matatizo yetu katika sura yake kamili. Na yanaonyesha mazingira Tanzania inamoishi na kufanya biashara. Tutake tusitake, tumeathiriwa vibaya sana na mazingira hayo. Vilevile tumeumizwa sana na matukio mengine yaliyo nje ya uwezo wetu. Ni vizuri kuuzingatia ukweli huu kwa sababu maadui zetu wanayo tabia ya kubwata kwamba matatizo yetu yanatokana hasa na siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea; na Watanzania wenye mioyo midogo siku nyingine hudhani kuwa labda ni kweli! (*Kicheko*).

Tulipopata uhuru wetu tulijipa jukumu la kuulinda uhuru huo. Wakati huo huo tukatangaza vita vya kupambana na ujinga umaskini na maradhi. Na mwaka 1967 tukatangaza na tukafafanua vizuri zaidi lengo letu, na njia ya kufikia lengo hilo, la Ujamaa na Kujitegemea. Msimamo wetu ungali pale pale. Mwanzoni mwa Novemba mwaka 1978 nililitangazia taifa letu kwamba tulikuwa tumeathiriwa katika shabaha yetu ya kwanza: sehemu ya nchi yetu

ilikuwa imetekwa ghafla na kukaliwa na mvamizi. Mwezi Aprili 1979 niliweza kutangaza kwamba tumekwisha kuirudisha tena ile sehemu ya nchi yetu iliyokuwa imetekwa, na kwamba chanzo cha udhia huo nacho kilikuwa kimekwisha kuondolewa; Utawala wa Idi Amin ulikuwa umeteketezwa. (*Makofi*).

Hali yangu ya leo inafanana kidogo na ile ya Novemba, 1978. Safari hii natoa taarifa kuwa tumepata pigo katika kutekeleza malengo yetu ya uchumi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Pato la Taifa la Tanzania limeongezeka kwa kiwango kidogo zaidi kuliko kiwango walichoongezeka watu. Maana yake ni kwamba, ukichukua mali tuliyonayo kila mwaka, ukaigawa kwa idadi ya Watanzania wote, pato la wastani la kila Mtanzania ni dogo zaidi mwaka huu kuliko lilivyokuwa mwaka 1977. Hali ya maisha ya watu wetu imeshuka.

Mwezi Novemba, 1978 tulipoteza sehemu ya nchi yetu. Lakini hatima yake tulimpiga adui na kurudisha sehemu hiyo. Leo pamoja na kutoa taarifa kwamba tumevamiwa na tumepoteza eneo katika upande wa uchumi wetu nasema pia kwamba tukipenda kushinda katika vita hivi navyo, tutashinda (*Makofi*)

Sisi hatukumwambia Iddi Amin atuvamie. Lakini kule kutokuwa tayari mapema kulifanya mwanzo tukapoteza sehemu ya nchi yetu. Ndipo tulipolazimika kukusanya na kutumia uwezo wetu wote kumrudisha nyuma mvamizi, na hatimaye kumwangamiza. Ni sisi wenyewe tuliochukua jukumu la kukusanya nguvu zetu; ni sisi wenyewe tulioamua kusimamisha baadhi ya mipango yetu mingine, ili tuvipe vita umuhimu wa kwanza. Tukashinda.

Kadhalika si sisi tuliokaribisha matatizo yanayoukabili uchumi wa nchi yetu. Lakini madhara yanayoletwa na mapigo hayo yamedhihirisha ubovu wetu na baadhi ya makosa yetu wenyewe. Kama tukifanya juhudi inayotakiwa tunaweza kusahihisha makosa yetu, na kuondoa sehemu ya ubovu wetu. Kwa kufanya hivyo na kwa kuchanganya nguvu zetu zote tulizonazo,tutashinda vita hivi vya uchumi. Mapambano haya ni magumu zaidi na ya muda mrefu

zaidi kuliko yale ya vita vya Kagera. **Lakini matatizo hukomaza**. Watu wazima hawaachi matatizo yakawapumbaza. Tanzania ya leo, pamoja na matatizo yake yote, na kwa sababu ya matatizo yake yote, ni nchi iliyokomaa zaidi kuliko Tanzania ya mwaka 1978. Kwa hiyo tukiamua kushinda vita hivi navyo, hapana shaka tutashinda. (*Makofi*).

Ili ushinde vita baada ya kurudishwa nyuma huna budi ufanye mambo matatu. Kwanza lazima unuie kuendelea kupigana. Na sisi hatuna la kufanya isipokuwa tunuie kuendelea kupigana. Tusipokubali kupigana vita hivi vya uchumi, hatuna budi tukubali kudidimia katika hali ya unyonge zaidi, na kupoteza kabisa kila tulichojijengea tangu tujitawale. Na katika hali kama hiyo tutapoteza pia uhuru wa nchi yetu. Hakuna uhuru wa kweli bila uwezo wa kuulinda uhuru huo; na wahenga wamesema mnyonge kupata chake ni mwenye nguvu kupenda.

Jambo la pili lililo lazima kama tunataka kupata ushindi ni kutambua kiasi cha hasara tuliyopata mpaka sasa, na kuchambua matatizo yanayoikabili nchi, ili tuweze kujua ubovu na makosa yetu wenyewe yaliyotuongezea uzito wa madhara.

Sharti la tatu la ushindi ni kuchukua hatua zozote zilizo lazima kusahihisha makosa na kuondoa ubovu wetu; kukusanya uwezo wetu wote, na kupigana kwa dhati katika mazingira halisi ya dunia ya leo. Na haya yote hayana budi yafanyike huku tukizingatia shabaha kubwa za harakati zetu, yaani kuushinda ujinga, umaskini na maradhi katika Tanzania na kulinda maendeleo yale ya kujenga haki ya kijamaa tuliyokwisha kuyapata.

Leo ninajaribu kueleza hali ya Tanzania ya sasa, yaani kutoa muhtasari wa matatizo yanayotukabili hivi sasa; kuonyesha nini Serikali inafanya kupambana na matatizo hayo; na kuonyesha wajibu wa Chama na wajibu wa wananchi wenyewe. Maamuzi ya Serikali hayana maana kama hayaeleweki, hayakubaliki, na hayatekelezwi. Kwa hiyo lazima maamuzi ya Serikali yawe, na yaonekane kuwa, ndani ya misingi ya siasa ya taifa letu kama

inavyotamkwa na Chama. Na lazima maamuzi hayo yatekelezwe na vyombo vya Serikali, wanachama wa CCM, na wananchi wa jumla.

Matatizo yetu ni makubwa sana; na ni ya kweli. Matokeo yake katika sehemu mbalimbali za uchumi wetu yatadhihirika zaidi kila ninapoendelea kueleza. Lakini msingi mkubwa wa matatizo yetu ni mmoja tu: **Mapato yetu na matumizi yetu hayalingani. Matumizi yetu ni makubwa zaidi kuliko mapato yetu**. Vitu tunavyouza nje ya Tanzania havitupatii fedha tunazohitaji kununua vitu tunavyotaka kutoka nje ya Tanzania: yaani vitu tuvyotaka kuwalisha, kuwavisha, kuwaelimisha na kutunza afya za watu wote, na papo hapo kupata zana, spea na malighafi za viwanda tulivyokwisha kujenga. Aidha, kwa sababu hatupati fedha za kutosha kutuwezesha kununua spea na malighafi za viwanda vyetu, au kugharamia usafiri, mbolea na madawa ya kuua wadudu kiasi cha kutosha kwa ajili ya kilimo chetu; basi hata uwezo wetu wa kujitengenezea bidhaa na kujipatia mazao humu humu Tanzania nao unazidi kupungua. Kwa hiyo upungufu wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya Tanzania unachanganyika na kuongezwa na upungufu wa bidhaa zinazotengenezwa ndani ya Tanzania. Matokeo yake ni kwamba bei zinazidi kupanda kwa sababu watu wenye fedha wako tayari kutoa bei kubwa kwa watu wachache walio na bidhaa hizo, ili wao wahodhi hicho kidogo kilichopo. Hali hiyo nayo inafanya iwe vigumu zaidi kwa huduma za umma kuendeshwa vizuri. Maana, kwanza, upungufu wa bidhaa umepunguza pia mapato ya Serikali, na pili, upandaji wa bei unafanya hizo fedha pungufu ambazo Serikali inazipa kutokana na kodi zinunue vitu na huduma kidogo zaidi.

Tarakimu chache zitaweza kuonyesha jinsi tulivyokuwa tunajaribu kuishi kwa gharama kubwa zaidi kuliko mapato yetu. Mwaka 1977, kwa bidhaa tulizouza nje ya Tanzania, tulipata shilingi 4,465 milioni, za fedha za kigeni. Lakini mwaka huo huo tuliagiza kutoka nje vifaa vya thamani ya shilingi 6,161 milioni. Mapato yetu ya fedha za kigeni yalikuwa madogo zaidi kuliko matumizi yetu. Hilo pengo la Shs. 1,696 milioni lilijazwa kwa misaada na mikopo

tuliyoipokea mwaka ule. Lakini kutokea mwaka huo wa 1977 hatujapata tena thamani ile ya fedha za kigeni kutokana na bidhaa tulizouza nchi za nje. Mwaka 1978 mapato yetu ya fedha za kigeni yalianguka kufikia thamani ya shilingi 3,671 milioni; mwaka 1981, kwa juhudi kubwa, tulisogeza mapato juu kidogo kufikia thamani ya shilingi 4,430 milioni.

Sababu moja kubwa ya kuanguka kwa mapato yetu ya fedha za kigeni inatokana na kuanguka kwa bei ya bidhaa tunazouza. Lakini mara nyingi hata kiasi cha mazao yetu tunayoweza kuuza katika masoko ya dunia nacho kimepungua: kwa mfano katani, pamba, korosho na karafuu. Kwa upande mwingine vifaa tunavyoagiza kutoka katika nchi za nje vimepanda bei mwaka hata mwaka, mpaka vimefikia thamani ya shilingi 10,003 milioni, katika mwaka 1980. Mwaka 1981 gharama hiyo ilipungua kidogo kufikia shilingi 9,282 milioni, lakini hiyo ni kwa sababu wenye mali walikataa kutukopesha, si kwa sababu mahitaji yetu yalikuwa yamepungua. Mali tuliendelea kuihitaji na kukosekana kwa vifaa na malighafi kutoka nje ndiko kulikolazimu viwanda vyetu vingi vifungwe. Kiasi cha misaada tunayopata kutoka kwa marafiki zetu hakitoshi tena kuziba pengo linaloongezeka kati ya thamani ya bidhaa zetu tunazouza nje na thamani ya vifaa tunavyoagiza. Na kwa vyovyote vile marafiki zetu wengi wanataka kutusaidia kuendelea siyo kuelea! Kwa sababu hiyo hivi sasa tuna madeni katika nchi za nje ya thamani ya shilingi 3,400 milioni, na inawalazimu wenye mali wasubiri muda mrefu kabla hawajapokea malipo yao, ama ya faida ya mikopo ya zamani, ama ya vifaa tulivyokwisha kuvinunua. Na madeni mengine yanakaribia kufika; kwa mfano, tulikubali kuanza kulipa deni la Reli ya Uhuru mwaka 1983.

Napenda kurudia. Tanzania si nchi peke yake iliyo na matatizo kama haya. Sehemu kubwa ni matokeo ya kuanguka kwa uchumi wa dunia, pamoja na maendeleo yetu wenyewe ya siku za nyuma. Lakini kusema kwamba nchi nyingi, hasa nchi nyingine za Dunia ya Tatu, ziko katika hali kama yetu, au hata mbaya zaidi, hakubadili ukweli kwamba ni sisi tunaoumia na ni sisi wenyewe tunaolazimika

kutatua matatizo ya Tanzania: ni matatizo yetu wenyewe. Hata sababu za matatizo hayo hazina maana kulingana na umuhimu wa kuyaondoa matatizo yenyewe hasa yale ambayo utatuzi wake umo katika uwezo wetu. Lakini kuelewa mambo yaliyotokea siku za nyuma, na sababu zake, kunasaidia kuelekeza hatua tunazoweza kuzichukua kutatua matatizo yetu, na kujua mambo yasiyokuwa chini ya uwezo wetu ambayo yatahitaji marekebisho ya namna nyingine kabisa.

Nimeeleza maana ya tatizo letu, au msingi wa tatizo hilo **Mapato yetu hayatoshelezi mahitaji yetu**. Huko nyuma na mara nyingi sana nimeeleza sababu mbalimbali zilizotufikisha hapa tulipo; lakini wako baadhi yetu ambao huwakubali ukweli na wanaendelea tu kulaumu ‘’serikali’’ ‘’mfanya-biashara’’ au hata ‘’Tume-ya-bei’’

Nitajaribu tena kuzieleza sababu hizo. Nimesema kwamba ziko sababu ambazo ziko nje ya uwezo wetu na sababu ambazo ziko ndani ya uwezo wetu. Ziko sababu nne ambazo ziko nje ya uwezo wetu. Na katika hizo ya kwanza kabisa, kama nilivyokwisha kusema, ni bei ya bidhaa.

Bei ya kila kitu tunachokinunua kutoka katika nchi za nje imepanda katika kipindi cha miaka mitano iliyopita: wakati mwingine imepanda mara nyingi. Mfano mmoja ni mafuta (ya petroli) kwa sababu yanaathiri gharama za kila kitu tunachokifanya. Ingawa idadi ya Watanzania imeongezeka sana, na ingawa huduma na viwanda vimeongezeka sana, bado tunatumia mafuta kidogo zaidi leo kuliko tuliyotumia mwaka 1972. Kwa sababu wakati wote tunajitahidi kupunguza gharama. Na tumejenga Bwawa la Kidatu kwa ajili ya kupata umeme. Lakini mwaka 1972 tulitumia fedha za kigeni za thamani ya shilingi 269 milioni kununulia mafuta yote tuliyoyahitaji. Kufika mwaka 1977 tulikuwa tumepunguza matumizi yetu kwa sehemu moja ya tano, lakini hata kwa mafuta hayo pungufu tulilazimika kulipa-thamani ya shilingi milioni 835 za fedha za kigeni. Mwaka 1981 tulishindwa kulipa gharama za mafuta yote tuliyoyahitaji; kama mnavyojua kulikuwako upungufu, hasa katika sehemu za mbali ya miji mikuu. Ingawa tulinunua asilimia

70 tu ya mafuta tuliyonunua mwaka 1972, lakini ilitubidi tulipe fedha za kigeni za thamani ya shililngi 2,053 (mbili elfu na hamsini na tatu) milioni! Ndiyo kusema kuwa kufikia mwaka 1981 tulilazimika kulipa gharama mara tatu kulinganisha na tulivyolipa mwaka 1977 kwa kila lita ya mafuta tuliyoagiza. Mwaka huu iko hofu kubwa kwamba tutatumia fedha kidogo zaidi kuliko mwaka jana; siyo kwa sababu bei ya mafuta imepungua, lakini kwa sababu hatuna fedha za kutuwezesha kununua hata kile kiasi kidogo cha mwaka jana.

Hali ni ile ile kwa bidhaa nyingine zote; bei zote zimepanda sana. Mwaka 1977 lori la tani 7 liligharimu shilingi 66,500, mwaka huu ni shilingi 123,500.

Wakati huo huo ambapo bei ya vifaa na bidhaa zote tunazoziagiza kutoka nchi za nje zimekuwa zikipanda; kiasi cha fedha ambazo tungezipata kwa kuuza baadhi ya mazao yetu makuu kimepungua. Tulikuwa tunapokea shilingi 40 kwa kilo ya kahawa yetu ya daraja la juu katika msimu wa mwaka 1976/77; mwaka 1981/82 tumepokea shilingi 24.40 tu kwa kilo. Bei imeanguka kwa zaidi ya asilimia 40 tu. Lakini kwa bahati mbaya kiasi cha mazao yote hayo mawili kilipungua sana katika kipindi hicho! Ng’ombe wa maskini waswahili wanasema "Hazai"

Tukizichukua hesabu hizo kwa pamoja, bei za bidhaa tulizolazimika kununa kutoka nchi za nje zilipanda, na bei tulizopata kutokana na mazao yetu tuliyouza nje zilianguka, ni dhahiri kwamba tunalo tatizo, hata kama tatizo hilo hatukulileta wenyewe. Kwa sasa tukitaka kununua lori la tani 7 tunalazimika kulima na kuuza pamba mara nne zaidi, korosho mara tatu zaidi, kahawa mara tatu zaidi au tambaku mara kumi zaidi, kuliko tulivyolazimika kulima na kuuza katika msimu wa 1976/77.

Tunalazimika ama kupata na kuuza kiasi hicho kinachohitajika; au kupunguza kiasi cha malori, mafuta, spea na mahitaji yetu mengine. ***Tumefanywa kuwa maskini zaidi kwa matukio yaliyo nje kabisa ya uwezo wetu. Ni sawasawa na unyang'anyi. Na matokeo ya***

***unyang'anyi wowote ni kumfanya yule anayenyang'anywa awe maskini zaidi kuliko alivyokuwa kabla ya kunyang'anywa huko.***(msisitizo umeongezewa).

Mabadiliko ya bei za bidhaa tunazonunua na kuuza katika nchi za nje ndiyo jambo la kwanza lililo kubwa kuliko yote lililofanya tuwe maskini zaidi, na ambalo hatuna uwezo nalo…..

Jambo la pili lilikuwa kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. […]

Sababu ya tatu ya matatizo yetu ya sasa ilikuwa ni vita. Tulipokuwa tunapanga mipango ya maendeleo kwa kipindi cha 1977/82 hatukutarajia kuwa kutakuwako gharama za kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wala tusingetarajia kuwa tungelazimika kupigana vita. Na vita vina gharama kubwa, ya fedha na ya maisha ya watu.

[…]

Jambo la nne na la mwisho hatukuwa na uwezo nalo, na ambalo liliathiri sana maendeleo ya uchumi wetu, ni hali ya hewa. Tumepata mavuno duni kwa miaka mingi mfululizo; ama tumekuwa na ukame katika sehemu kubwa ya nchi yetu, au tumepata mafuriko yaliyoharibu sana madaraja na barabara, pamoja na kuharibu sehemu ya mazao yetu.

Tumepokea misaada mingi au mikopo ya chakula kutoka katika nchi za nje, kutusaidia kupambana na mikasa hii ya hali ya hewa, na tunatoa shukrani kwa nchi zilizotusaidia kwa misaada hiyo. (*Makofi*). Bila ya msaada wao tusingeweza kupata chakula chote ambacho ilikuwa lazima kipatikane, hasa mwaka juzi na mwaka jana. Hata hivyo, kati ya mwaka 1977 na 1982 tumenunua tani 269,700 za mahindi, tani 71,600 za mchele, na tani 15,800 za ngano na kulipia zote hizo kwa fedha za kigeni zenye thamani inayokadiriwa kuwa shilingi 640 milioni.

Narudia: hatukuwa na uwezo wowote wa kuyazuia matukio haya. Hatuna kauli juu ya bei za bidhaa ama tunazouza au kununua kutoka

katika soko la dunia. Tulijaribu kuzuia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini tukashindwa. Hatukupanga kuchochea uvamizi wa Idi Amin katika Tanzania. Na wala hatuna kauli juu ya hali ya hewa. Lakini matukio yote hayo manne yamepunguza sana mali tuliyokuwa nayo na ambayo tungeweza kuitumia kwa maendeleo yetu wenyewe.

Hatuwezi kutabiri hali itakuwaje siku za usoni. Hatuna sababu za kutufanya tufikiri kwamba tunaweza kuingizwa katika vita nyingine. Lakini hakuna mtu aliye na hakika nchi gani ya Kusini au Mashariki ya Afrika itashamburiwa na makaburu. Kwa bahati mbaya hatuna sababu ya kutumaini kwamba bei za kimataifa zitabadilika kuwa nzuri kwa upande wetu; hatari ni kwamba zitazidi kuwa mbaya. Na hali ya hewa, ingawa dalili ni nzuri mwaka huu, bado haiwezi kutabiriwa.

Matatizo haya yanatokana na mazingira ya nje ndiyo sababu kubwa za mkasa wetu sasa. Lakini pia kuna fungu jingine la sababu za matatizo yetu. Hili linatokana na mafanikio yetu wenyewe. Fungu hili la matatizo ya Mafanikio, linatusaidia pia jinsi ya kuyapima matatizo yetu kwa jumla.

Mwanzo kabisa ni kupanuka kwa upeo wa matarajio ya Watanzania. Shabaha yetu katika Tanzania siku zote imekuwa kuinua hali ya maisha ya watu wetu wote. Tulisema kuwa kila mtu katika Tanzania, mwanaume, mwanamke, au mtoto, ana haki sawa ya kupata chakula cha kutosha na kilicho bora, kupata nguo za kufaa, elimu ya msingi na huduma za afya zilizo za lazima. Hatujafanikiwa bado kutoa huduma hizo za msingi kwa binadamu kuwatosheleza wananchi wote. Lakini tumepiga hatua kubwa sana katika lengo hilo mnamo miaka ishirini ya uhuru wetu.

Watu wazima miongoni mwetu wanakumbuka maisha ya vijijini yalivyokuwa kabla ya kujitawala. Katika sehemu nyingi sana za nchi hii hatukujua kunywa chai kabisa, achia mbali kunywa chai yenye sukari; hatukujua kuoga au kufua kwa sabuni, au kutumia taa ya mafuta giza lilipoingia. Waliokuwa na viatu walivivaa kwa

nadra, na hasa wakati wa siku kuu maalum. Wakati wa udogo wangu niliona wakitoka kanisani wanavua viatu (*Kicheko*). Chini ya nusu ya watoto wetu walikwenda shule, na katika hao waliokwenda shule, wengi wao waliishia darasa la nne. Tulikwenda hospitali tulipopatwa na maradhi mazito tu, isipokuwa kwa wale wachache waliokuwa na bahati ya kuishi karibu na hospitali za misheni. Karibu watoto wetu wote walizaliwa nyumbani, kwa msaada wa wakunga wa kienyeji, mama wazee wasiopata mafunzo kabisa ya kisasa

Hiyo ndiyo iliyokuwa hali ya nchi yetu wakati tunajitawala. Ndiyo hali ambayo vyama vyetu vya TANU na ASP vilivyorithi kutoka kwa wakoloni na kunuia kuibadili. Ilikuwa hali mbaya sana. Lakini kuonewa na kukatishwa tamaa na wakoloni kuliwafanya wananchi wengi wanyamaze na kuonekana kama kwamba wanaikubali hali mbaya hiyo. Leo sivyo mambo yalivyo. Uhuru umeinua upeo wa matarajio yetu na kutupa haki ya kunung, unika kama matarajio haya hayakutimizwa. Kwa hiyo sasa tukikosa sembe au mkate tutanung'unika; japo kama mtama upo na huko nyuma tulikuwa hatuli sembe wala mkate. Watu wengi wanatarajia kunywa chai yenye sukari angalau mara moja kila asubuhi, na wakati mwingine zaidi ya mara moja kutwa. Mgawanyo wetu wa pato la taifa umewezesha watu kuwa na uwezo wa kununua suruali mpya au doti mpya ya kanga au kitenge kila baada ya miezi michache. Na wanatarajia kupata saruji ya kujengea na mabati ya kuezekea nyumba zao kwa kuwa sasa wanaishi katika vijiji vya kudumu. Wanatarajia watoto wao wapate shule na matibabu karibu-karibu; na wanataka maji safi.

Chama kimefanikiwa katika kubadili mawazo na matumaini ya wananchi. Wananchi kwa ujumla, na sisi wote katika Chama na Serikali, sasa tunazungumza juu ya upungufu ikiwa mahitaji hayo hayawezi kutoshelezwa. Hivi sasa, nikisema kuwa matumizi ya kila mwanachi kwa mwaka ya vitu kama sukari, sabuni, nguo, na karibu kila kitu, yameongezeka sana katika kipindi cha miaka ishirini iliyopita, hakuna anayeshtuka. Walio vijana miongoni mwetu

wanaweza hata wasiniamini! Maana tulikuwa tunazungumza juu ya upungufu huu katika mwaka 1977; mwaka 1978 hali ilikuwa ya nafuu kidogo lakini bado tulikuwa tukizungumzia upungufu. Mwaka huu upungufu ni mkubwa zaidi kuliko ilivyokuwa wakati CCM ilipozaliwa, na wala sithubutu kubashiri ni lini hali itaanza kuwa nafuu tena au upungufu utakwisha.

Mafanikio yetu mengine yanayotudai matumizi zaidi ni yale tuliyoyapata katika elimu. Mwaka 1961 kiasi cha watoto nusu milioni walikuwa wanakwenda shule kwa kipindi cha miaka minne. Sasa hivi tunao watoto milioni 3.8 wanaokwenda shule kwa kipindi cha miaka saba. Kwa Tanzania Visiwani watoto wote wanapata elimu ya miaka 11. (*Makofi*) . Kama tukishindwa kupata darasa, pamoja na walimu, vitabu na kadhalika kwa kila mtoto anapofika umri wa miaka saba, basi tunalalamika juu ya upungufu, au hata mkasa katika taratibu zetu za elimu. Na ni haki tulalamike. Kadhalika tusipopata dawa katika zahanati zetu tunalalamika na ni haki tulalamike.

Tatu, tumekuwa na mafanikio makubwa sana katika kujenga viwanda. Tumetumia fedha nyingi katika kujenga viwanda na barabara, na kununua injini za dizeli na mitambo ya umeme. Vitu vyote hivi vinatumia mafuta, ambayo yanaagizwa nchi za nje; vinahitaji pia spea na madawa. Kama tusingalijenga viwanda hivi tusingalihitaji sasa kuagiza mafuta mengi kiasi hicho, na wala tusingalinung'unikia mashimo katika barabara zetu za lami, au upungufu wa spea na madawa katika viwanda vyetu na kadhalika. Nchi isiyokuwa na maendeleo kwa kawaida haina matatizo ya fedha za kigeni, isipokuwa kama viongozi wake ni walafi sana. Tanzania haikupata kuwa na matatizo ya fedha za kigeni kabla ya uhuru. Nchi inayopata mafanikio kiasi fulani katika juhudi zake za kuleta maendeleo italazimika kuwa na upungufu wa fedha za kigeni, hata ukiacha kupanda kwa bei za bidhaa zinazoagizwa nchi za nje kama nilizokwisha kuzieleza.

[…]

Mwaka 1977 nilizungumzia juu ya kuimarisha nidhamu katika viwanda, kupunguza gharama na kuongeza ufanisi katika Serikali na katika mashirika. Hatuwezi kusema kwamba mambo hayo yametekelezwa. Ni kweli kabisa kwamba tunao watanzania wengi sana ambao wanaendelea kufanya kazi kwa juhudi sana na kwa muda mrefu. Lakini ni kweli pia kwamba kuna wengine wengi mno ambao wakati wa kazi hupiga soga tu, au kuondoka mahali pao pa kazi, na hasa siku hizi kwa kisingizio kipya kwamba wanakwenda kutafuta bidhaa muhimu. Na wala isingekuwa kweli kudai kuwa mashirika yetu mengi, au kwa kweli shirika letu lolote, limepunguza sehemu ya wafanyakazi wake wa huduma na wa utawala kulingana na kazi inayofanywa na kutoa mali. Badala yake, hata kama kuna upungufu mkubwa wa malighafi, idadi ya wafanyakazi inabaki ni ile ile; au kama kuna kupunguza wafanyakazi au kuwapa likizo ya muda, wanaohusika ni wafanyakazi wa kawaida tu; lakini mameneja wa uzalishaji, wa Masoko na wa Utangazaji hawaguswi. (*Kicheko*). Gharama zao hudhaniwa kuwa ni za lazima na haziwezi kupunguzwa hata kama hakuna bidhaa yoyote inayotengenezwa, au hakuna chochote cha kutafutia masoko au kutangaza.

[…]

Nililieleza tatizo hili la kujitegemea kwetu katika taarifa yangu ya mwaka 1977. Hakuna mabadiliko makubwa ya utekelezaji wala hakuna mabadiliko yoyote ya mawazo yaliyopatikana tokea wakati ule. Na makosa yetu ya zamani yanatuzamisha zaidi. Hatuwezi kupata spea au mafuta au vifaa vya kutengenezea barabara zetu au kuendeshea viwanda vyetu ambavyo tumekuwa tukivijenga katika kipindi cha miaka 20 iliyopita. Mapinduzi ya fikra hizo lazima yatokee sasa kwa haraka sana na kwa nguvu sana. Mapinduzi hayo yatakuwa magumu zaidi na ya uchungu zaidi, kwa sababu hatukuchukua uamuzi uliokuwa sahihi kwa wakati wake.

Kazi kubwa inayotukabili mbele yetu ni jinsi ya kufanya mapato yetu na matumizi yetu yaanze kulingana. Kazi hii ina sehemu mbili: moja ni ya kuongeza mapato yetu na nyingine ni ya kupunguza matumizi yetu. Sehemu zote mbili ni za lazima. Lakini kwa kuwa

hatuna uwezo wo wote wa kuongeza mapato yetu kwa ghafla, jambo ambalo hatuna budi tulifanye bila kuchelewa ni lile la kupunguza matumizi yetu, ya serikali na ya binafsi. Wakati huo huo hatuna budi tufanye kila linalowezekana kulinda mafanikio yetu ya huko nyuma, hasa katika maeneo ya huduma za umma.

Na silaha yetu kuu ni moja tu, kujitegemea […].

Matokeo ya mpango wa kugawa madaraka mikoani uliofanywa mwaka 1972 yalikuwa kurekebisha kazi za utawala. Lakini mwaka 1975 tuliweka msingi wa Serikali za Vijiji, na sasa hivi serikali za vijiji zilizochaguliwa na wananchi zimeanza kufanya kazi za maana, zikianzishwa na kuendesha shughuli zao wenyewe za maendeleo, lakini zikipata misaada, hasa ya kiufundi, wakati zinapohitaji. Katika mwaka huu uliopita tumepitisha sheria itakayowezesha Halmashauri za Wilaya na Vijiji kujitafutia fedha ili kugharimia shughuli zao, na Wilaya zimepewa mamlaka kamili juu ya wataalam na mameneja wote wanaofanya kazi katika sehemu zao.

[…]

Napenda sasa kueleza kwa ufupi matatizo ya biashara na usambazaji wa bidhaa kwa ujumla.

Baada ya kipindi cha majaribio, Serikali ilianzisha sera mpya ya biashara mnamo mwaka 1980. Kwa sera hiyo bidhaa zote muhimu, na baadhi ya bidhaa nyingine pia, zinauzwa katika maduka ya ushirika au katika maduka yenye ruhusa maalum tu, bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi ya nje na baadhi ya bidhaa zilizotengenezwa humu humu nchini zinakabidhiwa makampuni maalum ya umma kugawa nchini kote kulingana na mpango wa ugawaji ambao huchunguzwa upya mara kwa mara kufuatana na mazingira.

Kwa kuhesabu idadi ya viwanda vilivyokwisha kujengwa na vilivyojengwa sasa na kukaribia kumalizika, mafanikio yetu ya viwanda ni makubwa. Nasema kwa kuhesabu viwanda. Katika Tanzania Bara viwanda vipya 43 vimeanza kufanya kazi tokea

1977, na vingine 28 viko katika hatua za mwisho za ujenzi. Viwanda vingine 5 vimejengwa Tanzania visiwani katika kipindi hiki, na hivi sasa viko katika hatua za kujaribiwa. Kwa mfano, sasa hivi tunacho kiwanda cha madawa, kiwanda cha saruji cha Tanga, kiwanda cha nguo cha Musoma, kiwanda cha ngozi Morogoro, kiwanda cha baiskeli, na karibu sana tutakuwa na kiwanda cha mafuta ya vikonyo cha Unguja, na vyote hivyo hatukuwa navyo miaka mitano iliyopita.

Lakini nimesema hapo mwanzo kwamba makosa yetu ya awali sasa yameanza kutotoa. Tumefanikiwa kujenga viwanda, lakini vile vile tumepata funzo. Karibu viwanda vyetu vyote tulivyovijenga tokea 1967 (maana hatukuwa tumeanza kabla ya hapo) vilijengwa kwa namna ambayo vinategemea sana vifaa vya kuagizwa kutoka nchi za nje. Wakati mwingine bidhaa zinazotengenezwa zinatumika badala ya zile zilikuwa zinaagizwa kutoka nje; wakati mwingine viwanda vimejengwa ili kusindika mazao yetu ya kilimo ama kwa kutosheleza mahitaji yetu ama kufanya yawe na thamani kubwa zaidi kabla ya kuyauza katika nchi za nje. Lakini hakuna kiwanda hata kimoja ambacho kinaweza kufanya kazi kutwa bila kuhesabu mafuta ambayo tunayaagiza pia. Viwanda vingi vikubwa vinategemea utaalamu wa uendeshaji kutoka katika nchi za nje vile vile.

Kuagiza mitambo kwa ajili ya viwanda ni jambo ambalo huwezi kuepuka unapoanza kujenga viwanda. Lakini, ukiacha viwanda vichache sana, pia viwanda vyetu vilijengwa kwa kudhani kwamba mafuta si tatizo, na kwamba spea na vifaa vingine vyote vitaweza wakati wote kuagizwa kutoka katika nchi za nje. Hatukufikiria sana uwezekano wa kutengeneza humu humu nchini vifaa hivi vidogo vidogo, lakini muhimu. Kwa mfano, kwa muda mrefu hatukutilia umuhimu wazo la kuchimba madini ya phosphate ya Minjingu, hata baada ya kiwanda cha mbolea kuanza kufanya kazi. Kwa hiyo tatizo a kutegemea malighafi kutoka nchi za nje halikufikiriwa kwa uzito wake wakati tulipoamua kuanzisha kiwanda kipya. Mipango ya kiwanda inapopendekezwa na shirika la Umma au na Wizara,

hoja inayotolewa ni kwamba itaokoa kiasi fulani cha fedha za kigeni kila mwaka. Mara chache sana inaelezwa, na wala serikali haina tabia ya kuuliza, kiasi gani cha fedha za kigeni kila mwaka.

Lakini ni kweli kwamba, katika hatua yetu ya maendeleo, kwa sehemu kubwa viwanda vyetu kutegemea malighafi za kuagiza kutoka nje si jambo linaloweza kuepukika. Na katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, viwanda vyetu vimekosa kabisa fedha za kigeni, na kwa sababu hiyo uzalishaji mali katika viwanda vyetu umepungua sana. Kwa kipimo cha bei za kudumu, thamani ya bidhaa zetu za viwandani mwaka 1979 ilikuwa shilingi 1,092 milioni. Mwaka 1980 thamani hiyo ilipungua na kufikia shilingi 903 milioni. Mwaka 1981 ilipungua zaidi na kufikia shilingi 648 milioni. Mwaka 1977 viwanda vilileta asilimia 10.4 ya Jumla ya Pato la Taifa; mwaka 1981 vilileta asilimia 5.8 tu ya Pato la Taifa ambalo nalo lilikuwa dogo zaidi.

Hata wastani wa ufanisi wa viwanda vyetu sasa ni kati ya asilimia 30 na 50. Kuna kiwanda kimoja ambacho mwaka jana kilitumia chini ya asilimia 10 ya uwezo wake. Katika hali kama hiyo ikiwa idadi kubwa ya wafanyakazi hawakupewa likizo za lazima, kiasi cha bidhaa kinachotengenezwa na kila mfanyakazi kitapungua sana: mshahara ataendelea kupata ule ule, lakini mali anayotoa kutokana na mshahara huo itakuwa imepungua. Kwa ajili hiyo bidhaa zinazotoka katika viwanda vyetu lazima zitakuwa ghali sana, na hii inatuzidishia tatizo la upandaji wa bei, hata kabla ya mlanguzi na bei yake ya mwendo wa kuruka!

Limekuwako pia ongezeko la viwanda vidogo vidogo, chini ya uongozi wa Shirika la Viwanda Vidogo vidogo (SIDO). Uchunguzi uliofanywa mwaka 1977/78 ulionyesha kwamba vilikuwako viwanda vidogo-vidogo 3,978, na katika hivyo viwanda 1,483 vilikuwa katika sehemu za vijijni. Viwanda hivyo vyote viliajiri wafanyakazi 52,284, na thamani ya bidhaa walizotengeneza ilikuwa shilingi 845.3 milioni kwa kutumia rasilimali ya shilingi 369.7 milioni. Kufikia mwezi Juni, 1981 idadi ya viwanda hivyo vidogo

vidogo iliongezeka kufikia 4,893 ongezeko la viwanda vidogo-vidogo 915.

Jambo moja la maana tunalojifunza kutokana na utafiti huo ni kwamba katika Tanzania, hata kabla ya matatizo ya fedha za kigeni, ufanisi wa kila mtu ni mkubwa zaidi katika kiwanda kidogo kuliko kiwanda kikubwa au cha kati. Kwa mfano, katika mwaka 1976/77 mfanyakazi katika kiwanda kidogo alikuwa akitoa bidhaa zenye wastani wa thamani ya shilingi 16,110 kwa mwaka. Katika viwanda vyetu vikubwa vilikuwa kila mfanyakazi aliweza kutoa bidhaa za thamani ya shilingi 14,172 kwa mwaka, ingawa katika viwanda hivyo kuna zana za gharama kubwa sana, kwa hoja ya kwamba kiwanda cha namna hiyo kitafanya bidhaa kwa gharama ndogo zaidi! Vile vile utoaji mali katika viwanda vidogo umeathirika kwa kiwango kidogo zaidi kuliko ilivyo katika vile viwanda vikubwa. Viwanda vya SIDO vinatumia asilimia 3 tu ya malighafi zote zinazoagizwa kutoka nje zinazotumiwa katika viwanda vyote kwa ujumla. Ni vizuri kulizingatia sana funzo hilo. Kila inapowezekana itafaa viwanda vya SIDO vipatiwe hiyo sehemu ndogo ya fedha za kigeni vinavyohitaji, hata wakati vinapofanya kila juhudi kupunguza mahitaji hayo.

Ni dhahiri kwamba si vitu vyote muhimu vinavyoweza kutengenezwa katika viwanda vidogo. Lakini ni dhahiri pia kwamba, kama tunayo nafasi ya kuchagua utaalam, ni vizuri kuchagua ule tunaouweza na ambao kwa sasa una manufaa makubwa zaidi. Kwa mfano, aina ya bidhaa zinazotengenezwa hivi sasa katika viwanda vyetu vya SIDO inaonyesha uwezekano wa kutosheleza mahitaji yetu mengi kwa kueneza viwanda kama hivyo nchini kote; na kwa kufanya hivyo tutapata faida nyingine ya kupunguza gharama za usafirishaji. Na viwanda vyetu vikubwa lazima vifikirie uwezekano wa sehemu za bidhaa zao kutengenezwa katika viwanda vidogo vinavyohusiana na shughuli zao. Sehemu nyingi za kiwanda cha Baiskeli, kwa mfano, zingeweza kutengenezwa katika viwanda vidogo vidogo. Na wakati huo huo lazima SIDO ijaribu kupunguza gharama zao za uongozi, na

kuongeza msaada wake kwa watoaji mali: hasa msaada wa kutafuta masoko kwa bidhaa hizo.

Tukiitazama sekta ya viwanda kwa jumla , tunaona wazi wazi kwamba hatuwezi kuendelea kama tunavyofanya sasa tukiwa na viwanda vyote vinaendeshwa chini ya uwezo wake kwa sababu ya ukosefu wa fedha za kigeni; wala hatuwezi kuendelea na mpango wetu wa kuongeza viwanda vipya ambao maana yake itakuwa kuongeza zaidi mahitaji ya fedha za kigeni.

Kwanza, lazima tutumie fedha za kigeni zinazotumika katika sekta ya viwanda kwa viwanda vichache, ili viwanda hivyo viweze kufanya kazi kwa kiasi kinachokaribia uwezo wake kamili. Maana yake ni kuamua viwanda gani tuviendeshe, na viwanda gani tuvifunge, angalau kwa muda huu. Itabidi serikali ifanye uamuzi huu bila ya kuchelewa. Kwa sasa tunachunguza uhusiano kati ya kiwanda na kiwanda, na hasa mbinu zitakazotupa nafasi ya kurudia hali ya uzalishaji kamili kwa haraka. Narudia: kufungwa kwa baadhi ya viwanda ni hatua ya muda mfupi ambayo tunalazimika kuichukua kwa sababu ya muda mfupi ambayo tunalazimika kuichukua kwa sababu ya matatizo yetu ya sasa ya uchumi. Bila hiyo tutaendelea kudidimia mpaka viwanda vyote vitafungwa, kwa kukosa fedha za kigeni.

Ni dhahiri basi kwamba itakuwa haina maana kufikiria kuanzisha kiwanda kipya wakati baadhi ya hivi tulivyonavyo tunavifunga. Kwa hiyo mipango ya kuanzisha viwanda vipya itasimamishwa; isipokuwa kama kiwanda kipya kitapunguza uingizaji wa malighafi au kutengeneza vifaa vinavyohitajiwa na viwanda vilivyopo.

Kwa sasa, viwanda vile ambavyo vinatengeneza bidhaa za kuuza nchi za nje lazima visaidie juhudi za sekta ya kilimo katika kutafuta fedha za kigeni. Kama kiwanda fulani kinaleta fedha za kigeni, au kinaweza kuleta fedha za kigeni, kiwanda kama hicho kitapewa nafasi ya kwanza ya kupata fedha za kigeni kinazozihitaji kwa ajili ya kutengeneza bidhaa hizo za kuuza nje. Mfano mzuri ni viwanda vya nguo na saruji.

Hatua zote hizi zinatokana na kutambua uzito wa matatizo yetu ya uchumi. Ni sehemu ya hatua za jitihada ya kujikwamua. Tunalazimika kujitegemea, kwa sababu hatuna njia nyingine. Viwanda vinategemea vifaa vya kuagiwa kutoka nchi za nje zaidi kuliko uwezo wetu wa kupata fedha za kigeni haviwezi kuendelezwa. (*Makofi*).

Jukumu kubwa la sekta ya viwanda katika Tanzania ni lile la kuwapatia wananchi mahitaji yao ya vifaa na bidhaa za kutumia. Lakini viwanda vyetu ni sawa na sekta za nishati na madini na usafirishaji: kwa muda mrefu ujao viwanda vitaendelea kuwa watumiaji wa fedha za kigeni. Ili tuweze kutumia uwezo wa viwanda vyetu kwa ukamilifu tutahitaji kutumia fedha za kigeni kiasi cha shilingi 3,000 milioni kila mwaka; na kiasi kikubwa cha fedha za kigeni ambacho viwanda vimepata kuingiza nchini ni shilingi 561.3 milioni

Kwa sababu hiyo Tanzania inategemea sekta ya kilimo kupata karibu fedha zote za kigeni zinazohitajiwa katika sekta za usafirishaji, huduma, ulinzi, utawala, viwanda na hata kilimo chenyewe.

Kitu chochote inachoweza kuitwa maendeleo hapa Tanzania ni matokeo ya kazi za wakulima wa Tanzania. Wao ndio waliolima mazao yaliyotusaidia kupiga hatua katika elimu, afya, ujenzi wa viwanda, ulinzi na kujenga njia za usafirishaji unaoaminika. Ni kweli kwamba tumepokea misaada mingi kutoka nje kwa ajili ya maendeleo hayo, lakini bila ya kazi za wakulima wa Tanzania tusingeweza kujenga viwanda tulivyovijenga, au kuanzisha elimu ya msingi kwa watoto wote, au huduma za afya vijijini ambazo nchi nyingi za hali yetu zinazionea wivu. Wakulima wanalima chakula chao wenyewe, na ukiacha miaka ya ukame mkubwa, wanalima chakula cha kuwatosha wafanyakazi wa mijini pia. Wamelima na kutupa malighafi ya viwanda vyetu vya nguo n.k na wanaleta zaidi ya asilimia 80 ya fedha zetu zote za kigeni. (*Makofi*).

Lakini ingawa kilimo ndicho kinachotuletea karibu maendeleo yote tunayojivunia, kilimo chenyewe hatukukiendeleza. Na sasa kinashindwa kubeba mzigo tuliokitwisha.

Kama nilivyokwisha kusema, katika miaka ya kawaida wakulima hulima chakula chao wenyewe, na pia chakula cha kuwatosha wakazi wa mijini. Lakini kauli hii haina maana kubwa tukitazama ukubwa wa nchi yenyewe ya Tanzania na idadi ya watu wanaoishi vijijini. Sehemu kubwa sana ya wananchi wa Tanzania ni wakulima, na wanalima mashamba yao wenyewe. Si jambo la ajabu kwa mkulima mwenye shamba la kutosha kulima chakula cha kutosha kwa ajili ya familia yake, kama mvua ni nzuri; na kama mwaka ni wa kawaida atakuwa na ziada kidogo kuwalisha watu wa mijini

Wakati wananchi wa Tanzania wanaoishi mijini walipokuwa wachache sana chakula hiki kilitutosha. Lakini idadi ya wananchi wanaoishi mijini imekuwa ikiongezeka, na kwa kweli idadi ya wananchi wa vijijini wasiolima pia imekuwa ikiongezeka kwa haraka sana, kutokana na kupungua sana kwa vifo vya watoto, na lazima ya watoto waliona zaidi ya umri wa miaka saba kwenda shule. Kilimo chetu hakikuendelea kwa haraka kiasi cha kutosha kulingana na ongezeko hilo la walaji, pamoja na kutosheleza mahitaji ya sekta ya viwanda na huduma za jamii inayoongezeka. Aidha, kilimo chetu hakikuendelea kiasi cha kutupatia ziada ya kuuza nchi za nje ya kutosha kufidia kuanguka kwa bei za mazao yetu makuu.

Kushindwa huku kundeleza kilimo kwa haraka kama zinavyoendelea sehemu nyingine za uchumu zinazotegemea kilimo kimeathiri sana utoaji wa mazao ya biashara. Kwa hiyo tumefikia mahali ambapo, ukiacha mazao ya kahawa na chai ambayo kwa kiasi chake kimebaki pale pale, wingi wa mazao mengine yote makubwa umepungua katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kwa mazao ya pamba, mkonge, korosho na pareto, upungufu huo ulianza toka miaka ya 1960. Kiasi cha karafuu kimeanza kuongezeka tena, baada ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa

kupanda mikarafuu mipya, na kuchukua hatua ya kupambana na maradhi ya mikarafuu mikuukuu.

Takwimu chache zitatusaidia. Pamba iliyonunuliwa na shirika la pamba imepungua kutoka tani 67,100 mwaka 1976/77 kufikia tani 45,000 mwaka uliopita. Mkonge umepungua kutoka tani 133,000 hadi tani 73,000. Korosho zimepungua kutoka tani 97,000 kufikia tani 42,300. Maelezo ya upungufu huu hayawezi kuwa ukame peke yake, na ingawa sababu maalumu zinaweza kutolewa kwa upungufu wa kila zao, ushahidi unaonyesha kwamba lazima maelezo mengine ya jumla yatafutwe kujua kwa nini umekuwako upungufu wa mazao mengi hivyo.

Wala tatizo haliwezi likawa ni upungufu wa mabwana shamba walioajiriwa na serikali. Tatizo hilo lipo kweli, lakini nalo peke yake halitoshi. Wataalamu 5,643 hivi sasa wameajiriwa na wizara ya kilimo kufanya kazi ya kuwasaidia wakulima. Kati ya hao, 1,795 wana stashahada, na 758 wana shahada. Hawa wenye shahada wametumiwa zaidi katika kazi ya elimu ya kilimo, vituo vya utafiti, na katika mashamba makubwa ya umma. Miaka kumi iliyopita tulikuwa na wataalamu 739 tu waliokuwa na stashahada, na 232 walikuwa na shahada kamili katika sekta hii. Kwa hiyo, ingawa tunatilia mkazo sana uhusiano kati ya bei anayopata mkulima na mazao yake anayotoa, uhusiano kati ya idadi ya mabwana-shamba na matunda wanayotoa hauridhishi.

Ni dhahiri kwamba ama mwelekeo wetu wa mafunzo si mzuri ama mabwana-shamba wetu hawafanyi kazi wanayotarajiwa kuifanya. Ni vizuri kujaribu kutafuta kasoro iko wapi na kuiondoa, kuliko kuendelea kuongeza mabwana-shamba , na kuendelea na ubovu ule ule.(*Makofi*)

Hatua nyingine tuliyoichukua imekuwa ya mafanikio zaidi. Vituo vyetu vya utafiti vimefanikiwa kutoa mbegu za pamba, mahindi, mtama, alizeti, na za mazao mengine, zenye kutoa mazao mengi. Nyingi ya mbegu hizi mpya sasa hivi zinatumika, ingawa itachukua muda kabla mbegu hizo hazijapatikana kwa wingi wa kutosha. Vile

vile utafiti wa aina za mikorosho na minazi inayozaa baada ya muda mfupi unaendelea; ndiyo kwanza mbegu hizi zinaanza kuenezwa. Ni jambo la lazima kuweza kupiga hatua kwa haraka kadiri inayowezekana katika jambo hili. Mazao yote haya mawili ya korosho na minazi yanaweza kuwaletea mapato makubwa wakulima wa sehemu za pwani, na pia kutusaidia kupata fedha za kigeni na kutupunguzia tatizo la mafuta ya kupikia

Maendeleo ya mifungo vile vile ni eneo linaloweza kutupa matumaini. Sasa hivi mifugo imepewa wizara ya peke yake, kwa kutambua umuhimu wa mifugo kwa watu wetu na kwa uchumi wa nchi yetu. Katika mwaka uliopita yameonekana maendeleo kidogo katika uuzaji wa ng'ombe na katika kuongezeka kwa ng'ombe bora wa maziwa na wa nyama. Lakini bado ni mapema mno kuwa na hakika kiasi gani cha maendeleo haya kinatokana na juhudi hizi za muda mfupi za kuimarisha mifugo, na kiasi gani mabadiliko ya usimamizi yatatusaidia kusukuma mwelekeo huo katika siku za mbele. Kwa hiyo maendeleo ya mifugo bado yamo katika majaribio.

Lakini narudia. Ukichukua mambo yote kwa jumla mazao yetu ya kilimo hayatoshi kwa mahitaji yetu; uzalishaji wa baadhi ya mazao umeanguka. Lazima sasa tukubali kuwa sababu zilikuwa zinatolewa kwa ajili ya kufikia hali hii ingawa ni za maana, hazitoshi, na kwa hiyo hatua zilizochukuliwa kuzuia upungufu huo kuendelea vile vile hazikutosha.

Wala upungufu huo ulitokea hauwezi kuwa umesababishwa na siasa ya Tanzania ya kuhimiza kilimo cha kijamaa. Kwanza kilimo chenyewe cha kijamaa ni kidogo sana! Tunayo mashamba makubwa ya umma, ambayo kwa sehemu kubwa yamekumbwa na matatizo yale yale ya viwanda ya kutegemea mno vifaa vya kuagizwa kutoka nje. Na matokeo yale yale ya kukosekana kwa zana na spea na dizeli; kwasababu haikuwezekana kuagiza kutoka nchi za nje. Baadhi ya mashamba hayo vile vile yana matatizo ya uendeshaji. Lakini kwa jumla mashamba haya makubwa yanaendeshwa vizuri sana , na ni dhahiri kwamba bila ya mashamba ya Mbarali, Ruvu na Dakawa upungufu wetu wa mchele ungekuwa mkubwa kuliko

ulivyo sasa; na bila ya shamba la Basotu pengine tusingekuwa na ngano hata kidogo.

Lakini kwa sehemu kubwa mazao yetu ya kilimo yanatokana na mkulima mmoja mmoja, au na mshamba ya bega kwa bega vijijini. Vijiji vingi vina mashamba ya ujamaa, lakini kwa kawaida ni madogo. Uongozi unapokuwa mzuri kijijini mshamba hayo hutoa mazao mengi; lakini vinginevyo mchango wa mshamba hayo katika uchumi wa kijiji kwa kawaida ni mdogo mno. Ndoto mbali, kilimo cha Tanzania hakikuathiriwa, wala kusaidiwa na mshamba ya pamoja; maana hayapo! Lakini ni kweli pia kwamba vijiji vichache vyenye mashamba makubwa ya ujamaa ndivyo pia vijiji vinavyoongoza katika maendeleo kwa jumla, pamoja na kilimo. Kwa kutambua ukweli huu Mwongozo wa Chama wa mwaka 1981 unatuhimiza kwa haki kabisa tuongeze idadi na ukubwa wa mashamba ya ujamaa vijijini mwetu.( *Makofi*).

Wala lawama yote ya ubovu wa kilimo chetu haiwezi ikasukumwa kwa mshirika ya Umma, yawe ni mamlaka ya Mazao ya Mashirika mengine. Mashirika haya yana kasoro zake nyingi kubwa. Kwa mfano, gharama zao za uendeshaji ni kubwa mno, kwa sababu watu wengi wazito wanang'ang'ania utawala; mengi yameshikilia mno madaraka katika Makao Makuu. Mameneja waofanya kazi zenyewe hawapewi nafasi za kutosha, na wala hawana vishawishi vya kuongeza uzalishaji ili wapate ziada za kutumia kuongeza mapato, kwa sababu mapato yote yanashikwa na Makao Makuu. Wakati mwingine maofisa wa serikali na wa mashirika wanapinga kugawa madaraka, hata baada ya maagizo kutolewa na serikali.

Mashirika mengi ya mazao hushindwa mara kwa mara kukusanya mazao kwa wakulima, na kuwalipa mara moja; na mara nyingi kuchelewa kupeleka mbolea, dawa na pembejeo nyingine kwa wakulima. Lakini ni vizuri kuzingatia kuwa mara nyingine kushindwa kukusanya mazao na kusambaza pembejeo si kosa la Mashirika ya Mazao; maana bila ya dizeli hakuna lori linaloweza kutembea; na kama pembejeo hazipo haziwezi kusambazwa. Tatizo la Malipo litamalizika wakati Mashirika yatakapotekeleza kwa

ukamilifu uamuzi wa Serikali kutenganisha hesabu za fedha za kununulia mazao na fedha za uendeshaji wa kawaida. Kwa kufanya hivyo tutahakikisha kwamba madeni hayalimbikizwi ambayo yanalipwa na mkulima, lakini bado tutapata matokeo yanayotarajia ya kuhimiza uendeshaji usiokuwa na gharama kubwa. Mgawanyo huu wa hesabu ni muhimu na lazima ufanywe haraka; Wizara zinatarajiwa kuhakikisha kuwa maamuzi ya serikali yanatekelezwa katika Mashirika yaliyo chini yao.

Tukiweza kuyaondoa matatizo yote haya Mashirika ya Mazao na Mashirika mengine, na kutatua matatizo maalum ya mazao fulani, nina hakika kuwa tutaongeza sana mazao yetu. Kwa hiyo hatuna budi tufanye kila jitihada kuyaondoa matatizo hayo. Lakini hatua hizo peke yake hazitatosha. Hazitatosha kwa sababu tatizo letu katika kilimo ni la msingi zaidi; si la uendeshaji tu.

Tangu mwaka 1967 tumekuwa tukisema kuwa ‘’Kilimo ndicho uti wa mgongo wa maendeleo yetu'’ Mwaka 1972 tukatoa mwongozo wa "Siasa ni Kilimo" Mwongozo huu una mambo yote muhimu yanayohitajiwa ili kubadili na kuendeleza kilimo chetu. Hatuachi kuzungumzia umuhimu wa swala hili. Viongozi wote wa chama na Serikali, pamoja na mimi mwenyewe, tumeendelea kuwahimiza wakulima kuongeza juhudi. Tumeweka '’maelezo'’ kwa mazao mbali mbali, kwa kawaida kuanzia katika ngazi ya serikali kuu na kwenda chini. Tumepanga ‘’mazao ya biashara'’ katika sehemu ambazo toka zamani hazina mazao ya kudumu. Tumeanzisha miradi ya mahindi na ya tumbaku kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa. Na kadhalika.

Lakini pamoja na yote hayo nasema leo kwamba tumekipuuza kilimo.

Kwa sababu ya umuhimu wa kilimo katika maendeleo yetu, ungetazamia kwamba kilimo na mahitaji ya wakulima, ndiyo kingekuwa mwanzo na msingi wa mipango yetu yote ya uchumi. Tuliutambua ukweli huu tangu mwaka 1967, tulipokiri katika Azimio la Arusha kuwa: "Maendeleo msingi wake ni wananchi na

juhudi yao na hasa katika KILIMO". Na mwaka 1972, tulizidi kuukiri ukweli huu katika kijitabu chetu, Siasa ni Kilimo, tuliposema: ‘’Kwa miaka ijayo wananchi walio wengi wataendelea kuishi vijijini na kujipatia riziki yao kwa njia ya Kilimo’. Lakini tumekifanya kilimo ama ni kitu cha pembezoni, ama ni shughuli ya kawaida, inayopewa uzito sawa na shughuli nyingine zote, na inayozihudumia sekta nyingine bila kudai kuhudumiwa na sekta hizo. Viwanda vyetu vinatumia mazao ya kilimo; lakini huduma ya viwanda kwa kilimo kwa kawaida si ya moja kwa moja, na tena ni kidogo sana. Mipango yetu ya elimu inategemea mazao ya kilimo lakini kwa wasomi na vyuo vyetu vya kila aina, kilimo hakina heshima: sana heshima yake ni kumpatia msomi diploma au shahada, Lakini baada ya hapo kilimo chenyewe hakimshughulishi. Vijana wetu wengi wanaacha vijiji na kwenda mijini kutafuta kazi za kuajiriwa, kwa sababu wanadharau kilimo na kilimo chenyewe tumekiacha katika hali ya kudharaulika. Katika sera yetu ya biashara, sasa hivi umuhimu wa kwanza, kwa kiasi fulani, unatolewa kwa mahitaji ya wakulima vijijini. Lakini hakuna maduka maalum yanayowapatia wakulima zana zao za kilimo. Na kwa mahitaji yao ya kawida mara nyingi tunayalazimisha maduka ya vijijini kununua bidhaa ambazo hawawezi kuziuza, kuwa ni sharti la kupata hizo bidhaa ambazo mkulima anazihitaji. (*Makofi*)

Tunakipuuza kilimo. Tungekuwa hatupuuzi kilimo kila Wizara moja moja, kila Shirika la umma, na kila kiongozi wa Chama, angekuwa anajishughulisha na mahitaji ya mkulima, na ya moja kwa moja na mengineyo. Tunakitegemea kilimo. Sababu moja ya kutumbukia katika matatizo yetu ya sasa ni kwamba kilimo bila ya kusaidiwa sana hakiwezi kubeba mzigo wa maendeleo yetu. Hata kama Wizara ya Kilimo ikiwa mbovu kiasi gani, matatizo ya kilimo si matatizo ya Wizara moja peke yake.

Kilimo chetu cha asili ndicho kimetulisha na kutupa maendeleo haya tunayojivunia. Lakini ni dhahiri kwamba kilimo hiki cha asili, bila mabadiliko, hakiwezi kutupatia ongezeko la mazao tunalohitaji kwa maendeleo yetu ya kisasa. Miji yetu inapanuka kwa haraka;

watu wetu wanaongezeka kwa kiasi cha 600,000 kwa mwaka; vijiji vyetu vinadai maendeleo ya kisasa. Mzigo unaobebwa na kilimo hiki cha asili sasa ni mzito mno. Wakulima wetu wanafahamu hivyo, na sisi tunafahamu pia. Wao wanataka mabadiliko. Na lazima tufanye mabadiliko katika kilimo chetu. Lakini mabadiliko yenyewe hayana budi yaeleweke kwa wakulima wetu. Na kueleweka huko kunataka vielelezo. Ni vijiji vingapi ambavyo vina mashamba mazuri ya vielelezo? Ni mabwana shamba wangapi vijijini ambao wanalima au kusimamia mashamba kama hayo? Mwanamke yeyote wa Kimasai anayepewa ng'ombe mmoja wa kisasa atagundua mara moja kwamba anapata maziwa mengi zaidi kwa ng'ombe huyu kuliko yale anayoyapata kutoka katika ng'ombe kumi wa kienyeji; na hapo atakuwa tayari kuuza ng'ombe wake kumi ili anunue ng'ombe watatu au wanne wa kisasa. Lakini ukijaribu kumshawishi auze ng'ombe wake bila ya kielelezo hutafaulu. Atakataa; na ana haki ya kukataa.

Mmasai yeyote yule anayefahamu kuwa ili ng'ombe wake aweze kumpatia damu au maziwa ya kutosha ni lazima ahakikishe kuwa ng'ombe huyo anapata majani na maji ya kutosha. Bila kufanya hivyo ng'ombe atakonda, na atashindwa kabisa kutoa damu au maziwa. Lakini sisi tumekuwa tukinyonya tu kutoka katika sekta ya kilimo, bila ya kurudisha rasilimali zinazohitajiwa ili kilimo kiendelee kuwa na afya na kukua kulingana na sekta nyingine za kilimo.

Tumeshindwa kutambua ukweli kwamba kama unataka ardhi ikupe chakula au mazao mengine, basi lazima ardhi yenyewe nayo ilishwe na ishibe.

Tumewashawishi wakulima kutumia mbolea ya chumvi chumvi kwa mazao ya biashara kama pamba na tumbaku, na wakati mwingine kwa kilimo cha mahindi. Kwa kawaida tumewapelekea wakulima mbolea hiyo. Lakini haiko mbolea ya kutosha inayotengenezwa itakayotosheleza kusaidia zaidi ya hapo, kama tunataka mashamba yetu makubwa yanayolimwa kwa vyombo nayo yapate mahitaji yake. Kwa hiyo rutuba ya ardhi yetu inadidimia kwa

haraka sana, hasa sasa ambapo hakuna tena nafasi ya kilimo cha kuhama-hama.

Mbolea ya chumvi chumvi si njia peke yake ya kuilisha ardhi, na kweli haifai kwa aina fulani ya ardhi. Inawezekana kudumisha rutuba kwa kubadilisha mazao, kwa kutumia mboji au ya samadi, na katika sehemu nyingine hata kwa kuchanganya aina ya mazao. Lini sisi, tukiwa viongozi wa Chama, au mabwana shamba wetu, tulipoonyesha mfano wa mambo hayo, kufundisha maana yake na umuhimu wake? Itakuwaje basi mazao yetu yasipungue?

Lazima tuongeze sana matumizi ya mbolea katika mashamba yetu, mbolea inayotoka viwandani na pia samadi na mboji. Katika aina mbili hizi za mbolea ya maana zaidi ni samadi na mbiji. Hii inatokana na viumbe vyenye uhai; na kwa afya ya ardhi inafanya kazi ile ile kama chakula kwa mtu mzima. Mbolea ya viwanda ni tofauti kidogo. Inafanana zaidi na dawa kwa mgonjwa au chumvi ya kukoleza chakula. Lakini kama kawaida tunapofikiria mbolea tumeanza sasa kufikiria hii ya viwandani zaidi kuliko mboji na samadi, ambayo ndiyo hasa inayohitajiwa na ardhi yetu.

Tumepuuza kilimo kwa sababu tumepuuza matumizi ya zana bora na kushindwa kuwapa wakulima au vijiji zana nyingine za kulimia na kusombea mazao badala ya jembe la mkono na migongo na vichwa vya wakulima. Tumezungumza sana juu ya matatizo yote haya mawili. Tumewahubiri wakulima kwamba watumie maarifa ya sasa ya kilimo na tumewaambia kwamba jembe la mkono si zana ya kufaa, na kuwa ni ukatili kuwatumia wanawake kubeba mizigo kama wanyama. Lakini kwa vitendo hatukufanya mengi kuiondoa hali hii.

Na tunapojaribu kuweka sera ya kushughulikia jambo hili mawazo yetu ni ya mwendo wa kuruka! Wengine tunasema kuwa hatuwezi kumudu kununua wala kutumia matrekta mahali popote maana nchi yetu bado iko nyuma mno; kwa kundi hili sera bora ni kuendelea na jembe la mkono.  Wengine tunasema kuwa tukitaka kutokana na jembe la mkono, dawa ni matrekta tu; kwa kundi hili nalo, ama ni

matrekta ama ni jembe la mkono; hakuna chombo cha katikati. Matokeo ya mawazo haya ya mwendo wa kuruka ni kwamba msingi wa kilimo chetu unaendelea kuwa jembe la mkono. Tunajali magari ya anasa zaidi kuliko matrekta na wala hatujishughulishi na zana nyingine za kilimo kati ya jembe la mkono na matrekta. Sasa hivi tunayo matrekta 10,000 nchini. Matrekta haya, hasa kama yote yangekuwa mazima, na tukataka kuyagawa kwa vijiji vyetu kila kimoja kingeweza kupata trekta moja tu. Lakini yote si mazima: yanayoweza kufanya kazi ni 3,000 tu! Tunao mpango wa kuyafufua matrekta haya ili yote yaweze kufanya kazi; lakini kwa tabia yetu ya kupuuza kilimo na mahitaji ya kilimo, inawezekana tena tukapuuza mpango huu, na kuunyima mahitaji yake (*Makofi*).

Tunaweza tukawa na upungufu hata wa hayo majembe ya mkono yenyewe. Mpaka sasa mwaka huu hatuna majembe ya kutosha. Lakini hapa Makao Makuu ya Serikali manung'uniko ni juu ya ukosefu wa karatasi za misalani; na kiongozi wa serikali anaahidi kwamba karatasi hizo au malighafi za kuzitengenezea, itaagizwa kutoka katika nchi za nje! Kwa sasa tunayo ahadi ya kupata chuma ili kiwanda cha zana za kilimo, UFI, kitengeneze majembe; lakini miezi minne kutoka ahadi hiyo kutolewa ilikuwa hakuna kilichofanyika kukileta chuma hicho kutoka India.

Mara moja moja tunazungumza na wananchi vijijini juu ya umuhimu wa mikokoteni na vifaa vingine vya kilimo vya kukokotwa na ng'ombe. Wakulima wengi wanajaribu kuitikia, na hilo ni rahisi kuelewa angalau kwa wale wenye mazoea ya ng'ombe. Basi lazima maplau hayo na vyombo vyake vingine vipatikane wilayani wakati wowote mkulima au kijiji kitakapoamua kununua moja au zaidi; uendeshaji wa zana hizo hauwezi kuwa matatizo kwa sababu seremala au muhunzi wa kijijini anaweza, kwa rahisi, kutengeneza kitu kitakachoharibika. Lakini hata zana hizo hazipatikani. Nimeambiwa kwamba wilaya moja ilipata kuagiza mikokoteni 500 kwa sababu haja ilikuwapo. Miaka miwili baadae mikokoteni hiyo ilikuwa haijafika. Uwezo wa kuitengeneza hauko; na wilaya wala haikujaribu kujitengenezea uwezo huo.

Tumepuuza kilimo kwa sababu tumepuuza umwagiliaji. Mawazo kama haya ya mwendo wa kuruka yanazuia maendeleo ya umwagiliaji maji katika Tanzania. Watu wanadhani kuwa tunalazimika kuchagua tu kati ya miradi mikubwa yakumwagilia maji na kilimo cha mvua. Lakini miradi mikubwa inagharimu fedha nyingi, na inahitaji wahandisi waliofunzwa vizuri kuisimamia. Kwa hiyo tunaweza kuwa na miradi ya namna hiyo michache tu. Kwa sasa hivi maziwa yetu na mito isiyokauka inaweza ikawa meta kumi tu kutoka katika shamba la mahindi yanayonyauka kwa kukosa maji! Hatujishughulishi kuchimba mitaro wala kubeba ndoo za maji kunywesha mimea kutoka katika mto au ziwa lililo karibu kabisa. Nchi kama India inatumia sana maji ya visima kwa umwagiliaji wa mashamba madogo madogo. Lakini sisi tunalalamika tu juu ya ukosefu wa mvua. Na mvua ni maji na maji yako hapo hapo.

Hakuna njia ya mkato ya kutatua tatizo la kilimo cha Tanzania. Lakini kusema kuwa hakuna njia ya mkato maana yake siyo kusema hakuna njia kabisa. Ziko. Mwanzo wake ni kuwasilikiliza wananchi na kuzungumza nao na kuacha kuwahubiri. Lazima tujenge juu ya msingi ulioko, tofali moja moja. Maana yake ni kuondokana, kwa vitendo si kwa maneno, jembe la mkono na kuanza kutumia plau na zana nyingine za kilimo, ni kuondokana na kubeba mizigo kichwani na kutumia mikokoteni. Maana yake ni kurutubisha ardhi, kwa kutumia samadi na mboji na kubadilisha mazao kwa shabaha hiyo, na kuongezea tu mbolea za chumvi-chumvi kama zinapatikana. Maana yake ni kuwa na miradi midogo midigo ya kumwagilia maji kila inapowezekana na miradi mikubwa yenye kutumia vyombo vya kisasa vya kilimo katika mashamba makubwa. Maana yake ni kuwa na mabwana shamba vijijini ambao wako karibu sana na wakulima; ambao wanawaheshimu wakulima; ambao wana vielelezo vya zana na utunzaji bora wa mashamba. Maana yake ni vitendo vya kila mfanyakazi wa serikali na umma, pamoja na wakulima wenyewe, kusaidia kilimo. Maana yake kubwa ni kukubali kutekeleza kwa ukamilifu mwongozo wetu wa 1972 kuhusu SIASA NI KILIMO. (*Makofi*).

Lakini haina maana kuzungumza habari za kilimo kuwa ni msingi wa maisha yetu na maendeleo yetu ikiwa wakati huo huo tunaharibu ardhi yetu na kuitia sumu. Ardhi tunayoitumia kwa kufugia ng'ombe imeharibika, na katika sehemu zinazozunguka baadhi ya vijiji vyetu, mimea yote inaondolewa kwa muda mrefu kabisa katika mwaka, au tunaachia wanyama wale kila jani, au tunakata kila mti unaojitokeza. Matokeo yake ni mmomonyoko wa udongo au unaoletwa na upepo.

Sehemu kubwa ya Tanzania hasa katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Arusha, Singida na Dodoma, sasa zimo katika hatari ya kuwa jangwa. Tayari rutuba yake imedidimia sana. Makorongo mapya yanatokea kwa haraka kuliko tunavyoweza kuzuia mmonyoko wa zamani. Kutoka kwenye vilima ambavyo ndivyo kwanza vitolewe miti yake, udongo wote unaondoka na kusukumiwa baharini, na wakati huo huo vijiji vilivyokuwa vinapata maji yake kutoka katika vilima hivyo sasa hivi vimekauka, havina maji.

Hili ni jambo ambalo hatuwezi kuendelea kilipuuza. Na mimi siamini kuwa idadi kubwa ya wananchi wetu vijijini watashindwa kuelewa tatizo hili kama wakielezwa. Juu ya miti, tayari wanakubali mawazo ya faida ya kuwa na misitu ya vijijini kwa ajili ya kuni, mwaka jana hekta 12,000 za miti zilipandwa katika vijiji vya Tanzania Bara, na wastani wa hekta 600 kwa mwaka zilimepandwa Tanzania visiwani katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Katika mikoa mingine miche ya miti sasa ni kidogo kuliko ile inayotakiwa. Labda ni vizuri kuzingatia kwamba asilimia 90 ya nishati ambayo watanzania wanatumia kwa maendeleo yao ya kila aina inatokana na kuni na makaa ya miti. Asilimia 10 tu ndiyo inayotokana na mafuta tunayoagiza kutoka nje, na umeme unaotokana na mitambo inayosukumwa na maji. Kwa sababu tumekuwa tukikata miti bila ya kupanda, sasa kuni ni tatizo, makaa ni tatizo na mmomonyoko wa udongo unaongezeka kwa haraka. Na upungufu wa kuni na makaa unafanya hata samadi itumiwe kuwa kuni badala ya kupelekwa mashambani kuongeza rutuba. (*Kicheko*)

Wakati Waingereza walipokuwa wanatawala nchi yetu walijaribu kupambana na tatizo la mmomonyoko wa udongo kwa kutunga sheria za kulima matuta na kuzisimamia. Juhudi zao zilishindwa. Sisi wenyewe tumepuuza tu suala zima, kana kwamba lilikuwa linahusiana tu na ukoloni, na halikuwa na maana kwa nchi huru. Na huo ni ujinga. Rutuba yetu ndiyo inayoondoka, na watoto wetu ndio watakaojaribu kulima katika mashamba hayohayo ambayo sisi sasa, kwa kweli tunayachimba kama migodi .Lazima tuanze tena kilimo cha matuta na kinga-maji katika sehemu za miteremko. Baadhi ya mashamba yetu makubwa yameanza kutumia matuta ya kinga-maji lakini si yote.

Nilipotembea mkoa wa Ruvuma mwaka huu niliwapongeza sana wakulima wilaya ya Mbinga kwa utalaamu wao wa kilimo cha ngoro. Wakulima wengi wa Tanzania wanaoishi vilimani au wanaolima katika sehemu za miteremko, wangeweza kujifunza kutoka kwao. Wakulima wa Tanzania visiwani waliwahi kupelekwa Mbinga kwenda kujifunza. Wakulima wetu wa Lushoto wanahitaji sana kujifunza kutoka Mbinga; maana ardhi yao ya vilimani inaharibika kwa haraka sana kwa sababu ya kukata miti yote vilimani na kulima bila matuta wala kinga-maji. Mashamba yetu makubwa, kama yale ya ngano kule Basotu, yanahitaji pia kupanda miti ya kinga kwa upepo. Maana mmomonyoko wa udongo hauletwi na maji tu; huletwa pia na upepo katika maeneo ambayo yameachwa wazi kwa sababu miti yote imekatwa.

Kazi ya kulinda na kuhifadhi ardhi yetu si kazi ya Wizara ya Kilimo au Maliasili peke yake. Ni yetu wote; maana uhai wetu wa leo na kesho unategemea afya ya ardhi yetu.

Narudia. Sasa lazima kabisa tuache kupuza kilimo. Lazima sasa tukipe kilimo kikao cha katikati kabisa katika mipango yetu yote ya maendeleo.(*Makofi*).Tukiacha kilimo kiendelee kuwa pembezoni katika mipango yetu ya maendeleo, basi na Tanzania yenyewe itaendelea kuwa nchi ya pembezoni na watanzania wataendelea kuwa watu wa pembezoni; maana kilimo ndicho msingi wa maendeleo yetu yote.

[…]

Tanzania inaweza kujiondoa katika matatizo yake ya sasa ya uchumi, ikiwa Watanzania watajitegemea. Na watanzania watajitegemea ikiwa kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi, na anaifanya kwa dhati. Narudia: kumbe tusipojitegemea tutamtegemea nani?

Mwanzoni nilikumbusha vita vya silaha tilivyolazimishwa kupigana mwaka 1978. Nilisema pia kwamba sasa hivi tunakabiliwa na vita vya uchumi. Hivi vitachukua muda mrefu zaidi kuliko vile vya silaha. Lakini tunaviweza. Tukiamua kushinda na tukanuia kushinda tutashinda. Kwa sasa hivi karibu kila taifa duniani linakabiliwa na kazi hii inayotukabili sisi: Kurekebisha na Kuimarisha Uchumi wake, ili kujipatia uwezo wa kupiga hatua mpya za maendeleo. Katika jitihada hizi mataifa yatakayofaulu ni yale yenye siasa safi na mipango safi: ni yale yatakayokataa kabisa kuyumbayumba katika msimamo wake wa siasa na mipango yake; na ni yale yatakayotambua kuwa silaha yao kubwa ni Kujitegemea. Tanzania ni lazima tuwe katika kundi la mataifa hayo. Siasa safi tunayo, mipango safi tunayo; Mwongozo safi tunao! Tukiamua kushinda na kunuia kushinda tutashinda. Uwezo wa kushinda tunao! (*Makofi/Vifijo*).

# SURA YA NNE

## Hotuba ya Mjumbe wa Mkoa wa Arusha Katika Mkutano Mkuu wa CCM 1982[5]

***Edward Moringe Sokoine***

*Mara baada ta hotuba ya Mwalimu Nyerere kwenye Mkutano Mkuu wa CCM wa mwaka 1982, Wajumbe mbalimbali walitoa michango yao. Edward Moringe Sokoine, Mbunge wa Monduli, na Mjumbe wa Mkutano Mkuu akiwakilisha Mkoa wa Arusha, alitoa mchango wake. Katika mchango wake Ndugu Sokoine alisisitiza mambo mawili ya msingi: kujenga uwezo wa kuzalisha chakula na kujilisha wenyewe kama taifa, na kuvitazama vijiji kama vitovu vya uzalishaji …..*

Ndugu Mwenyekiti, wa Chama, Ndugu Makamu wa mwenyekiti wa Chama, Ndugu wajumbe wa Mkutano mkuu wa Chama cha Mapinduzi. ….

Ndugu Mwemyekiti, jana ulitoa maelekezo kwamba usingependa kupongezwa au kupewa shukrani kwa kazi kubwa na maelekezo ya hekima uliyatoa hapo juzi kwa Taifa letu. Lakini kwa kweli nashindwa namna ya kuanza kusema bila ya kusema kidogo. Kwanza kukupongeza na pili kutoa shukrani kubwa sana kwa niaba ya Wanachama wenzangu tuliopo katika Mkutano Mkuu na hata wale ambao hawapo na ambao ndio waliotutumia tuje hapa kwa niaba yao. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti, jana msemaji kutoka Mkoa wa Kilimanjaro Ndugu Kimario alisema kwamba hotuba yako ilikuwa ya kihistoria kwa mambo mawili. Kwanza kwa urefu wake muda uliouchukua

[5] CCM 1987 Majadiliano ya Mkutano Mkuu wa Kawaida Oktoba, 1982: Taarifa Rasmi; Dodoma, Idara ya Uenezi na Ushirikishaji Umma. Uk. 353-371.

naambiwa dakika 240 na vile vile kwa kiwango chake cha kwenda ndani katika uzito wa fikra zake.

Lakini Ndugu Mwenyekiti, ningependa nitofautiane kidogo na rafiki yangu Kimario kwamba si kweli kwamba hotuba yako hiyo ndiyo imekuwa ya kwanza labda kwa urefu wa muda uliochukua. Lakini kwa kina sikubali. Ndugu Mwenyekiti kwa kawaida kabisa tangu uanze kuwa Kiongozi wa Taifa letu na hata kabla ukiwa mwanafunzi tukisoma maandiko yako mbali mbali daima mawazo yako yamekuwa ya kina kirefu na jana nilikuwa natafuta neno la Kiswahili sikulipata ya kueleza nini zaidi ya kina isipokuwa kusema hotuba zako nyingi kwa kweli huwa hazina kikomo cha kina. (*Makofi*/*Kicheko*).

Ndugu mwenyekiti, ingawa Waswahili wanasema hakuna refu lisilo na mwisho lakini mawazo huwa hayapimiki sana kama unavyoweza kupima mwendo wa safari. Mawazo yanaweza yakaanza na yakaenda mbali mno kwa Kiingereza wanasema ndani ya *silence space* na huoni mwisho wake. Na mimi nasema hotuba zako nyingi zimekuwa za tabia hiyo.

Kwa hivyo, Ndugu Mwenyekiti, ningependa nikupongeze sana kwa hotuba hiyo ndefu na ambayo imejaa maelezo mengi ya hekima ambayo yanaweza yakalisaidia Taifa letu kujiondoa katika matatizo magumu ya kiuchumi tuliyonayo hivi leo.

Ndugu Mwenyekiti, pili ningependa nikushukuru zaidi si kwa kina tu cha mawazo na maelekezo uliyotoa kwa Taifa letu lakini zaidi kwa kuwaeleza Watanzania ujasiri wako wa kusema ukweli kuwaeleza Watanzania na dunia nzima, chanzo cha matatizo yetu yote ya uchumi tuliyonayo jambo ambalo ni Viongozi wachache mno katika dunia ya tatu na hasa hizo nchi za dunia ya kwanza walioendelea wanaweza wakawa na ujasiri wa kuwaambia watu wao ukweli bila ya kuwaficha. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti, mara nyingi Viongozi na hasa wa dunia hiyo ya kwanza huyasema mengine na mengine huachwa mpaka yafichuliwe na kashfa ya namna fulani. Kwa hivyo kwa suala hili la

kutuambia ukweli mimi ningependa nikushukuru sana na kusema kwamba kama Watanzinia walikuwa hawajui chanzo cha matatizo yetu mimi nafikiri hotuba yako itakuwa imewazindua waelewe matatizo yatokanayo na nje ya uwezo wa Taifa letu, matatizo yanayotokana na hatua mbali mbali ya maendeleo tuliyopiga katika Taifa letu na vile vile matatizo yanayotokana na udhaifu wa uongozi wetu katika Chama na vile vile katika Serikali. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti wasemaji wengi jana walisema na hasa wasemaji wa Mkoa wa Kijeshi kwamba hotuba yako ni tangazo la vita ya kiuchumi. Na hivyo ndivyo tungelienda Watanzania wote watafsiri hotuba hii. Nasema hivyo Ndugu Mwenyekiti kwa sababu sipendi nijitie kama Waingereza wanavyosema ni *prophet of doom* au ni Nabii wa kutabiri hali mbaya inayokuja. Lakini ukweli ulivyo kwa nchi changa za dunia ya tatu mbele yetu kuna giza kubwa sana. Kwa mara ya kwanza Ndugu Mwenyekiti katika historia ya uhuru wetu mwaka huu tulilazimika kuchukua hatua ambazo hatujawahi kuzichukua tangu tupate uhuru. Tulisimamisha miradi ya maendeleo zaidi 940. Tulifunga viwanda vingi, tumepunguza miradi ya maendeleo yaani miradi mipya na vile vile uwezo wetu wa kujilisha na kulisha viwanda vyetu umepungua kwa kiwango kikubwa. Jambo ambalo hatukuthubutu kilifanya katika hatua ya sasa ni kuwapunguza wafanyakazi kwa maelfu na hiyo ni kwa sababu ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea tunayofuata katika Taifa letu.

Ndugu Mwenyekiti, hali hii ngumu ya uchumi tuliyonayo juzi ukitoa hotuba yako ulieleza kihistoria kwamba hata hizo nchi zilizoendelea hazijawahi kuwa na matatizo kama hayo pengine kwa kipindi cha miaka 40 au 50 iliyopita. Lakini si Watanzania wote waliokuwa wamegutuka wakati wa Bajeti kwamba Taifa letu limefikia katika hatua ngumu ya kiuchumi na ambayo lazima tufikirie upya namna ya kujiondoa katika hali hiyo.

Ndugu Mwenyekiti, kama alivyosema ndugu Jamal sasa hivi Watanzania wote walibahatika mno kukupata wewe kama Kiongozi wao. Na bahati hiyo waliyoipata kwa bahati mbaya mara nyingi

inafanya wafikiri kwamba Kiongozi wao kila anapopenda ana uwezo wa kufanya miujiza ya namna fulani. Kuna hadithi Ndugu Mwenyekiti sijui katika Rabianaisi walikuwa wanasema kuna mtu mmoja masikini aliyopewa ataje mahitaji yake matatu tu lakini asitumie zaidi na alizitumia mpaka zimekwisha. Sasa watanzania nao mara nyingi wanafikiri tunapokuwa na tatizo Mwalimu bado ana uwezo wa kutumia uwezo wake huo wa jambo hili likatendeka. Kama ingekuwa rahisi hivyo Ndugu Mwenyekiti nina hakika Watanzania wasingekuwa na tatizo lolote la kiuchumi wala kijamii hivi sasa. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti matumaini yangu ni kwamba hotuba yako imewazindua Wajumbe wa kikao hiki na kwa kupitia kwao lazima uwazindue vile vile Watanzania waliokuleta katika kikao hiki. Ndugu Mwenyekiti hotuba yako lazima ituelekeze katika kujua kwamba majibu ya matatizo yetu ya kiuchumi lazima yatokane ndani ya nchi yetu wenyewe.

Ndugu Mwenyekiti, nchi za dunia ya tatu hivi sasa kwa maoni yangu naona tunazo njia tatu za kuweza kupambana na hali hii tuliyonayo. Tatu nzuri moja mbaya. Kwanza nchi zetu za dunia ya tatu njia yetu ya kwanza *action* tulizonazo ni kuchagua kabisa kuwa Wanamapinduzi na kusimamia kwa miguu yetu wenyewe. Na Ndugu Mwenyekiti nafikiri silaha hiyo kwa upande wa Watanzania tunayo kwa kupitia Siasa yetu ya Ujamaa na kujitegemea.

Ndugu Mwenyekiti, pili nchi za dunia ya tatu zina uwezo wa kupunguza tatizo hili la kiuchumi kwa kushirikiana wao kwa wao wenyewe *Regional Cooperation*. Suala hili ambalo tunafanya na wenzetu wa Uganda, Rwanda, Burundi na wenzetu kusini ya Afrika. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti, la tatu lilipo la kuweza kupunguza matatizo yetu ya kiuchumi ni kushirikiana baina ya yetu na nchi zingine za kirafiki hasa nje ya Afrika *by Natural Relation*. Nasema hivyo ndugu mwenyekiti kwa sababu ingawa mara nyingi tumehutubia vikao vingi vya Kimataifa na kusema kwamba tuwe na ushirikiano

wa nchi zisizofungamana na upande wowote *The Third Region of the poor* lakini suala hili bado halijazaa matunda yanayotakiwa.

Kwa hiyo, kubwa katika hayo yote ninaloliona ni lile la mwanzo la kila nchi kuamua itafanya nini ili iweze kusimama kwa miguuu yake yenyewe. Lakini vile vile lipo au kina *Abortion* [*soma 'option'*] ya nne na hili ni baya zaidi nalo ni kulazimika kwa nchi kujiuza kitumwa au kuuza uhuru wa nchi yake kusudi iweze kupata misaada kwa nchi zinazoendelea. Sijui kama nitaeleweka vizuri Ndugu Mwenyekiti lakini mpaka sasa nchi zilizo nyingi za dunia ya tatu hasa katika Afrika tulio na matatizo ya kiuchumi tuna uhuru wa bendera hatuna uhuru wa kiuchumi na ndio huu tunaopigania. Lakini baadhi yetu ni lazima niwataje wameanza kuuza uhuru wa nchi zao, kutao maeneo ya Kijeshi kwa nchi zilizoendelea ili mradi wawe na hakika wanaendelea kupata misaada. Hilo ndilo nasema ni suala la kuuza uhuru wa nchi. (*Makofi*).

Maana huko mwanzo tulishirikiana lakini lakini wakishajiingiza kiasi hicho, sijui kama kushirikiana kwetu kutawezekana tena au ndio ile *scramble* ya pili uliyoisema.

Ndugu Mwenyekiti, nasema hivyo, kwa sababu sasa hivi chanzo cha matatizo ya nchi changa ni biashara hii inayopendelea nchi zilizoendelea dhidi ya nchi zinazozalisha. Sasa hivi tumeweka, tumekuwa na mshikamano wa nchi zote zinazoendelea na kuzungumza katika vikao vya kimataifa, pamoja na Baraza la Umoja wa Mataifa lenyewe kudai kubadilishwa kwa mfumo wa uchumi duniani.

Lakini Ndugu Mwenyekiti, ingefaa Watanzania tusijidanganye. Kwamba mapambano haya ya kubadili mfumo wa dunia ni suala linaloweza kubadilishwa kwa haraka na upesi na kwa hivyo, kurekebisha hali ya uchumi wa nchi zilivyo. Suala hili Ndugu Mwenyekiti, linaweza kuchukua miaka 50 hata miaka 100 na lisitekelezwe.

Ndugu Mwenyekiti, ni vizuri tuelewe kwamba hakuna nchi iliyoendelea itakayokubali kupunguza mkate na siagi ya watu wake kwa ajili ya kuwalisha watu maskini wa Afrika.

Ndugu Mwenyekiti, sasa hivi dunia tuliyonayo haina upungufu wa chakula, ukiachilia Bara la Afrika. Asia kidogo wameendelea karibu wanajitosheleza, Latin Amerika nao ni hivyo hivyo. Tatizo kubwa la chakula lipo katika Bara la Afrika. Lakini ukichukua dunia yote nzima kwa ujumla, hakuna upungufu wa chakula. Isipokuwa utu haupo.

Ndugu Mwenyekiti, chakula ni kingi mno. Kinatumika kulisha wanyama kama vile kulisha ng'ombe kulisha nguruwe, kulisha kuku na baya zaidi hata kulisha mbwa, kuliko kupeleka kwenye nchi zenye dhiki kweli ya chakula. Sasa hivi wenzetu wa nchi za Sahel wana matatizo ya chakula. Lakini chakula kinapelekwa na kinapopelekwa jambo hili hutangazwa kwa kiwango cha kutia aibu.

Kwa hiyo, hata ile heshima ya kutoa kile chakula, kule kutangazwa nchi kinakopelekwa chakula kunaondoa heshima na utu wa kupokea chakula kile. Ndugu Mwenyekiti, dunia ya leo silaha zinatengenezwa na *nuclear* kwa gharama kubwa na kwa ma-bilioni ya fedha ambayo yangeweza kuondoa matatizo ya dunia yote nzima. Silaha hizo zinaweza zikaharibu dunia yetu ya leo, sayari yetu hii ya sasa pengine mara elfu moja na zaidi. Lakini zingali zinaendelea kutengenezwa

Na sijui ni za kuangamiza nini zaidi baada ya kuwa na uwezo wa kuharibu sayari tuliyonayo hivi leo zaidi ya mara mia moja. Lakini hizo ndizo tabia na fikra za binadam.

Ndugu Mwenyekiti, sasa hivi nisije nikaeleweka vibaya, zipo nchi ambazo zimeitikia mapendekezo ya Umoja wa Mataifa wa kutoa msaada wa kila mwaka ili kusaidia maendeleo ya nchi changa. Nchi hizo, Ndugu Mwenyekiti sio nyingi sana. Lakini wale wachache wanaotusaidia na hasa wenzetu wa Scandinavia, hao Ma-Kanada waliotajwa sasa hivi na wengine wote na ambao wameshafikia

kiwango kile cha asilimia moja ya pato la taifa, hatuna budi tuwashukuru. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti, huko mbele, kama nilivyoanza kusema hapo mwanzo. Matazamio yetu huko mbele kwa nchi za dunia ya tatu ni kwamba tunaweza tukaingia katika hatua kama tatu au nne. Lile la kwanza nililosema, wana-amua kuchukua njia ya kweli ya kusimama kwa miguu yao wenyewe wataweza kujivusha hivyo mpaka waamue kwa dhati kabisa kwamba jukumu ni lao na msaada watakaopata utakuwa ni nyongeza ya juhudi zao. Naamini Watanzania wataamua kufuata njia hiyo. (*Makofi*).

Pili, Ndugu Mwenyekiti, nchi zingine za dunia ya tatu zitalazimika kusimama pale pale, zilipo. Hawataweza kwenda mbele, kurudi nyuma inawezekana.

Ndugu Mwenyekiti, kundi la tatu wenzetu ambao wanaweza wakawa katika hatari ya kurudi kabisa kule tulikotoka kusikokuwa na maendeleo. Na baya ni wale niliosema wanaweza wakathubutu hata kuuza uhuru wa nchi zao ili waendelee kuishi lakini ni kuishi kitumwa.

Sasa, Ndugu Mwenyekiti, ningependa niseme hali yetu kama ulivyoeleza jana ni hali ngumu. Lakini si hali ya kukatisha tamaa. Ndugu Mwenyekiti kwa nini nasema hivyo. Nasema hali yetu ya uchumi ngumu. Kwa sababu kila Mtanzania kuanzia ngazi ya taifa hadi huko vijijini amekwisha elewa matatizo haya ya kiuchumi. Lakini kwa nini nasema si matatizo ya kutukatisha tamaa. Nasema hivyo, kwa sababu Ndugu Mwenyekiti, nina imani na kukubali kabisa, kwamba Watanzania wote au waliowengi sehemu kubwa ya Watanzania wanakubali siasa ya ujamaa na kujitegemea kwamba ndio njia yao ya ukombozi. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti, ujamaa ndio mwelekeo wa dunia tulionao hivi leo.

Ndugu Mwenyekiti, kwa hivyo wale wanaoamua kuogelea dhidi ya maji yanayofurika shauri yao. Sisi lazima tukubali kwenda

mwelekeo wa dunia unavyokwenda na unakwenda katika ujamaa. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti, jambo la pili linalonipa imani ya kusema matatizo yetu si ya kukatisha tamaa ni kwamba Watanzania wanayatambua matatizo yao na kwamba wapo tayari kupambana nayo wao wenyewe na kuondoa matatizo hayo. Na Ndugu Mwenyekiti, ukiwasikiliza wasemaji wote waliosema tangu tuanze kusema juzi utaona kwamba asilimia 99.99 karibu wote wanajua kwamba jibu la matatizo yetu yapo ndani ya mikono yetu, kuanzia katika familia, katika kata, tarafa, wilaya, mkoa hadi ngazi ya taifa. Kwa hiyo, hilo linanipa imani ya kuamini kwamba hili si jambo la kutukatisha tamaa.

Tatu, Ndugu Mwenyekiti, Watanzania walio wengi na hasa katika kikao hiki wengi walilalamika na malalamiko yalianzia kwako mwenyewe, kuhusu utekelezaji mbovu wa mipango na maamuzi yetu. Ndugu Mwenyekiti utekelezaji mbovu unategemea uongozi. Uongozi katika Chama, uongozi katika serikali na vyombo vyake. Na baadhi ya wajumbe, jana walikuwa wanakuomba Mwenyekiti uwe mkali. Lakini nitatoa jibu hapo baadae.

Jambo la nne, Ndugu Mwenyekiti, Watanzania wote kwa jumla wanachukizwa na wizi wa mali ya umma na ubadhilifu katika serikali na katika mashirika yake. Na hapo walilalamika na matumaini yangu ni kwamba wenzetu wa sheria walikuwa wakisilikiza juu ya suala hili sana. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti, jambo lingine linalonifanya niamini kwamba matatizo yetu si ya kutukatisha tamaa ni kuwa Watanzania wote hivi sasa wamechukizwa na uzururaji wa maelfu ya watu wasio na kazi. Wanao kula na kuvaa na kunywa lakini bila ya kuvuja jasho.(*Makofi/Vigelegele*).

Kadhalika, Ndugu Mwenyekiti, Watanzania wamechukizwa na wizi, ujambazi wa kutumia silaha na tamaa ya mali iliyojaa miongoni mwa vijana wetu lakini bila ya kutaka kufanya kazi.

Ndugu Mwenyekiti, jana msemaji mmoja alisema ukianza kutambua matatizo yako ni nusu ya kuyatanzua matatizo yenyewe. Na mimi ninaamini Watanzania wameyachambua wao, wanayajua na kwa hivyo vile vile watajua tiba yake itakuwa ni nini.

Ndugu Mwenyekiti, kuhusu tatizo la uongozi ambalo jana baadhi ya wajumbe wanasema Mwenyekiti hofu yao nahisi alikuwa msemaji kutoka Tabora. Anasema hofu yake, Mwenyekiti ametufungulia mlango lakini akahisi utafungwa tena. Samahani, yule msemaji ni wa Singida, msemaji yule hodari.( *Kicheko*).

Ndugu Mwenyekiti, nasema kama ni kiongozi wetu kichama, kiserikali tumekupa madaraka ya kikatiba lakini huwezi kafanya kila kazi kwa niaba ya kila mtanzania. Na ndio sababu tuko hapa, tuna jukumu lililotuleta.

Ndugu Mwenyekiti, Kikao hiki ni cha kihistoria katika Chama chetu na hasa katika kufafanua matatizo ya kiuchumi tuliyonayo. Na ndio sababu umetolewa Mwongozo mpya wa Chama na vile vile Katiba mpya ya Chama, na vile vile mapendekezo mapya ya Katiba ya Jamuhuri.

Ndugu Mwenyekiti, sasa hivi kichama tumeishafanya uchaguzi. Wanachama wameshatekeleza jukumu lao la kuwachagua viongozi wao watakaowashughulikia watakaoongoza maendeleo yao kwa miaka mingine mitano ijayo kuanzia shina, tawi, wilaya, na mkoa. Kulikobakia ni suala hili la Uchaguzi wa ngazi au Taifa ambalo umelisema kweli. Sasa hivi baadhi ya wajumbe hawapati usingizi vizuri. Lakini ninalopenda kusema Ndugu Mwenyekiti, ni kwamba Kikao hiki, leo kina nafasi moja tuu inayoweza kutumiwa katika miaka mitano ijayo. Katika kuwachagulia, kujichagulia au kuwachagua viongozi wa kitaifa ambao watalingana na matarajio na matatizo yanayohusu nchi yetu.(*Makofi*/ *Vigelegele*).

Ndugu Mwenyekiti, hofu yangu ni kama kikao hiki Kitukufu cha Chama hakitatumia bara bara uwezo wake wa Kikatiba Kichama kuwachagua viongozi wa kitaifa wanaoweza kusaidia kulivusha taifa letu katika matatizo tuliyonayo. Wasipofanya hivi, lawama

itarudi kwako tena kesho. Lakini kwa nini tukulaumu wakati uwezo upo mikononi mwa kila mmoja wetu. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti, unayo madaraka uliyopewa Kichama na Kiserikali ambayo unaweza kulaumiwa nayo lakini nasi lazima tukubali kama wajumbe wawakilishi tuliotumwa na wanachama wenzetu huko wilayani na mikoani kutoka vijijni, wilaya, mkoa kuja katika kikao hiki kutekeleza wajibu wetu katika uchaguzi wa viongozi.

Ndugu Mwenyekiti, hotuba yako kama kawaida imejaa mawazo mengi ya hekima ambayo kama yangezingatiwa, yatalivusha taifa letu katika matatizo haya ya kiuchumi tuliyonayo hivi leo.

Kwa hivyo, Ndugu Mwenyekiti, jambo ambalo ningependa niseme ni kutoa wito wa wajumbe wenzangu wa mkutano mkuu huu wa chama kwamba katika uchaguzi ambao utafuata siku chache kuanzia sasa; sijui lini labda jumatatu au labda jumanne, lakini ningeomba tuzingatie misingi ifuatayo kama tunataka kuliondoa taifa letu katika matatizo tuliyonayo.

Msingi wa kwanza, katika uchaguzi wetu, Ndugu Mwenyekiti ningesema tuongozwe na umoja wa kitaifa katika kuwachagua viongozi tutakaowachagua wa ngazi ya taifa. (*Makofi*). Tunaomba wajumbe wakatae suala la ukabila. (*Kicheko*). Msingi wa umoja ndio uliotupa nguvu na iliyoifikisha taifa letu kuanzia wakati wa kupigania uhuru hadi hivi sasa. (*Makofi*).

Mimi, Ndugu Mwenyekiti, sipendi kujisifu lakini sikuzunguka kutafuta kura au kujaribu kuomba kura kwa wapiganaji. Lakini tetesi zilizopo, Ndugu Mwenyekiti, ni kwamba uchaguzi huu kama ulivyokuwa ule wa Bunge wa mwaka 1980 ambao fedha kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu zilitumika na mbinu nyingine mbalimbali za kusema msimamo wetu ni huu na huu na zinatuharibia. (*Makofi*).

Ndugu Mwenyekiti, jambo ambalo ningeomba tujihadhari na suala la ukabila, tuzingatie umoja wa kitaifa na mwenye sifa tumchague. Ndio wataotuvusha katika matatizo. (*Makofi*)

Jambo la pii, Ndugu mwenyekiti, ambalo ningeomba lituongoze vile vile katika kuwachagua viongozi wetu wa chama na taifa ni suala la kulinda uhuru wa taifa letu. Lazima tuwakatae vibaraka ambao wanaweza wakatumiwa na mataifa ya nje au hata vibaraka wa ndani kwa lengo la kubadili siasa yetu au kuidhoofisha. (*Makofi*)

Msingi wa tatu, Ndugu Mwenyekiti, ambao ningependa kushauri utuongoze katika kuwachagua viongozi wetu ni kuzingatia suala la ujamaa wa kujitegemea. Tumekwishajua wazi wazi kwamba ujamaa na kujitegemea ndio msingi wa Uhuru wetu, na ndio msingi wa maendeleo yetu. Na jana napenda nirejee mazungumzo ya msemaji wa Singida aliyesema vizuri sana kwamba ingawa maadui wa siasa yetu husema kwamba Ujamaa ndio chanzo cha matatizo ya kiuchumi Tanzania. Watuambie nani katika Tanzania amenyang'anywa ardhi yake, mifugo yake na kadhalika.

Kwa hivyo, Ndugu Mwenyekiti, narudia kusema kuwachague viongozi ambao wanatuelekeza katika lengo la ujamaa wa kujitegemea ili tuweze kulivusha taifa letu katika magumu ya kiuchumi tuliyonayo hivi leo.(*Makofi*).

Jambo la nne Ndugu mwenyekiti, ni suala la uzalendo. Suala la uzalendo nalo ni la msingi mkubwa katika kila taifa. Kama tusingekuwa na uzalendo wa kutosha, tusingeweza kupigana na wavamizi waliovamia nchi yetu mwezi Oktoba, 1978. Lakini, Ndugu Mwenyekiti , wewe wajua na labda kwa faida ya wajumbe, walijitokeza vijana kwa maelfu na malaki waliotaka kwenda mstari wa mbele; ila taifa tulikuwa hatuna uwezo wa kuwapeleka wote. (*Makofi*).

Na kwa hivyo tuliweza kupeleka pengine nusu au theluthi ya majeshi yetu tu. Lakini majeshi yaliyobaki nyuma yangeweza kupigana katika medani nyingine.

Kwa hivyo, suala la uzalendo, ndugu mwenyekiti, lazima tulitumie katika kuwafikiria viongozi wenye msimamo wanaotaka kuchaguliwa kitaifa ili waweze kulisaidia taifa letu katika kipindi hiki kigumu.(*Makofi*). Na hasa nasema suala hili, zaidi kwa suala la kiuchumi, lazima tukatae ubadhilifu, lazima tukatae watu wanaoangamiza Mashirika yetu ya umma, na wenzetu wa sheria watusaidie kulinda maslahi ya umma. Katika vikao vingi vya chama vilivyokwisha dai kuanzia Tabora, Arusha mpaka hapa, ningependa kuona siku moja tunasimama na kusema leo tuna sheria inayoweza kulinda maslahi ya mashirika yetu ya umma. (*Makofi*)

Ndugu mwenyekiti, jambo la tano ambalo ningependa nilitaje, hili nalo ni la msingi vile vile ningewaomba wajumbe tusitupilie mila zetu nzuri mbali. Ndugu mwenyekiti, vijana wetu sasa hivi wameanza kusemwa sana, hawa wanaomaliza kusoma kwamba hawapendi kufanya kazi vijijini, hukimbilia mijini na wengine wanajulikana wamejitajirisha kwa haraka sana. Lakini wazazi tumeacha tabia ya malezi mema ya kijadi ya kuwalea watoto wetu.

Vijana leo wengi wana mali zaidi kuliko wazee waliofanya kazi miaka 30 au 40. (*Makofi*). Lakini wanaitaka ndio iwaulize mali hiyo mliipata wapi.Hivi kwa nini mzazi asimuulize mwanae mali hii umeipata wapi. (*Makofi/Kicheko*).

Ndugu mwenyekiti, uliwahi kuwaambia akina-mama, nahisi katika Ukumbi huu huu, siku hiyo sikuwepo, sijui nilikuwa wapi lakini nilikuwa nasikiliza kwamba mbona hamuwaulizi mabwana zenu hizi saa za dhahabu mnazoletewa zinatoka wapi. Hiyo ni sehemu ya mila zetu.

Lakini sasa hivi, Ndugu Mwenyekiti, utamaduni wetu na mila zetu umeingiliwa mno na mila na tabia za kigeni za kuwa na tamaa za vitu, hasa visivyosaidia katika maisha. Pengine sio vizuri sana mtu kusema siri zote, lakini juzi wakati wa sabasaba, wewe ulisema ulianza kufagia fagia nyumbani kwako. Na mimi ningependa niseme mwanangu wa kwanza si mtu mzuri sana. Na sasa hivi

nimeomba msaada wa nchi za kirafiki za kijamaa zinisaidie kurekebisha tabia hiyo. (*Makofi*).

Ndugu mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tungali tuna tatizo kubwa na hasa la viongozi wa kitaifa la kutoweza kuwalea watoto wao kutokana na muda mchache walionao wa kuwa majumbani. Tatizo hili taifa bado halikutambua na baadaye watoto wa viongozi wetu wanaweza wakakutwa kwamba wote hawafai; na taifa zima litafute jibu juu ya suala hili.(*Makofi/Kicheko*).

Ndugu mwenyekiti elimu yetu ya jadi ni mzazi kufuatana na mwanae kwenda shambani, machungani, kuvua, kufua chuma-ndio elimu yetu ya jadi; elimu na kazi. Suala hilo hilo lazima tulirudie kwa kutumia shule zetu za msingi na hata za juu katika kushirikisha kazi zao na kazi za vijijini. Elimu na kazi vijijini bila ya kuwatenga na wazazi wao wanaweza wakawa na maeneo yao lakini wakafundishana katika kazi. Na vijana kwa kutumia maarifa yao ya kisasa wanayopata shuleni, watatoa mafunzo ambayo mabwana shamba ingebidi waende kutoa pale kijijini.

Ndugu Mwenyekiti, hayo yalikuwa yanahusu suala hili la uchaguzi, ni misingi gani itusaidie na ningependa kuendelea na suala lingine ambalo ningependa nitoe mchango wangu kidogo. Hili ni suala ulilolisema katika hotuba yako juu ya suala la kutolingana mapato na matumizi ya serikali yetu.

Ndugu mwenyekiti, serikali na mashirika sasa hivi kama tulivyosema, yamekuwa ni mzigo mkubwa sana kwa mkulima wa Tanzania. Na sasa hivi kama tusingependa kuelezana ukweli, hali ya upungufu wa chakula katika Tanzania, huwa sio mbaya kama inavyotangazwa ama kama tunavyosema. Wakulima wetu walio wengi kwa sababu ama ya kutoridhika na bei au kwa sababu nyingine wameanza kuficha vyakula na badala ya kuuza kwa Mashirika ya Umma, wanauza wenyewe kidogo kidogo kwa madebe yaliyogongwa mpaka msimu wote mzima; wanalangua.

Ndugu Mwenyekiti, lakini nasema Chama na Serikali ina uwezo wa kumuondoa mkulima wetu kutoka pale kwa kutazama kwa hali

halisi kabisa gharama zake za uzalishaji wa mazao yake. (*Makofi*). Kwa sababu mwenye kutoa bei ya mazao kwa sasa ni serikali lakini serikali hupata kwanza taarifa kutoka kwa Mashirika au Mamlaka yanayohusika na zao hilo. Sasa hapo pana mgongano wa maslahi. Mamlaka au Shirika litapenda lipate faida. Wamejijengea maofisi makubwa, wameongeza idadi kubwa ya wafanyakazi na mambo mengine mbalimbali na kwa hivyo kuumia kwa mkulima. (*Makofi*). Kwa bahati njema, Ndugu Mwenyekiti, sasa hivi kwa maelekezo ya Chama, serikali imekwisha agizwa irejeshe vyama vya Ushirika. Matumaini yetu ni kwamba Vyama vya Ushirika vitafanya kazi ya kumuhudumia mkulima na vitakuwa chini ya usimamizi wa mkulima mwenyewe. (*Makofi*). Na kwamba Mmlaka haya tuliyoyaunda, ama yarejee yafanye kazi zao za biashara ya nje kama zamani ama yasaidie katika uzalishaji (*Makofi*).

Lakini, Ndugu Mwenyekiti, ushauri wangu binafsi juu ya suala hili la mapato yetu kutolingana na matumizi ni kwamba tungepanda tupunguze; na neno la kupunguza siyo sahihi, ni ku- *freeze*; ndilo neno ninalotaka kulitumia-uongezekaji wa wataalamu wasiohitajika katika serikali na katika mashirika mpaka hapo hali yetu ya uchumi itakapokuwa nzuri. (*Makofi*).

Sasa hivi, Ndugu Mwenyekiti, sina tawimu sahihi lakini nahisi watu warioajiriwa na serikali na mashirika pengine wako karibu 400,000 au 500,000 sina hakika, lakini ni watu wengi sana. Wataalamu hao kama wangetumika vizuri; kwa kweli hali ya kilimo chetu na mifugo yetu, uvuvi wetu, misitu yetu isingekuwa kama ilivyo hivi leo.

Vile vile ushauri wa pili, Ndugu Mwenyekiti, ni namna ya kufikiria namna ya kuwapata wataalamu wanaohitajika kwa siku za usoni. Kama tulivyokwisha kusema katka vikao vingi vya Chama, vijiji ndivyo vitovu vya maendeleo ya Tanzania na kule ndiko wanakohitajika wataalamu walio bora sana. Hili ni pambano kubwa, maana vijijini hakupendeki sana ingawa kwa Tanzania hali inaanza kubadilika. Lakini hakuna watu watakaogeuza hali duni ya

maendeleo ya vijiji vyetu, isipokuwa wataalamu walioelimishwa na jasho la wakulima wenyewe.

Kwa hiyo, ningeshauri wataalamu walio bora kabisa na wenye tabia njema ndio wangekwenda kukaa vijijini na hasa katika kazi za uzalishaji mali. (*Makofi*).

Vile vile sina hakika, Ndugu Mwenyekiti, kwamba hatuna vyuo vingi. Pengine tuna vyuo vingi vya kuwazalisha wataalamu wengi kila mwaka na pengine wasiohitajika huko vijijini au hata katika mashirika. Suala hili nalo lingetizamwa.

Maoni yangu Ndugu Mwenyekiti, ni kwamba pengine mtazamo wa lengo letu kwa baadae ni kwamba tuwafundishe wataalamu wachache ambao watakwenda kuwafundisha wakulima na wafugaji wenyewe huko vijijini. Badala ya kuzalisha malaki ya wataalam tuwageuze wakulima na wafugaji wawe ndio wataalam wenyewe na kwa hivyo tutawahitaji wataalam wachache zaidi. Na wakulima wenyewe na wafugaji wenyewe ndio watakuwa wataalam katika kazi wanazozifanya. Na hapa ningezidisha kidogo Ndugu Mwenyekiti, kwamba wakulima wetu wengi huko vijijini ni kina mama, na wafugaji wengi ni kina mama. Kwa hivyo katika suala hili la mafunzo ya wakulima huko vijijini suala hili tungeanza kutiliwa mkazo. (*Mkofi/ Vigelegele*)

Ndugu Mwenyekiti, vile vile ningependa niseme kwamba tumepiga hatua kubwa katika maendeleo ya taifa letu na katika Chama chetu. Lakini Ndugu Mwenyekiti, Chama chetu tunakiita ni Chama cha Wakulima na Wafanyakazi. Sisemi kwa kulaumu lakini nasema ndio hatua za mwanzo, lakini Ndugu Mwenyekiti, walio wengi katika uwakilishi katika Chama chetu ukiacha ngazi ya shina na labda tawi lakini ukianzia wilaya, mkoa na hata taifa utakuta kwamba wote ni wasomi. Hili hatulipendi sana. Kwa sababu gani Ndugu Mwenyekiti, vyama hivi vina wenyewe na tuna maslahi tunayolinda. Kwa bahati njema tumebahatika chini ya uongozi wako kuzuia kusiweko na tabaka kubwa katika jamiii ya Kitanzania. Lakini tungependa katika uwakilishi ujao katika Bunge hata katika

mkutano mkuu wa Chama wawakilishi walio wengi wawe ni wakulima na wafanyakazi wenyewe. (*Makofi*)

Ndugu Mwenyekiti, katika Mwongozo wa Chama Chetu, mwongozo wa TANU wa mwaka 1971 tulitamka wazi wazi kwamba wataalamu si wanyapara wa wakulima na wanyakazi. Lazima waende wawasikilize wanachotaka na kisha wawapangie yale wanayoyataka. Na sisi tutafaidika sana kiserikali, katika Bunge kama mawazo yanayotolewa yanatoka kwa wakulima wanaoshika jembe kwa mikono yao na wafanyakazi wanaovaaa *over*- roli kuliko wasomi watupu. (*Makofi*). Kwa bahati mbaya, Ndugu Mwenyekiti, hili ni tatizo la dunia yote nzima. Viongozi katika vyama vyote duniani, ziwe nchi za kibepari, za kijamaa walio wengi ni wasomi. Lakini ni kazi ya uongozi, lakini ya uwakilishi lazima uwe wa wenyewe.

Jambo lingine ambalo ningependa niseme, Ndugu Mwenyekiti ni kuhusu kilimo ambacho umeikazia vizuri sana pengine kuliko wakati mwingine wowote. Tangu Azimio la Arusha mwaka 1967, suala hili ulilitamka na shirika la chakula duniani, Ndugu mwenyekiti, miaka miwili mitatu iliyopita walikupa heshima ya kuwa mkulima bora katika nchi za dunia ya tatu nafikiri walikupa kwa niaba ya watanzania wote.

Suala la kilimo hatujawahi kulisahau lakini nafikiri sasa tutatilia mkazo kuliko tunavyofanya wakati mwingine wowote huko nyuma. Jana ulitumia maneno ya kusema “mwalimu mmoja wa zamani aliwaambia wanafunzi wake kwamba ukweli utawakomboa” Nafikiri kwa hivyo ungeweza ukatuambia kwamba kujitosheleza kwa chakula kwa watanzania, vile vile kutatukomboa na kulinda uhuru wetu

Isipokuwa Ndugu Mwenyekiti ningependa niseme nini yatatokea kutokana na hotuba yako hiyo kama tumekubali kutoa umuhimu zaidi kwa kilimo kuliko tulivyofanya huko nyuma. Mpaka hivi sasa Ndugu Mwenyekiti, utaratibu wetu katika kuliendeleza taifa letu kwa kilimo kwa viwanda na kwa fani au sekta zingine mbalimbali

ulikuwa ni wa kugawa fedha kwa mikoa mbali mbali bila kujali mikoa inayoweza kuzalisha zaidi. Yaani tumekuwa tunafuata *extensive approach* na sasa lazima tuanze kuchagua maeneo na Mkutano huu Mkuu wa chama lazima ukubali kwamba hiyo ndiyo mbinu inaweza kutusaidia kujitegemea kwa chakula haraka. Baada ya kusambaza nguvu zetu zote za fedha na vyombo vya kazini na wataamu tungechagua mikoa michache yenye uhakika wa mvua na tukaweka nguvu zetu pale. (*Makofi*). Na hili nasema ni kwa fedha, wataalam, pembejeo na kadhalika. Mikoa mitatu au hata minne ya Tanzania kama tukitilia juhudi kwa muda mfupi nina hakika kubwa tukajitosheleza kwa chakula.

Ndugu Mwenyekiti, jambo lingine katika suala hili la kilimo. Mara nyingi huwa binafsi naona kama tunalifanya kama ni suala jepesi mno. Lakini kilimo katika nchi za joto kama Tanzania na kwingine katika Afrika ni vigumu sana kuleta mapinduzi ya haraka ya kilimo. Na sababu zake zipo kwamba mvua zake haziaminiki, udongo wake si mzuri sana. Kuna wadudu na wadudu wa kila aina. Juzi juzi bungeni tulikuwa tunasikia scania huko Tabora, sijui vifaru huku Pwani na kule kusini wadudu wa aina gani. Na hata ukishavuna ndani ya ghala na bado una matatizo.

Kwa hivyo, ni vizuri tujue kwamba katika suala la kujitegemea kwa chakula tunahitaji kupata teknolojia na msaada kwa nchi za kirafiki ili tuweze kufikia lengo kwa haraka na mapema zaidi.

Lingine Ndugu Mwenyekiti, ambalo ningependa kusema ni juu ya mifugo na nitasema kwa kifupi. Suala la kupunguza, kwanza tunashukuru ulizindua mawazo ya kitaifa Mwaka jana katika kuweka sera ya mifugo. Na tunashukuru ulituwekea wizara. Vile vile chama kimezungumza kwa muda mrefu suala la kupunguza mifugo kwa asilimia 10 kila mwaka. Maelezo nafikiri yameshatolewa kila mahali na wenyewe tumeona, tulihisi hapo mwanzo kwamba wakoloni walipokuwa wakizungumza juu ya suala la kupunguza mifugo walikuwa wanataka tuwe maskini. Lakini sasa kwa kweli tuna amini kabisa kwamba hakuna njia ya kutunza mazingira ya ardhi yetu isiharibike, hakuna njia ya kutumia

mifugo kama mali isipokuwa kwa kukubali kupunguza mifugo yetu kwa ajili ya maendeleo ya wafugaji wenyewe, maendeleo ya taifa lenyewe na vile vile kwa ajili ya kutunza mazingira yetu.

Kwa hivyo, suala hili Ndugu Mwenyekiti tungependa litizamwe na serikali na uwezekano sasa wa kuweka kasheria na hasa kwa maeneo yaliyo na mifugo iliyo mingi sana ili upunguzaji huu uanze kufanywa. Jambo kubwa lazima tutafute masoko. Sasa suala hili Ndugu Mwenyekiti lina tatizo. Tuna ng'ombe milioni 12, mbuzi sijui kiasi gani. Lakini hatuna soko. Juzi mkataba uliotiwa saini tunasikia tena umefutwa. Lakini kama tungeweza kuuza kama ng'ombe laki moja kwa mwaka ambayo ni sehemu ndogo sana, idadi ya ng'ombe tuliyonayo hata kwa dollar 500 hapo tunaweza kupata dollar 50,000,000 hizo sio pesa kidogo. Malalamiko haya ya kukosa madawa ya mifugo naamini yangekwisha na mifugo ingetoa mchango mkubwa sana kwa maendeleo ya taifa letu. Sasa soko sijui tupate wapi. Waingereza, rafiki zetu tulioshirikiana nao zamani sijui kwa nini wanapokea nyama kutoka kwingine bila ya nyama kutoka Tanzania. Kwa kweli tunahitaji soko. Kama tungekuwa na soko la Afrika lingekuwa vema. Lakini lazima tupate soko ili rasilimali hii iweze kutumika vizuri

Hali kadhalika, ndugu Mwenyekiti, juu ya suala la wanyama pori. Na hasa katika Mkoa wa Arusha. Inaoneka kanuni ile ya Msayansi Dar-win kwamba wanyama watajichagua na kufa wenyewe. Wale walio na nguvu wataishi na wale dhaifu watakufa, sijui nani anayewapa huduma kiasi hicho maana siku hizi nao ni kama binadamu na mifugo wanazidi kuongezeka tu. Na ardhi inazidi kuharibika. Na mipango yetu ya kuwavuna wala si sawa kui-ita ni mipango maana juzi nilikwenda kusimamia katika eneo moja la Monduli, mahali waliokuwepo nyumbu na punda milia kwa maelfu labda elfu kumi lakini waliuawa 100. Lakini malisho na eneo na eneo lote limekuwa jangwa. Siju tunataka tuiharibu nchi yetu kiasi gani. Wana maeneo yao tunakowahifadhi lakini hao wa ziada wanaokwenda nje wanaozidi katika maeneo yao lazima nao tuwatizame kwa lengo la kuhifadhi mazingira yetu.

Ndugu Mwenyekiti, Suala lingine nitasema kwa kifupi sana ni juu ya suala ulilosema jana la watu waliosongamana. Na ulitaja sehemu na sina haja ya kurudia. Mimi ninataka nijibu kidogo hoja zilizokuwa zinatolewa na baadhi ya wajumbe waliokuwa wanasema watu wasiokuwa na kazi au hao watu waliobanana, tuwatengenezee utaratibu maalum kabla ya kuwahamisha.

Ndugu Mwenyekiti kwa hao watu waliosongamana wapo watu aina mbili. Wako watu wasiojiweza kabisa. Hawa wanahitaji msaada na maandalizi kabla ya kuwahamisha. Lakini vile vile wapo wengi walio na uwezo ila hawana ardhi. Hawa wanachohitaji ni kupewa ardhi, kuelekezwa wapi na watakwenda wenyewe. Na nasema kama tukisema swala hili lisitekelezwe mpaka tuwe na mipango maalum maana yake tunarudi katika mawazo yale yale ya mwanzo ya *re-settlement scheme*. Lazima utaratibu wetu uwe tofauti.

Ndugu Mwenyekiti, mjumbe mmoja wa Tabora, jana alizungumzia juu ya wafugaji kutoka usukuma na vile vile ningependa kusema kutoka mkoa wa Arusha ambao wanahama wenyewe mwaka hata mwaka bila ya kuigharamia Serikali wala Chama hata senti moja. Wanapoona matatizo yameingia mahali, wanajiondokea wenyewe. Matatizo yetu ni kwamba kule waendako huenda hawafanyiwi mipango. Hili nalo ni tatizo, lile lisingetuweka gharama kubwa kama waendako wapewe ardhi kusudi waweze kufunga na kufanya shughuli zao za kilimo.

Ndugu Mwenyekiti, juzi tumezungumza vile vile suala hili la kila mtu kufanya kazi na ningependa niseme kwamba sasa hivi Tanzania huwa tunasema na Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa (ILO) kwamba Tanzania ina utaratibu wa kuwalazimisha watu kufanya kazi *forced labour*.

Ndugu Mwenyekiti, nafikiri wenzetu hawajatuelewa, sipendi kuwasema sana kwa sababu taarifa zao nyingi juu ya Tanzania mara nyingi huwa ni sahihi isipokuwa kwa suala hili. Sisi tunachofanya ni kumwambia mtu ajitegemee, hatumlazimishi aende kuwa mtumishi wa serikali au kwenda kufanya kazi shirika la umma. Ni

kwenda kujifanyia kazi mwenyewe ya kujitegemea katika maisha yake. Tofauti hii lazima waifanye kabisa. Na hapo tutakapoanza kutekeleza suala hili la kila mtu kufanya kazi tunaweza vile vile tusieleweke. Lakini tungependa waelewe kwamba tunataka watu wetu wajitegemee si kuwa wafanyakazi wa watu wengine. (*Makofi*)

Lingine, Ndugu Mwenyekiti, ni hili nililosema juu ya suala la malezi ya watoto. Nilisema ni rahisi kuzaa kuliko kulea. Hili limesemwa vile vile katika hotuba yako na juzi huko Zanzibar umelizungumzia vizuri. Lakini bado inaelekea tunasema kwa haya kidogo juu ya suala hili. Ningefikiri kikao chako hiki cha chama, mkutano mkuu ungelipokea suala hili la malezi ya watoto na suala la kuzaa kwa majira kama ni sehemu ya sera ya serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Ndugu Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu mipango mingi inavurugika kwa sababu ya uwingi wa watu wanaozidi lakini wanaohitaji huduma. Kwa hiyo lazima tuwe na sera ya kutuongoza katika suala hili.

Sasa lingine, Ndugu Mwenyekiti, ni hili la utekelezaji ambalo linahusu uongozi na ambalo umelisema vizuri sana. Mimi ningependa hili kwa kifupi. Kwamba katika uteuzi Ndugu Mwenyekiti, mradi tumetambua tatizo letu la utekelezaji, ujitahidi sana kwa kutumia vyombo vinavyokushauri kuwatia watu ambao ni hodari katika usimamizi wa utendaji wa kazi. (*Makofi*).

Pili, Ndugu Mwenyekiti, mara nyingi umetuambia katika vikao mbalimbali kwamba zipo aina mbili za serikali. Serikali zilizo *soft* na serikali zilizo *tough*. Baada ya maamuzi kufikiwa katika vikao, kinachobakia kiwe ni utekelezaji na sheria zilizopo zitumike. Mahakama, Polisi na vyombo vyote vya utekelezaji vifanye kazi. (*Makofi*). Na kama watakosea, tumeweka njia nyingi za kuweza kurekebisha mambo haya lazima tuamue kuwa *tough* katika kusimamia utekelezaji wa maamuzi yetu. Ndugu Mwenyekiti, ningependa niongeze maneno mengine mawili kabla ya kumaliza.

La kwanza ni namna ya kutekeleza maazimio hayo yatakayopitishwa na Mkutano huu Mkuu na hata mwongozo wa chama wa mwaka jana ambao tumezungumzia lakini utekelezaji wake bado haujaanza rasmi

Ndugu Mwenyekiti, nilikuwa na mawazo mawili kwa suala hili. Kwanza kwa nchi changa kama yetu hatuwezi kukwepa kabisa kuwa na matatizo ya ghafla ya mara kwa mara. Mara dizeli inakosekana wakati wa kulima mara madawa ya mazao yanakosekana au ya mifugo yanakosekana. Na kwa hivyo, nilihisi ili kuweza kutekeleza mambo yetu vizuri ama kwa utaratibu wa sheria ama kwa utaratibu wa ki-utawala, tungekuwa na kamati ya kusimamia mambo ya dharura.

Pili, Ndugu Mwenyekiti tumekuwa tunafanya mabadiliko mengi, si mabaya na baada ya muda tunarejea nyuma huko tulikotoka. Mfano mfupi ni suala la kuvunjwa kwa Vyama vya Ushirika, na kuanzishwa kwa mamlaka za mazao, suala la kuvunja Town council na District Council tukawa na mfumo mmoja tu wa kiserikali. Lakini baada ya muda tukarejea tena kule tulikotoka. Ningefikiri vile vile Ndugu Mwenyekiti, ili tutokane na tatizo hili kwa siku zijazo ni vizuri tungekuwa na board ya utafiti-*Research/controller Advisory Board* ambayo itasaidia serikali kufikia maamuzi yake kabla ya kufanya maamuzi rasmi. Kwa sababu gharama za kuresjesha serikali za miji, gharama za kurejesha serikali za mitaa, gharama za kurejesha *cooperative* ni kubwa mno. Na pengine sipendi kusema sana lakini limetupotezea muda mrefu katika kipindi cha hapo katikati.

Sasa jinsi nchi inavyokomaa ndivyo inavyoweza kutizamia matatizo yake kabla hayakutokea, nafikiri kwa njia hiyo, pengine tunaweza tukakwepa kufanya yale maamuzi uliyoyasema jana, ni maamuzi ya jukwaani. Ya kuamua kwamba leo tumeamua tunafanya. Tuamue mambo kutokana na utafiti na ushauri uliofanywa baada ya kujua nini na nini kinachoweza kutokea. Faida na hasara ya kitu hicho.

Mwisho, Ndugu Mwenyekiti ningependaa niseme juu ya suala hili la uchumi tulilonalo na kukumbusha kidogo suala tulilokubaliana katika Mwongozo wa Chama wa 1971 nalo ni suala la utaratibu wa Watanzania kujiwekea akiba. Kila nchi Ndugu Mwenyekiti, lazima iwe na utaratibu wa namna ya kupata fedha ya kuweka mahala kama NPF ya wafanyakazi inavyosaidia serikali na vyombo mbali mbali katika suala la fedha na kwa ajili ya kuweka katika miradi ya maendeleo. Ndugu Mwenyekiti, sisi ni watu masikini lakini bado tungeweza tukaamua kwamba kusudi tuweze kujiwekea nguvu ya kujenga kilimo cha kisasa katika Tanzania, kujenga viwanda vya kujitosheleza vinavyohusiana na kilimo cha Tanzania. Tungeweza kabisa tukasema ama chama kinaamua walao kila mfanyakazi, kila mkulima angeweza akakatwa asilimia tatu au hata tano ya mshahara na ikaingia katika suala la akiba au katika kununua dhamana za serikali.

Kwa njia hii tunaweza tukajiwekea fedha kwa ajili kujijengea viwanda na kuendeleza nchi yetu.

Mwisho, ndugu Mwenyekiti ningesema kwamba umelivusha Taifa letu katika matatizo mengi. Hupendi kusifiwa wala hatuko hapa kukusifu. Lakini matunda tunayofurahia leo sisi katika Tanzania na wenzetu walio wengi katika Afrika ni uongozi wako mzuri. Kwa kweli lazima tukiri kwamba hiyo inatokana na juhudi na hekima zako. (*Makofi*).

Sasa hivi, inchi changa ziko katika matatizo, ya namna ya kuendelea na kutokana na masharti magumu wanayopewa na shirika la fedha la kimataifa. Ndugu mwenyekiti, mimi nafikiri,chini ya uongozi wako na chini ya maamuzi ya Mkutano huu Mkuu wa chama bado tunaweza tukaamua tusiyumbishwe na tukaendelea kutegemea siasa yetu ya ujamaa na kujitegemea na kupokea misaada ile ambayo haivunji misingi yetu na imani zetu katika chama chetu na chini ya uongozi wa Ujemedari wako. Nina hakika vita hivi vya kiuchumi tutavishinda. Ahsante Sana. (*Makofi na vigelegele*)

# SURA YA TANO

## Jitihada Zetu Zilenge Kujitoa Katika Hali ya Uchumi Tegemezi[6]

***Julius K. Nyerere***

*Mwezi Mei 1989 kulikuwa na semina ya wazalishaji wakubwa ambayo iliandaliwa na Chama cha Mapinduzi ili kubadilishana mawazo juu ya maswala mbalimbali. Semina hiyo ilikuwa chini ya Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mwalimu Julius Nyerere. Katika hotuba yake ya kufunga semina, Mwalimu Nyerere aligusia mambo mengi ikiwemo suala la ujenzi wa uchumi wa kitaifa, na nafasi ya sekta ya umma na binafsi ya kizalendo katika ujenzi wa uchumi wenye sura ya kitaifa. Sehemu ya muhtasari wa hotuba hiyo unaelezea mawazo hayo ya Mwalimu Nyerere ….*

[…]

Ninalosema karne ya 21 bado kuna miaka 11 tu inakuja, tatizo letu la msingi ni la nchi za Kusini zote. Nalo ni hili, uchumi wetu una sifa mbili. Sifa ya kwanza ya uchumi, duniani; uchumi huu unapitanapitana. Uchumi wa Tanzania ni tofuti na uchumi wa Brazil au wa India au wa China au hata wa Zimbabwe. Na huu ni uchumi duni kwa maana mbili. Maana ya kwanza, […] maana ya hali halisi ni kwamba ukienda kwa mfano tu, sisi tunalima kwa jembe la mkono, tunatumia mikokoteni. India, mpaka leo, wanatumia mikokoteni ya ng’ombe, pale New Delhi ziko sekta utazikuta ni sekta za maendeleo lakini ni uchumi wa namna hii, nasema ni duni kwa namna hii. Namna ya kwanza ni hiyo hiyo ni kweli kwa sababu bado kuna shughuli nyingine zinafanywa katika hali ya nyuma kabisa.

---

[6] Gazeti la *Mzalendo* ; Jumapili Mei 21 1989.

Pili, uchumi duni kwa kulinganisha na wenzetu wa Kaskazini. Ukitazama sisi na ukitazama uchumi wao, uchumi wetu uko nyuma. Sifa ya kwanza ya uchumi wetu ni duni, hii sifa ya uduni ni mbaya lakini si mbaya sana hii, inawezekana likawa ni kama la kawaida. Kwa nini? Kwa sababu kama kuna duni kule ni uchumi ulioko nyuma, kama maana yake ingekuwa uchumi mchanga, uchumi ambao haujakomaa. Juzi nilitumia mti, mti mmoja umepandwa ni mkubwa umestawi na ndege wa anga wanakuja mle wanastawi. Mti mwingine wa mbegu ile ile umepandwa lakini bado ni mdogo lakini wa aina ile ile na bado unakua.

Sasa unaweza ukawa na mti huu umekomaa, huu bado lakini ni mti. Hali yake ni nzuri tu, upe muda na kuumwagia maji na siku moja mti huu kwa namna yake utakuwa imara na kuanza kutoa matunda. Kwa maana hiyo, uduni huo ni uchumi uko nyuma isingekuwa mbaya kama ingekuwa sifa hiyo peke yake tu tungeweza kuutilia mbolea uchumi ule utabadilika.

Lakini uchumi huu una sifa ya pili, ni uchumi tegemezi. Ni uchumi unaotegemea Kaskazini, tena sifa ile ya kutegemea inaupa ugonjwa. Kwa hiyo, utegemeaji ule ni kama maradhi; maradhi hayatokani na uduni peke yake, maradhi, hasa ya uchumi wetu ni ule utegemezi wake kama [..] hivyo, ni duni tu kwa maana ya uchumi mchanga, haujakomaa lakini una afya. Ni sawa na mtoto, unakua tu, lakini ni uchumi tegemezi. Ni ugonjwa. Ni kilema. Ni uchumi kilema.

Safari moja jeshi letu nadhani lilikuwa likiadhimisha miaka 20 ya kuanzishwa jeshi. Kama *Commander-in-Chief*, nilikwenda pale uwanjani na jeshi letu lilipitisha silaha zake na zana za vita. Zilikuwa nyingi, gwaride zuri, nikaziona zote – zote zinatoka nje, zote kabisa. Leo siku ya kujivunia kidogo, jeshi letu limetimiza miaka 20. Kwa hiyo ni siku ya kujivuna, lakini hii paredi, tunaparedi nini? Hatuparedi jeshi, tunaparedi biashara. Huwa ni gwaride la namna hii. Tangu hapo huwa natembea nakwenda kwenye nchi za ndugu zetu, siku zingine nakaribishwa nayaona maparedi hayo hayanivutii, isipokuwa yanavutia kwa ufanisi wa Kaskazini wa kuvuta pesa za maskini hawa wa Kusini.

Kwa hiyo, kama unatazama magwaride ya kijeshi, kama unatazama viwanja vya ndege, sisi hatuna ndege nyingi sana, lakini hata Dar es Salaam nenda uone ndege ziko pale. Hata Dar es Salaam utakuta ndege pale. Magwaride ya majeshi, viwanja vya ndege, hata nchi zenyewe ziwe zina mali nyingi kama vile nchi zenye uwezo wa kutoa mafuta, utakuta zimejaa tele viwanja vya madege makubwa makubwa ya kila aina.

Mabarabara yetu katika nchi za Kusini yamejaa magari tele, ikiwa ni pamoja na Dar es Salaam. Kwa baadhi ya nchi zingine, hata bidhaa madukani, maduka yamejaa tele – zimetengenezwa wapi? Yote hayo kama magwaride, kama ni viwanja vya ndege, kama magari, kama ni bidhaa madukani nasema kwa baadhi ya nchi fulani fulani hata kama ni Coca-Cola ni maonyesho, ni magwaride ya utegemezi kote katika nchi zetu.

Kwa Coca-Cola, kwa sababu Marekani wao wana nguvu sana kwa Coca-Cola, Marekani sasa anataka wote tuwe ni wanywa Coca-cola. Ndugu [Mengi] mkipenda msipende, mtatuuzia tu Coca-Cola basi Coca-Cola inauzwa tu.

Sasa uchumi wetu basi ni uchumi tegemezi. Uchumi wa nchi zetu hizi zote una sifa hizo mbili. Hili tatizo letu kubwa la msingi. Uchumi wetu ni uchumi duni, lakini uduni peke yake si kitu sana, lakini tatizo kubwa kabisa kabisa ni uchumi tegemezi.

Kwa hiyo tunajivunia ule ugonjwa… tunajivunia ule ugonjwa wala hatuuonei haya… unaparedi silaha za wakubwa, unaparedi madege ya wakubwa, unaparedi bidhaa za wakubwa, unaparedi ma-Coca-Cola ya wakubwa na unajivuna tu, unasema sisi tumeendelea. Ukimwambia umeendelea kwa nini atakwambia njoo uone barabara yetu.

Sasa nasema hilo ndilo tatizo letu la msingi watu wote – nchi zote za Kusini na hapa tujenge uchumi. Pamoja na kwamba uwe ni uchumi haulingani na wa wakubwa lakini ni uchumi unaokua.

Kwa hiyo jitihada zetu ziwe ni kujitoa katika hali hii hasa sifa hii ya pili. Kwa sababu bila kuitoa sifa hii ya pili ni vigumu sana kupambana na sifa ya kwanza. Kwa nini? Kwa sababu katika nchi kama Tanzania…, Tanzania si mfano mzuri sana lakini upo, zipo sehemu mbili. Acha ile Ndugu Idi Simba alikuwa anasema '*informal sector*' na '*formal sector* '. Ipo tunayo sisi hapa na zipo katika sehemu zetu zote.

Tunao uchumi tunaweza kuuita wa kisasa. Uchumi wa kisasa ni ule uchumi uliochuma. Uchumi wa kisasa katika nchi hizi ni wa kigeni. Kwa hiyo, Coca-Cola, chombo cha kigeni ni mtambo unapokea tu pale.

Eh! Yuko Mhindi mmoja Kiswahili chake kilikuwa kizuri sana kuliko cha Babu Patel, aliniambia: ''Mwalimu ee wewe sema nakwishakata mirija, lakini bomba je kwishakata?'' Sasa mabomba… sasa uchumi wetu ule wa kisasa ni wa mabomba, mwanzo wake huko nje. Utazameni wote. Utazameni. Ni wa mabomba, na madhali hii sekta '*modern*' ni ya mabomba, hii sekta '*modern*' hii msingi wake ni nje, ni tegemezi si yako. Ni vigumu kwamba '*modernisation*' ya [ya] sekta nyingine ambayo si '*modern*' itatokana na nguvu yako, itatokanaje na nguvu yako? Si yako hii sekta '*modern*', si yako hii.

Hivi upewe na Marekani kiwanda chake cha Coca-Cola hapa halafu ukiendeshe kwa madhumuni yako? Ndivyo kweli kwa kitu kingine chochote mtakachokubaliana naye umwendeshee hapa Tanzania kwa masharti yake, mnamwendeshea chake kwa masharti yake kwa faida yake. Sasa nasema hilo ndilo tatizo namba moja kwa nchi zetu.

Na nchi zote tunazosema, zote ziwe za kibepari ama za kijamaa, madhali tatizo hili ni la kawaida kwao, hazina budi zipambane nalo. Ni yao yote ikiwa ni mabepari, wakiwa wajamaa ni tatizo. Na kweli, tatizo la nchi ni tatizo linawahusu wote.

Nyingine nasema lazima tushirikiane. Nasema kushirikiana humu si rahisi. Sasa mimi wenzangu nadhani tutafanya mapendekezo. Mapendekezo yetu katika kupambana na tatizo hili na msingi

mmoja ni umoja. Ninasema tunaona jinsi tutakavyofanya na tutaiambia kila nchi tumieni uwezo wenu wa ndani wote kwa ajili ya maendeleo. Hapana kukimbia. Mnatoka nje haraka haraka kabla ya kuonekana uwezo wenu wote wa nyumbani unapatikana. Lakini tutasema vilevile tumieni kikamilifu ushirikiano wenu kwa ajili ya maendeleo.

Tukitaka sisi washauri tutakwenda nje, tunaletewa wabovu zaidi kuliko hawa, wengine wamefundishwa na hawa hawa. Sasa tumieni watu wa nyumbani hapa. Tumieni kikamilifu uwezo wenu wa ndani. Pili, kama nyumbani hawapo uliza Kenya – vunja hii kasumba yako hii, uliza Kenya, uliza Uganda, uliza Zimbabwe, uliza Malawi, potelea mbali. Kwa sababu katika hii lazima tushirikiane wote… Uliza Malawi. ‘‘Tunataka mtaalamu wa aina fulani hivi, hamna hapo mtaalamu huyu?’’ Uliza Malawi, uliza Zimbabwe, uliza Msumbiji, kama huna uliza sehemu nyingine Afrika. Hakuna. Uliza India. Hata hii akili tegemezi kwamba India ni nchi yenye nguvu za nyuklia kwamba haina washauri ambao wanaweza … kukusaidia nyie hapa. Huu ni ukoloni. Nasema tutapendekeza hilo hapa.

Kwanza tumieni kikamilifu uwezo wetu wa ndani kujitegemea. Pili, tumieni kikamilifu uwezo wenu wa ushirikiano katika ngazi mbalimbali. Nchi mbili, nchi tatu, nchi nne. Fanyeni hivyo na muuone utegemezi kuwa ni adui. Muuone hivyo na muupige vita, hivyo msiufurahie, mnafurahia maradhi. Mnafurahia ukoloni. Sasa nasema hii si rahisi. Kwa nini nasema si rahisi? Labda nitalisemea nitakapofika katika sehemu yetu ya pili.

Dunia imegawanyika hivyo sehemu ya wakubwa wana nguvu za uchumi na wanaitumia kuendeleza nguvu hizo. Nilisema Ndugu Kaunda alijaribu kuacha Coca-Cola nikamwambia: ‘‘Sasa utafanyaje?’’ Alisema: ‘‘Mwalimu, tunaanza mtambo wetu pale wa vinywaji vya nyumbani, unaweza kufanikiwa.’’ Nikamwambia: ‘‘Ken, huwezi… huwezi kwa sababu wako Wazambia pale watakuletea taabu kweli kweli.’’ Nimeambiwa jana kwamba nadhani sasa Coca-Cola watarudi. Wamesharudi kwa sababu sasa mapambano hayo dhidi ya ukoloni mamboleo si rahisi. … ni

magumu zaidi kuliko mapambano dhidi ya ukoloni kwa sababu tulipokuwa tukipambana na ukoloni ilikuwa ni rahisi zaidi kuunganisha nguvu za ndani. Ilikuwa rahisi vilevile kwa nchi changa kushirikiana. Kwa Tanzania kushirikiana na India; TANU kushirikiana na KANU, kushirikiana na Indian Congress, kushirikiana na UNIP, kushirikiana na African Congress. Tulikuwa tunaweza kufanya kazi pamoja na marafiki bila tatizo, lakini sio sasa.

Sasa niiache hii niende haraka haraka. Nasema hili ni tatizo letu. Kwa hiyo tatizo la Tanzania ni hilo na pia ni la wenzetu wote; uchumi wetu ni duni kwa maana zote mbili. Kama nilivyowaambia juzi, tungeweza kulima kwa ng'ombe tungekuwa na maendeleo makubwa sana. Kwa hiyo, uchumi wetu uko nyuma, wenzetu wako mbali. Sisi tuko nyuma, uchumi wetu ni tegemezi. Ni uchumi tegemezi. Lazima tuutoe katika hali hii ya kuwa uchumi tegemezi. Na katika hali hii ya kwamba tunataka uchumi wa Tanzania uwe uchumi unaojitegemea ndio lazima wote tuwe pamoja kwa sababu tunamkabili mtu wa nje. Hii haina itikadi, ni uzalendo tu.

Wajapani wanaulinda uchumi wao. Wanaulinda kwa mbinu za ajabu ajabu, na washindani wao wa Kaskazini, wengine hata hawazijui mbinu hizo. Wajapani, anakwenda kwenye mkutano, wanaambiwa: ''Lakini ninyi Wajapani namna gani, soko lenu gumu sana kuliingia.'' Wanasema: ''Tutajaribu kuona njia za kuweza kusaidia saidia.'' Wanakwenda, sijui wanafanyafanya mambo yao huko, inabaki ngumu.

Wajapani mnauza magari mengi sana katika nchi yetu, hapo Mjapani anacheka kimoyomoyo: 'Ah! Si mmesema tushindane bwana? Kwani tunayaleta kwa nguvu, si watu wenu wanayaagiza?' Lakini namna yalivyokuwa rahisi kuliko hayo ya Uingereza, kuliko hayo ya Ujerumani, kuliko hayo ya Ufaransa, kuliko hayo ya Mmarekani, Mjapani anajua mwenyewe ni madhubuti kweli kweli, lakini ziko njia nyingine ndio… ndio… lakini si bepari yule? Kwani katika jambo hilo la kusema biashara ya Japani lazima iwe ya

Japani, huu ni uzalendo. Kwa hiyo, nchi ya kijamaa inasema hivyo, na nchi ya kibepari inasema hivyo.

Kwa hiyo, sisi hapa Tanzania ***tutakaposema tunataka kiwanda cha Tanzania kiwe cha Tanzania lazima wote tuseme hivyo.*** Mimi niseme hivyo, Mengi useme hivyo, Patel aseme hivyo, Shomari aseme hivyo. Wote. Lazima iwe ni biashara yetu, lazima … lazima tujenge biashara ya Tanzania. Sisi si watoto wadogo, dunia inabadilika hii bwana. Tumesomesha watu bwana. Kulikuwa kuna wakati tunaweza kusema kijingajinga, lakini sasa tumesomesha watu wote, yani watu wote hawa tumewasomesha. Kazi yetu nyinyi mtujengee tegemezi. Sasa nyinyi mtukwamue. Ndio hamuwezi kwenda mnakwenda kwenye Benki ya Taifa tumekupanga kwenye Benki ya Taifa mnakwenda kuomba fedha katika Benki ya Taifa kusudi kutusaidia kujenga uchumi tegemezi, haiwezekani. Mtusaidie kutukwamua. Katika hiyo lazima tuungane wote. Ujumbe namba moja; Somaia unanisikia? … Ndio ujumbe namba moja, hili halina itikadi; Waingereza wanafanya hivyo, wamekuwa wakifanya hivyo.

Nyinyi wadogo mkiambiwa muungane mnasema “tunapotezwa na aliyetwambia”. Mnapotezwa; ni walewale wakubwa. ***Sasa nasema tujenge uchumi wa Tanzania. Kazi hiyo ya kujitoa katika ukoloni mamboleo tegemezi lazima mshirikiane – mabepari na msiokuwa mabepari, sekta ya umma na sekta binafsi;*** katika kazi hii lazima tufanye kazi moja. ***Tujenge uchumi wa Tanzania ambao sio uchumi tegemezi.*** Sasa ujumbe huo nadhani niubakize hapohapo.

[….]

Tutazidi kuongeza sekta ya umma na kuifanya imara. Sio dhaifu hata kidogo. Lakini sekta ya binafsi ipo tangu 1967 na kabla, sasa fanyeni kazi nzuri lakini tukabiliane na watu wa nje kwa pamoja. Mtu ambaye tutamkataa sisi ni yule ambaye kazi yake yeye ni kutufanya sisi tu ni wafanyakazi wa nchi za Kaskazini. Huyo si mwenzetu hata kidogo. Si mwenzetu, Mengi. Jifanye bepari mzalendo, tutakuunga mkono asilimia mia moja kama bepari

mzalendo. Hatutakusaidia, tutapambana nawe kama utajaribu kuifanya nchi hii koloni mamboleo kwa ajili ya mtu mwingine nje ya Tanzania. Tuelewane hivyo. Kuwa bepari, tengeneza fedha, lakini fedha hizo kwa ajili ya Tanzania – kwa ajili ya kujitegemea kwa nchi yetu – lakini tukupe uwanja wa nchi yetu uutumie kutufanya wafanyakazi wa watu wengine, hatukubali hata kidogo. Tutapambana na nyinyi mkiwa namna hiyo. Ndio maana sasa hivi tunasema waziwazi. Tujenge nchi yetu. Hatutaji, katika hali ya kujaribu kuutoa uchumi wetu katika hali hii ya ovyo, tutatumia uwezo wetu wa ndani kwa ajili ya maendeleo, ubepari na ujamaa. Tutazichanganya zote hizi kwa nguvu kabisa kabisa kujenga uchumi wa nchi yetu.

[…]

Sasa, mwisho kabisa nitasema haraka haraka. Jamani nyie katika jitihada hizi za kuanza kujitegemea kidogo, mambo machache yafuatayo tukubaliane tuyafanye. Kwanza, lazima tujitegemee kwa chakula. Lazima tuseme kwamba tutaacha kuombaomba chakula. Sasa nchi inajitegemea kwa chakula… sijui Patel zile eka zako 12,000 unalima nini? Pilipili? Lazima tujitegemee kwa chakula. Hilo liko katika uwezo wetu. Kusema kwamba Watanzania hawawezi kujitegemea kwa chakula ni uongo. Tunaweza kujitegemea kwa chakula.

Sasa tufanye hivyo basi, maana aibu sana watu wazima kuomba chakula kila siku. Na matajiri hawa hawana haya. Waswahili tunaona haya kumsimulia mtu kitu kama chakula. Kumsimulia mtu kwa chakula ni kumsemasema. Unampa chakula halafu unamsema kwamba watu hawa bwana kwao hawali. Akija kwako hapo atakaa wee haondoki, na anasikia hivyo. Sasa waswahili hawapendi tabia hiyo. Mtu unaweza kumsimulia kitu kingine chochote lakini chakula; chakula hasimuliwi mtu bwana. Lakini wenzetu hawa wakubwa, anakupa chakula huku anakusema bwana. Anakupa chakula kwanza halafu wakati uleule wanatuwekea vikwazo sisi tusijitegemee katika jambo la kilimo. Wao wanatoa ruzuku kwa

kilimo chao, wana mapesa mengi kwa hiyo vilimo vyao ni vyenye ufanisi kabisa.

Kilimo cha Wamarekani hakiwezi kushindana wakiondoa ruzuku. Waondoe; kama hodari kiasi hicho si waondoe ruzuku! Maana sisi wametuambia tuondoeb ruzuku, tumeondoa. Ndugu Rais, na wao waondoe basi maana wanajidai hodari sana hawa. Waondoe, waache kuwapa wakulima wao pesa za bure. Wakulima wao na wakulima wa Kusini tushindane tu; kama wanatuweza, waondoe kesho. Si wanajidai hodari sana. Sitaki kusema zaidi, nasema ingawa kilimo jamani, ndugu Rais, tujilishe wote hawa tunaolima, tujilishe. Hilo la kwanza, tujilishe kwa chakula; sisi tunaingia karne ya 21 bado hatujilishi kwa chakula. Majitu mazima, tumesomesha watu wengi sana, wasomi tele.

Pili, mavazi. Tulipofanya rasilimali zile kubwa katika viwanda tukasema tunalima pamba sisi. Sasa tunalima pamba, halafu pamba yetu tunauza nje. Watu wazima tunalima pamba, tunauza nje; sasa angalau tuanze kutengeneza nguo. Kwa hiyo, lengo letu la mwanzo, tulikuwa tunataka – tulitaka kutumia pamba yetu asilimia 60 ndani na asilimia 40 kuuza nje. Sasa sijui tunauza kiasi gani… Tunatumia theluthi moja, kama asilimia 30. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile hatujafikia, lakini rasilimali inatosheleza. Kwamba kama viwanda hivi vingekuwa vikitumika kwa uwezo wao wote, pengine vingesogelea hapo au hata kuvuka viwanda tulivyonavyo. Sasa ninasema katika hilo uwezo tunao. Ingawa bado uwezo wa kutengeneza viwanda vyetu wenyewe hatuna, lakini viwanda hivyo tulivyonavyo tuvitumie basi angalau tujitosheleze kwa nguo – kwa mavazi – kwa maana ya mavazi, yaani nguo zenyewe na viatu. Sisi tuna ng'ombe, tuna mbuzi; tunaendelea, watu wazima tunauza ngozi nje, ngozi hasa… tufanye hivyo, maana uwezo tunao, sio wa kutafuta, rasilimali ipo tayari… hilo tunaweza tukafanya.

Tatu, madawa, madawa… Madawa hili nalo tunaliweza bwana, hivi kweli au hata vidawa vya hospitali zetu. Ndugu Rais, kitu cha kutengeneza dawa za hospitali, maana dawa za hospitali miaka 11 kabla ya karne ya 21 bado hatuwezi kufanya hivyo? Hivi hatuwezi

kuwa na orodha maana tulitengeneza ya madawa muhimu. Nasema madawa haya kwetu sisi ndiyo ya lazima. Hatuwezi kuyatengeneza?... Tuzitengeneze sisi wenyewe hapa, tuna viwanda viwili sisi hapa. Nadhani tuna viwanda viwili au vitatu sijui vya kutengeneza dawa. Na vitengeneze ama vigawane kazi; kimoja kitengeneze dawa hizi, hiki kitengeneze dawa hizi, hiki kitengeneze dawa hizi na kile tusichokiweza tukitafutie uwezo, tutengeneze dawa zile za lazima.

Tunayo orodha ya madawa muhimu, tunaweza kutengeneza. Kwa nini kwa afya ya watu wetu vilevile tuwe tegemezi? Hata afya ya watu tunakuwa tegemezi. Vitu vidogo sana kuweza kutengeneza dawa na tunaweza kutengeneza dawa. Najua wakubwa hawapendi. Brazil wanatengeneza dawa, wamebanwa na Marekani; nimeambiwa kwamba ingawa wanatengeneza dawa karibu kujitosheleza, hii sekta ya nyumbani ya dawa hii sehemu kubwa kabisa ni ya Marekani. Lakini hata hivyo, wamekabwa na wakubwa.

Sasa dawa angalau tutengeneze. Tujitegemee katika kitu kama dawa sio kwa kila kitu lakini kwa madawa ya lazima. Tuna matatizo ya afya. Sasa hilo nalo tuendelee kuwa tegemezi? Tunauziwa unga lakini miaka 11 kutoka karne ya 21 wanatuuzia vidonge vya unga wa muhogo, sijui. Tunalisha watu wetu, wataalam, nyinyi hamuwezi kutukomboa kwa hilo?

Vifaa vya elimu… vifaa vya elimu. Mengi, si ulianza na kalamu? Sasa tuanze, tutengeneze karatasi. Leo tunatengeneza vifaa vya elimu vinatupa taabu tuna watoto wengi wanaosoma. Tuna watoto wanasoma kama milioni nne. Mimi nadhani kusema kweli tunaweza tukawa na viwanda maalum tu kwa shughuli za vifaa vya elimu. Tunaposema kwamba tunataka watoto wa shule wavae viatu, tunajua viatu vyenyewe vinapatikana wapi? Eh! hivi viatu tu, kusema viatu, sijui watu wana viwanda vyao wenyewe, sijui maduka yao wenyewe? Angalao tuseme, kwa shughuli za shule, tunatengeneza. Hivi yunifomu zinatengenezwa mahali fulani, hizi kalamu madaftari yanatengenezwa mahali fulani. Tufanye hivyo, maana kubwa jambo hili, ni kubwa kwetu; kusomesha watu wetu ni

kubwa, na uwezo tunao, sio kwamba hilo nalo tena ni kazi ya kuweza kutegemea Kaskazini. Hivi sasa ni balaa kupata madaftari katika shule zetu. Watoto hawana daftari, walimu hawana ile chaki ya kuandika.

Mwisho. Nimeyasema hayo: chakula, mavazi, madawa ya watu na mifugo, vifaa vya elimu, na spea mbalimbali. Yule Mhindi aliyekuwa akiniambia bomba ni za spea. Leo Tanzania mtu wa nchinyingine anaweza akatupa gari lake bure bure, akasema hilo gari chukua bure madhali utanunua spea kwake. Kwa hiyo matumizi yetu ya spea hapa ndiyo huyu Mhindi alikuwa akisema bomba, lile bomba… lile bomba hasa linazoa fedha zinazokwenda nje bure. Kama lazima, sawa. Kile kitu ambacho hukitengenezi na huna uwezo wa kukitengeneza na unataka agiza kutoka nje.

Lakini spea nyingi ni bure, za magari yetu, za matrekta. Hayo tungetengeneza. Ndugu Rais, nimechukua muda wenu mrefu sana na (….) matatizo.

Niwashukuruni sana.

---

[1] Nyerere, Julius 1977. *Azimio la Arusha Baada ya Miaka Kumi*; Dar es Salaam, Uk. 36.

[2] CCM 1987. *Majadiliano ya Mkutano Mkuu wa Kawaida Oktoba, 1982: Taarifa Rasmi*; Dodoma; Uk. 110.

[3] CCM 1987. *Majadiliano ya Mkutano Mkuu wa Kawaida Oktoba, 1982: Taarifa Rasmi; Dodoma*; Uk. 112.

[4] Nyerere, Julius. 1989. Hotuba Kwenye Semina ya Wazalishaji Wakubwa, Dar es Salaam Ukumbi wa IFM.

[5] CCM 1987. *Majadiliano ya Mkutano Mkuu wa Kawaida Oktoba, 1982: Taarifa Rasmi*; Dodoma; Uk. 114.

[6] CCM 1987*. Majadiliano ya Mkutano Mkuu wa Kawaida Oktoba, 1982: Taarifa Rasmi; Dodoma*; Uk. 366.

[7] CCM 1987. *Majadiliano ya Mkutano Mkuu wa Kawaida Oktoba, 1982: Taarifa Rasmi*; Dodoma; Uk. 364.

[8] CCM 1987. *Majadiliano ya Mkutano Mkuu wa Kawaida Oktoba, 1982: Taarifa Rasmi*; Dodoma; Uk. 74.